# Nipashe

Jumatatu Februari 3, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580144

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710




## Mzee mbaroni kwa tuhuma za kujeruhi mtoto akitaka kumbaka

UKURASA 4




UKURASA 13

# Simulizi mkasa wa Mwamposa

**NI** tukio la watu 20 kufa wakikanyaga mafuta, wamo wanawake 15, watoto wanne, 16 hoi hospitalini...*Endelea ukurasa wa 2 & 3*



Mwamposa

Lango la kutokea




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play · App Store


## Duni afunguka mazito kuhusu Zitto Kabwe

UKURASA 4



## W'SHARA WALIA CORONA KUSHUSHA BEI BIDHAA

UKURASA 5


**MICHEZO** SVEN AMPONGEZA MGUNDA AKIKUBALI KIPIGO CHA SIMBA UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Simanzi Moshi

Na Mary Mosha, MOSHI

VILIO, majonzi na simanzi jana vilitawala katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi baada ya matumaini ya kauli mbiu ya Mtume Boniface Mwamposa ya "mwaka 2020 wa Raha" kuwa wa vilio kufuatia watu 20 kufa na wengine 16 kujeruhiwa katika maombezi katika uwanja wa mpira Majengo.

Miongoni mwa waliopoteza maisha ni muuguzi wa Hospitali ya Wilaya ya Hai, Joyce Chamshama (58).

Kati ya waliofariki wanawake 15, watoto wanne na mwanaume mmoja, Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Salum Hamduni, aliitaja miili 19 iliyotambuliwa ni Anna Kimaro, mkazi wa Sambarai; Nancy Kawa, mkazi wa Majengo; Elias Moshi, mkazi wa Old Moshi na Catherine Macha mkazi wa Miembeni.

Wengine ni Michael Chuwa, mkazi wa Arusha Kimandolu; Funis Ngazi, mkazi Sanya Juu; Laurencia Mallya, mkazi wa Kibosho; Royal Shirima, mkazi wa Mbokomu; Basila Lyimo, mkazi wa Marangu na Elimhoo Macha, mkazi wa Mbokomu.

Wengine ni Meshark Kombe mwanafunzi Mwereni Shule ya Msingi, na Philipina Malya, mkazi wa Mlowe.

**HALI ILIVYOKUWA KABLA YA IBADA**

Katika uwanja huo kulikuwa na bango kuu la Mtume Mwamposa, katika maombezi yake 'linasomeka mwaka 2020 ni mwaka wa Raha, Mungu atakupa furaha, pumziko na starehe'.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na mkuu wa kitengo cha magonjwa ya nje na dharura wa Hospitali ya Mawenzi, Dk. Victor Adolph, juzi majira ya saa 2:00 usiku walipokea miili 20 ambapo miwili imetambulika.

Aidha, uongozi wa hospitali ya rufani ya mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi, imeomba wakazi wa maeneo na wilaya tofauti za mkoa wa Kilimanjaro kujitokeza katika chumba cha kuhifadhi maiti cha hospitali hiyo kujitokeza kutambua miili ya ndugu zao.

Watu hao walifariki wakati wa utekelezaji wa imani ya kukanyaga mafuta kama ishara ya kupata uponyaji wa maradhi, kuimarika kiuchumi, kupata mke, mume na mikosi mingine katika maisha ya kila siku.

Dk. Adolph alisema tukio hilo lilitokea Jumamosi majira ya saa 2:00 usiku katika uwanja wa Majengo Manispaa ya Moshi wakati watu hao wakitoka kwenye uwanja huo, huku wakitekeleza imani ya kukanyaga mafuta ya upako.

"Jana tulipokea miili 20, watu wawili, akiwamo mtoto mmoja walitambuliwa na ndugu zao na walihamishiwa kumhifadhiwa Hospitali ya Rufani ya KCMC, tunaomba wananchi wajitokeze kutambua ndugu zao," alisema.

Alisema watu wengi wamefariki

INAENDELEA UK. 8



Kamati ya Ulinzi na Usalama ikiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, wakitembelea eneo la tukio. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Walivyokufa wakitafuta miujiza kwa

Na Mary Mosha, MOSHI

KATIKA kile kinachoelezwa ni kwenda kutafuta miujiza kwa ajili ya kupata utajiri, kazi, ndoa na kuponywa magonjwa, waumini 20 wa dini ya kikristo wamepoteza maisha kwenye msongamano wa kukanyaga mafuta ili kupata vitu hivyo.

Aidha, watu 16 wamejeruhiwa kati yake wanne wana hali mbaya na wamelazwa hospitalini kwa matibabu zaidi.

Tukio hilo lilitokea juzi katika uwanja wa Majengo mjini Moshi majira ya saa 1:30 usiku, mara baada ya kumalizika kwa mkutano wa Injili wa Mtume Boniface Mwamposa maarufu kama Buldoza wa Kanisa la Calvary Assemblies of God, na ndipo yalipokwekwa mafuta kwenye moja ya mageti kati ya matatu yaliyokuwpo kwa ajili ya watu kupita kukanyaga na kupata haja za mioyo yao.

Katika eneo hilo ambalo vimekutwa vitambaa na kanga za kina mama, viatu na kanda mbili kulikuwa na tope jingi lililochanganyikana na mafuta ambayo waumini walikuwa wanagombania kukanyaga na kupata wanayohitaji.

**WALIONUSURIKA WASIMULIA**

"Hakukuwa na utaratibu ulioeleweka wa namna ya kukanyaga mafuta hayo, na kusababisha watu wengi kukanyagana huku baadhi walianguka na kupoteza maisha... mimi nilifanikiwa kutoka baada ya mtu mmoja kunivuta, nililaliwa na watoto wawili ambao walipoteza maisha muda ule ule,"alisema Magreti Shoo.

Alisema alijeruhiwa sehemu ya miguu ambapo alisaidiwa na baadhi ya vijana ambao wakimkimbiza katika katika kituo cha afya cha Majengo na kupata huduma ya kwanza.

"Nilipofikishwa katika kituo hicho sifahamukilichoendelea hadiusikuwa manane ambapo nilishtuka ndugu zangu wakiwa wamenizingira na huku nikiwa nimetundikiwa maji," alisema.

Agnes Lyimo ni majeruhi aliyelazwa katika hospitali ya rufani ya Mawenzi, ambaye alisema tukio hilo lilitokea majira ya 1:30 usiku ambapo Mtume Mwamposa aliwaagiza watendaji wake kuhakikisha watu wote wanakanyaga mafuta ya upako.

Alisema pamoja na maelekezo ya Mtume Mwamposa, lakini hapakuwa na utaratibu maalumu wa ukanyagaji wa mafuta hayo kama sehemu ya uponyaji wa maradhi yanayowakabili.

" Nilianguka wakati nainama kuvua viatu ili nikanyage mafuta ya upako nilimlalia mtu na sikumbuki kilichoendea hadi leo alfajiri nilipojikuta katika Hospitali ya Rufani ya Mawenzi...siwezi kunyanyuka kwa maumivu ya mgongo, huku mguu mmoja ukiwa umekufa ganzi," alisema Agnes.

Ester Rubeni, alisema vifo vilitokana na kukosekana na utaratibu maalumu katika geti la kutokea nje ya uwanja huo kupitia eneo maalum lililokuwa na mafuta ya upako.

Alisema ilikuwa ni mwenye nguvu ndiye anapita na kuwa vurugu kubwa ambazo ziliSleta maafa ya watu hao.

Baadhi ya ndugu wa marehemu, Koleta Efraimu ambaye ni babu wa marehemu Nancy Kawa, mwanafunzi wa darasa la tano katika Shule ya Msingi Langoni, aliomba

# RC: Udhibiti mafundisho yanayotesa watu kuanza

**Na Mary Mosha, MOSHI**

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, amesema wataanza kudhibiti aina zote za mafundisho ya dini yanayotesa watu kwa lengo la kuepusha madhara kutokea.

Amesema aina ya mafundisho yanayokanganya watu, yanayotoa ahadi za utajiri, kupona magonjwa na mafanikio yameanza kuna na athari mbaya katika jamii.

Aliyasema hayo jana mkoani Kilimanjaro wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tukio la watu 20 waliofariki kutokana na kukanyagana wakiwa katika ibada ya Kanisa la Calvary Assemblies of God linaoongozwa na Mtume Boniface Mwamposa.

"Tunashaka na hao watu wanaotangaza watu kupata baraka, tutaanza kudhibiti aina zozote za mafundisho yanayopotosha watu, siyo kawaida mtu anakwenda kupata baraka kwa kukanyaga mafuta," alisema Mghwira.

Kuhusu tukio la vifo vya watu hao, Mghwira alisema miili ya watu 14 waliofariki imeshatambulika na mingine bado haijatambulika.

Alisema leo mchana kutafanyika misa ya pamoja katika Uwanja wa Majengo.

"Eneo limeshawekwa salama, hakuna kitu kilichosogezwa, kila kitu kiko palepale, vitambaa vya kina mama, mafuta, tutaviacha hivyo hivyo hadi misa itakapomalizika," alisema Mghwira na kuongeza:

"Miili tutaiweka sehemu salama ya maziko, na ile mingine ambayo haijatambulika tutaiweka uwanjani kwa ajili ya kuaga na itarudishwa mochwari hadi pale ndugu zao watakapopatikana," alisema Mghwira.

Alisema Uwanja wa Majengo ni mkubwa na wasanii wakubwa wamekuwa wakifanya matamasha katika eneo hilo, lakini hakujawahi kutokea vifo vya watu kukanyagana.

Alisema kutokana na tukio hilo, Jeshi la Polisi limeshawakamata watu nane akiwamo Mwamposa.

**HABARI KITAIFA**



# Mtume Mwamposa anaswa mafichoni, waziri anena

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAKATI taifa likiomboleza msiba mzito wa watu 20 waliopoteza maisha kutokana na kugombea kukanyaga mafuta yanayodaiwa kuwa na upako mkoani Kilimanjaro, serikali imesema inalichunguza vizuri tukio hilo na itafanya marekebisho ya kisheria kwa kuangalia mifano ya nchi nyingine wamefanya nini katika udhibiti wa utoaji wa huduma za kiroho.

Kabla ya kutokea maafa hayo yaliyosababisha pia majeruhi kwa watu wengine 16 kati ya watu zaidi ya 10,000 wanaodaiwa kuhudhuria kongamano la injili uwanjani hapo, Mtume na Nabii Boniface Mwamposa maarufu kama 'Buldoza' wa Kanisa la Calvary Assemblies of God, anadaiwa kuwaelekeza waumini wake wapite katika sehemu ambapo kulikuwa na turubali lililomwagwa mafuta ili wapate nafuu ya matatizo au shida zao.

Jana, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alisema ni lazima ifike hatua kwa jambo kama hilo iwe fundisho na kwamba serikali sasa itaweka utaratibu mzuri katika utoaji wa huduma za kiroho.

"Matukio kama haya sasa yanaanza kutupa fundisho kwamba pengine hata kanuni zetu na sheria zetu hazijakaa sawa, kwa sababu huyu anakuja na sabuni anasema mkiogea matatizo yanaisha, mtakuwa matajiri, huyu anakuja na maji, huyu anakuja na mafuta, mwingine anakuja na maziwa, mwingine anakuja na hiki, lakini ni vizuri kukawekwa utaratibu.

"Na unajua hivi vibanda imani hivi vime

INAENDELEA UK. 8

# Mwamposa

serikali kuingilia kati utaratibu wa makanisa ili kuacha kuwalaghai wananchi .

" Hatutaki kuongea mengi bali inadaiwa katika uwanja huo hakukuwa na gari la kubebea wagonjwa, Shirika la Msalaba Mwekundu jambo ambalo serikali iliridhia na kuwapa kibali bila kutazama hayo ndiyo chanzo matatizo yote haya," alisema.

Naye, Hashimu Omary, mkwe wa Anna Kimario aliyefariki, alisema ipo haja kwa serikali kuchukua hatua zaidi.

Gazeti hili lilitembela uwanja huo ambao uko umbali wa kilomita mbili kutoka Stendi Kuu wa mabasi yaendao mikoani na kukuta baadhi ya mabaki ya nguo, Viatu pochi vikiwa zimetelekezwa huku kukiwa na ulinzi wa polisi.

Jana majira ya asubuhi mamia ya wananchi walifurika katika uwanja wa huo, wakitafuta baadhi ya mali zao ikiwamo funguo za nyumba zao, pochi na simu za mkononi.

Katika Hospitali ya Rufani ya Mawenzi, mamia ya wananchi walijitokeza kutambua miili na majeruhi wa tukio hilo.

# Upinzani wataka vigogo kuwajibika

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MBUNGE wa Arusha Mjini (Chadema), Godbless Lema, amesema vifo 20 vilivyotokea katika Uwanja wa Majengo-Moshi mkoani Kilimanjaro, chanzo cha tatizo hilo ni kukosekana kwa ufahamu ama weledi wa mambo yanayohusu udhibiti wa mikusanyiko.

Akizungumza jana jijini Dodoma, Lema alisema kutokana na ajali hiyo anashauri Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro (RPC), Salum Hamduni, Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Moshi (OCD), Joseph Kate, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali Simon Sirro na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene wajiuzulu.

Lema ambaye ni Waziri Kivuli wa Mambo ya Ndani ya Nchi alisema: "Mahali penye crowd (mkusanyiko) ya watu 5,000 Polisi na Zimamoto na Red Cross (watu wa Msalaba Mwekundu) wanatakiwa kuwa hapo. Yaani 'crowd management' (udhibiti wa mikusanyiko) kunapokuwapo na mkusanyiko wa zaidi ya watu 100 kuna hitaji 'sensitivity' ya hali ya juu (uangalizi) ya Jeshi la Polisi, Jeshi la Uokoaji na Red Cross," alisema Lema.

Zaidi Lema alieleza: "Mwamposa anaweza asikwepe makosa, lakini mtu wa kwanza kuwajibika ni Jeshi la Polisi na kwa vile Jeshi la Polisi liko chini ya Simbachawene, nilikuwa nashauri Simbachawene sasa aage tena arudi mtaani, halafu afikiriwe tena."

Alisema ajali hiyo ni funzo hasa mahali penye mikusanyiko ya dini, iwe ya kisiasa ama iwe ya kimichezo, kwamba Polisi wanahitaji sana kuwa na maarifa ya kudhibiti mikusanyiko.

Alisema kwa sasa huwezi kuanza kujadili suala hilo la imani, kwamba ni kwa nini watu wanakanyaga mafuta.

"Ukianza kujadili hivyo mambo ya imani utapata tabu, kuna wakati Yesu alidaiwa kodi akawaambia kina Petro nendeni huko ziwani kavueni samaki wa kwanza atakayemkuta teni dinari sasa issue za 'faith' (imani) ni 'trick' (mbinu) kidogo," alieleza Lema.

# Magufuli atuma salamu rambirambi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, ametuma salamu za rambirambi kwa familia za watu 20 waliopoteza maisha wakati wakitoka katika ibada Moshi mkoani Kilimanjaro, na kwa familia za watu zaidi ya 20 waliopoteza maisha kutokana na madhara ya mvua kubwa zinazonyesha mkoani Lindi na mikoa mingine nchini.

Watu 20 waliofariki dunia baada ya kukanyagwa na wenzao wakati wakitoka katika lango moja waliloelekezwa kupita ili kukanyaga mafuta ya upako katika viwanja vya Majengo, mjini Moshi na watu 16 walijeruhiwa.

Aidha, watu wengine zaidi ya 20 wamefariki dunia mkoani Lindi na katika mikoa mingine nchini ambayo imekumbwa na madhara yatokanayo na mvua nyingi zinazoendelea kunyesha.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, Rais alieleza kusikitishwa na idadi kubwa ya vifo vya Watanzania waliopoteza maisha katika matukio hayo, na amewaombea wapumzike mahali pema peponi na majeruhi wote wapone haraka na kurejea katika majukumu yao.

Aidha, alimtaka Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi na wakuu wa mikoa wengine

INAENDELEA UK. 8


LAND O'LAKES VENTURE37 — AgResults INNOVATION IN RESEARCH AND DELIVERY

**Wito wa maombi ya kushiriki katika shindano la mradi wa AgResults (AgResults Tanzania Dairy Productivity Challenge Project)**

Kwa niaba ya **Mradi wa AgResults , Land O' Lakes Venture37** inapenda kukaribisha mashirika na taasisi zinazojihusisha na uuzaji na usambazaji wa pembejeo kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa, kushiriki katika shindano la tuzo ambapo mradi umedhamiria kutumia mfumo wa kutoa motisha kutokana na kuuza pembejeo na kutoa huduma za ugani ili kuongeza wigo wa kutumia teknolojia bunifu, vifaa na mitizamo kwa ajilli ya kuongeza uzalishaji wa maziwa kwa kutumia pembejeo zilizo bora. Shindano hili litafanyika katika eneo la **Pwani ya Tanzania**, hasa Mikoa ya **Dar Es Salaam, Pwani, Tanga na Morogoro** (bila kushirikisha Wilaya za **Kilombero na Ulanga**)

**Land O' Lakes Venture37** inatoa wito kwa wote wanaotamani kushiriki kutoka kwenye sekta binafsi, taasisi au mashirika ya umma, na taasisi zisizo za kiserikali kushiriki katika mradi.

Wito wa Maombi ya Ushiriki (Request for Proposal – RFA) unaeleza historia, malengo, sheria ya kushiriki shindano hili ikijumuisha fomu ya maombi na taratibu za namna kuomba na mawasilisho. Katika kuwasilisha maombi, kampuni / shirika / Taasisi itakubaliana na masharti ya wito wa maombi ya ushiriki, ikiwa ni pamoja na taratibu za maombi na maelekezo yaliyowekwa.

Tafadhali kumbuka muda uliopangwa kwa ajili ya kupokea/kuwasilisha maombi ni **saa 11:00 Jioni ya Tarehe 28 Februari 2020.** Nyaraka za maombi lazima ziwasilishwe au zitumwe kwa anwani maalumu ya barua pepe ambayo ni **AgResultsTanzania@gmail.com**, kwa kuwasilisha Ofisi za AgResults zilizopo Veterinary Complex;131 Nelson Mandela Road, Dar es Salaam. Tafadhali andika "**Competitor RFA-AgResults Tanzania Dairy Productivity Project**" katika mstari wa somo la barua pepe au kwenye bahasha itakayobeba maombi hayo.

Mradi utapitia maombi yote na kutathimini kulingana na vigezo vilivyowekwa. Wale wote watakaofanikiwa kuchaguliwa watajulishwa na kuelezwa namna ya ushiriki.

**Ndugu mdau,** unahimizwa kuwasilisha maombi kwa wakati ili ujipatie tuzo/motisha na kuchangia maendeleo katika sekta ya maziwa Tanzania. Kama una maswali au maoni tafadhali tuma kwenye barua pepe ifuatayo; **NMrema@landolakes.org.**Tunatanguliza shukrani zetu kwa kwa kutuma maombi ya wito huu kwa wakati na pia tunategemea ushiriki wako katika mradi huu muhimu.

**Pata nakala ya wito wa maombi kupitia:**

https://agresults.org/news-and-blog/10-blog/152-rfa-tanzania-dairy-competitors

215578602

## Mbunge awachongea watumishi kwa waziri

**Na Romana Mallya,** MOROGORO

MBUNGE wa Ulanga, (CCM), Goodluck Mlinga, ameahidi kumkabidhi Waziri wa Madini, Doto Biteko, majina ya wanaokwamisha miradi katika sekta hiyo.

Aidha, miongoni mwa watu hao wamo watumishi wa Halmashauri ya Mahenge wilayani Ulanga mkoani Morogoro.

Mlinga alitoa ahadi hiyo juzi jimboni kwake wakati Waziri Biteko akikabidhiwa majengo matatu yatakayotumika kama ofisi za serikali ya Kijiji ya Wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro zilizojengwa na kampuni ya uchimbaji madini Mahenge Resources kama sehemu ya kuchangia shughuli za maendeleo.

Ofisi hizo zimejengwa kwa gharama ya Sh. milioni 51 na zitatumiwa na vijiji vitatu ambavyo ni Nahenge, Mdindo na Kisewe wilayani humo.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Mbunge Mlinga alisema kuna shida ya baadhi ya watu wanataka kukwamisha miradi hiyo.

"Cha kusikitisha zaidi wengine ni watumishi wa serikali, kuna changamoto ya mitegesho, leo hii unaweza kufanya uthamini wa mradi unasema mradi huu uthamini wake ni Sh. bilioni 10, unaanza mchakato inapofika siku ya uthamini wa mali unakuta siyo tena Sh. bilioni 10 ni Sh. bilioni 20, je, ni mwekezaji gani atakayewekeza mradi wa namna hii," alisema. "Ipo shida kubwa wengine ni watumishi wa halmashauri, ninao majina yao nitakukabidhi waziri," aliahidi. Kwa mujibu wa Mlinga, jimboni kwake ipo miradi mikubwa mitatu ya madini, lakini mmoja wapo aliwahi kumpeleka waziri na watu hawajafanyiwa tathmini.

"Nimechukua kumbukumbu za ambao hawajatathminiwa baada ya kukaa nao, niliwataka wachague wawakilishi ili kwenda ofisi moja baada ya nyingine kufuatilia changamoto hii, lakini ipo shida ya baadhi ya watu wanataka kukwamisha miradi," Mlinga alisema.

Alisema maeneo ya Ulanga kwa kiwango kikubwa yana madini lakini watu hawanufaiki nayo.

Alisema Januari 24, kulisainiwa mikataba ya makubaliano ya madini baina ya serikali na Kampuni ya Madini ya Barrick ambayo sasa italeta manufaa kwa taifa.

"Siku iliposainiwa ilikuwa anguko la makabulu weupe na weusi, ninapoongelea makabulu weusi ni wale wanaokwamisha miradi ya serikali ambayo sasa inaiwezesha serikali kupata asilimia 16," alisema.

Aidha, aliwaeleza wakwamishaji hao kuwa, wakiukwamisha mradi wa Mahenge Resources ni kuikosesha serikali asilimia hiyo 16 na manufaa mengine.

Naye Waziri Biteko aliwaeleza wananchi wa jimbo hilo kuwa, "Mageuzi makubwa katika sekta ya madini kwenye Wilaya yenu Mbunge wenu Mlinga ana mkono wake, nilikuja hapa nikiwa Naibu Waziri baada ya Mlinga akiwa bungeni alieleza matatizo mengi yaliyopo hapa na nilikuta yote ni kweli," alisema.

# Duni ataka Zitto alindwe

**Na Enock Charles**

NAIBU Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji, amewataka wanachama wa chama hicho kumlinda kiongozi wao Mkuu wa chama Zitto Kabwe, kufuatia kile walichodai kutishiwa maisha kufuatia waraka wake kwa Benki ya Dunia.

Barua hiyo ililenga kuitaka benki hiyo isitishe kuidhinisha mkopo wa dola milioni 500 kwa Serikali ya Tanzania. Kwa ajili ya kuendeleza elimu nchini

Akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, alisema hoja za Zitto zinapaswa kujibiwa kwa hoja bora zaidi badala ya kutumia vitisho huku akiitaka serikali kukutana na WB kutoa majibu ya kuridhisha, ili kuupata mkopo huo unaohitajika katika sekta ya elimu nchini.

"Chama cha ACT-Wazalendo kimevichukulia kwa uzito mkubwa vitisho vya wabunge wa CCM dhidi ya kiongozi wetu ndugu Kabwe, tunawaeleza lolote lile baya likimkuta, watawajibika kikamilifu, chama chetu kimewaweka katika hali ya tahadhari wanachama wetu nchi nzima kumlinda kiongozi wao kwa lolote," alisema Haji.

Zitto ambaye ni Mbunge wa Kigoma Mjini, anadaiwa kuandika barua kwenda WB kuiomba isitoe mkopo kwa Serikali ya Tanzania kwa madai ya kutotekelezwa kwa baadhi ya masuala

katika elimu na jamii kama vile watoto wa kike waliopata ujauzito wakiwa shule kutotakiwa kuendelea na masomo katika mfumo rasmi wa elimu nchini.

Mjadala huo uliibuka bungeni baada ya Mbunge wa Siha, Dk. Godwin Mollel, kuhoji uhalali wa mbunge huyo kuandika barua hiyo na kukiita kitendo hicho kuwa ni usaliti kwa nchi.

Kutokana na shutuma hizo, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alimuagiza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Adelardus Kilangi, kuchunguza kama hakuna jinai dhidi ya Zitto.

# Wateule wa JPM kuapishwa leo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Pombe Magufuli leo atawaapisha viongozi wa wizara, mahakama, majeshi na mikoa aliowateua juzi kushika nyadhifa mbalimbali.

Taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu ilieleza jana kuwa viongozi watakaoapishwa ni Makatibu Wakuu 5, Naibu Katibu Mkuu 1, Makatibu Tawala wa Mikoa 3, Kamishna Jenerali wa Magereza na Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji. Wengine ni Kamishna wa Ardhi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Msajili wa Mahakama ya Rufani, Msajili wa Mahakama Kuu na Wajumbe 3 wa Tume ya Utumishi wa Mahakama.




Waziri wa Madini, Doto Biteko (wa pili kushoto) pamoja na Mkuu wa Wilaya wa Ulanga, Ngolo Malenya (wa pili kulia) wakizindua moja ya majengo matatu ya ofisi ya serikali ya kijiji, iliyojengwa Ulanga mkoani Morogoro na kampuni ya uchimbaji Madini ya Mahenge Resources. Kulia kwa Waziri ni Mwenyekiti wa Mahenge, John De Vries ambaye ni Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Black Rock Mining kutoka Australia na wa kwanza kulia ni Mbunge wa Ulanga, Goodluck Mlinga. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# Mzee mbaroni kwa tuhuma za kujeruhi mtoto akitaka kumbaka

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma linamshikilia mkazi wa Masange wilayani Kondoa, Ally Busi (60) kwa tuhuma za kumbaka mwanafunzi wa darasa la saba (jina limehifadhiwa).

Akizungumzia na Nipashe jana, Kamanda wa Polisi mkoani humo, Gilles Muroto, alisema tukio hilo lilitokea Januari 29, mwaka huu wilayani humo.

Alisema katika purukushani za kutaka kumbaka binti huyo, mtuhumiwa alimjeruhi na kitu chenye ncha kali shingoni mtoto huyo na kukimbia, lakini polisi walimsaka na kufanikiwa kumkamata eneo la milimani wilayani humo.

"Mtuhumiwa alikamatwa na kufikishwa kituo cha polisi Kondoa, mtuhumiwa amefanya kitendo cha kikatili kwa mtoto mdogo kama huyo na kumjeruhi vibaya katika eneo la shingo na pia alimpiga na kitu kizito maeneo ya kichwani," alisema Kamanda Muroto.

Kamanda Muroto alisema ripoti ya daktari inaonyesha binti huyo anaendelea vizuri na amepata majeraha sehemu ya koromeo, kichwani na shavuni.

"Majeraha aliyopata yalimsababishia kuvuja damu nyingi, lakini juhudi za madaktari wanaendelea na jitihada za kumpatia tiba ili afya yake iimarike na kurejea katika hali yake ya kawaida," alisema Muroto.

Hata hivyo, alisema mtuhumiwa huyo kwa sasa anaendelea kushikiliwa na polisi, huku upelelezi ukiendelea na atafikishwa mahakamani.

Muroto aliwataka wazee wa umri huo kuachana na tabia za tamaa za kimwili kwa watoto wadogo.




Ofisa Utumishi wa Mahakama Kuu-Masijala Kuu, Jumanne Msuta, akiwapa maelezo wanafunzi kuhusu masuala ya sheria, walipotembelea banda la ofisi hiyo, katika kambi ya kutoa msaada wa kisheria kwa wananchi katika viwanja vya Mnazi Mmoja, ikiwa ni kuadhimisha Wiki ya Sheria Kanda ya Dar es Salaam, juzi. **PICHA NA JUMANNE JUMA**

# TRA, ZRA kudhibiti pamoja magendo, kuondoa foleni

**Na Mwandishi Wetu,** SONGWE

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) na Mamlaka ya Mapato Zambia (ZRA) zimesaini makubaliano ya kubadilishana taarifa kwa njia ya mtandao lengo kuu ikiwa ni kuondoa kero ya foleni ya malori, kudhibiti biashara ya magendo ili kukusanya mapato stahiki na kukuza uchumi wa nchi hizo.

Makubaliano hayo yamesainiwa kati ya Kamishna Mkuu wa TRA, Dk. Edwin Mhede na Kamishna Mkuu wa ZRA, Kingsley Chanda.

Kusainiwa kwa mkataba huo ni utekelezaji wa maelekezo aliyoyatoa Rais John Magufuli Oktoba 5, mwaka jana, wakati akiwa na Rais wa Zambia, Edgar Lungu, walipofungua kituo cha huduma za pamoja mpakani Tunduma. Akizungumza wakati wa utiaji saini makubaliano hayo, Dk. Mhede alisema kuwa Desemba 13, mwaka jana walikutana na Kamishna Mkuu wa ZRA na kukubaliana kuwa kuna umuhimu wa kuboresha huduma, kutatua changamoto za kiforodha na kuimarisha uhusiano wa kibiashara katika nchi hizo mbili ili kuongeza ufanisi.

Alisema walichokubaliana ni pamoja na kurahisisha kuweka mfumo wa kubadilishana taarifa kwa njia ya mtandao, njia ambayo itawezesha nchi zote mbili kupata taarifa sahihi za mzigo inayosafirishwa na kuziwezesha kukusanya kodi kwa urahisi na ufanisi.

Alisema maboresho mengine ni kutatua changamoto ya mizigo kukaa muda mrefu mpakani na kukwamisha shughuli za biashara kurahisisha taratibu za kiforodha kwa kubadilishana taarifa ya mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam hadi inapovuka mpaka wa Nakonde kwa upande wa Zambia.

"Ninayo furaha kubwa kuwaambia kuwa tayari tumeshakamilisha makubaliano ambayo tuliahidiana kukamilisha, sasa tuna mahusiano rasmi katika hili eneo la mpaka wetu na kupitia utaratibu huu tutapunguza changamoto ya magendo," alisema Dk.Mhede na kuongeza:

"Tumeziagiza idara zote zinazohusika na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) kwa upande wa Tanzania na Zambia kuhakikisha ndani ya muda usiozidi miezi miwili kuja na mfumo wenye uwezo wa kusoma taarifa za mizigo na magari yanayotoka bandarini moja kwa moja ili kuziona taarifa kwa muda mwafaka lengo likiwa ni kuongeza ufanisi na kutatua changamoto ya upotevu wa mapato," alisema Dk. Mhede.

Kwa upande wake Kamishna Chanda alisema malengo waliopanga yametimia na kusema kuwa ushirikiano mkubwa ndio umesababisha kufanikiwa katika kuboresha mpaka huo ambao ni lango kubwa la nchi za kusini mwa Afrika ambazo ni wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Alisema Zambia itaendelea kuboresha na kutatua changamoto ambazo zilikuwa zikikwamisha magari kuchelewa kuvuka kwa kuboresha miundombinu ya barabara na kujenga sehemu kwa ajili ya kuegesha magari yatakayoondoa msongamano.

# Mpina awapa vigogo watatu siku saba

**Na Mwandishi Wetu,** KATAVI

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ametoa siku saba kwa Daktari Mkuu wa Mifugo Tanzania (CVO), Kamishna wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na Wakili Mkuu wa Serikali wakutane kutathmini na kuondoa dhuluma zinazoendelea kwa wafugaji pamoja na kuandaa kanuni na miongozo itakayoweka uwazi katika usimamizi wa sheria za misitu na mifugo.

Mpina ametoa agizo hilo mwishoni mwa wiki baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika Mkoa wa Katavi kutoza faini ya shilingi milioni 60 sawa na shilingi laki moja kwa kila ng'ombe baada ya ng'ombe 600 kukamatwa wakichungwa ndani ya Msitu wa Tongwe Mashariki unaomilikiwa na halmashauri hiyo.

Waziri Mpina amefikia hatua hiyo baada ya kuwapo ukiukwaji mkubwa wa sheria na ukamataji holela wa mifugo unaofanywa kwenye baadhi ya halmashauri, hifadhi za wanyama, mapori ya akiba ambapo mifugo inapokamatwa hunyimwa huduma muhimu ikiwamo malisho, maji, chanjo na dawa hali inayosababisha mifugo mingi kudhoofika na kufa.

Alibainisha manyanyaso mengine ni wafugaji kutozwa faini kubwa ambazo hazipo kwa mujibu wa sheria, kupigwa, mifugo kuibiwa, kupigwa risasi na mingine kuuzwa kwa njia ya mnada kwa kisingizio cha kukosekana mmiliki wa mifugo hiyo, huku idadi inayotajwa mahakamani ni ndogo ikilinganishwa na mifugo iliyokamatwa.

Akizungumza baada ya kufika eneo ilikoshikiliwa mifugo hiyo umbali wa zaidi ya kilomita 50 kutoka barabara ya Mpanda-Kigoma, Waziri Mpina alihoji iweje halmashauri hiyo iache kufuata sheria za nchi zinavyoelekeza kwa watu wanaoingiza mifugo na badala yake wakabuni faini ya kutoka kichwani kinyume cha sheria na kuitafsiri hatua hiyo kuwa ni uonevu, rushwa, wizi, dhuluma na manyanyaso kwa wafugaji.

Waziri Mpina alisema yeye kama msimamizi mkuu wa sekta ya mifugo nchini hawezi kumtetea mfugaji anayevunja sheria kwa kuingiza mifugo kwenye maeneo yaliyokatazwa kisheria lakini kilichomfanya kuingilia kati suala hilo ni kuvunjwa kwa Sheria ya Misitu Namba 14 ya mwaka 2002 inayoeleza bayana kwamba mtu atakayekutwa ametenda kosa ndani ya msitu atatozwa faini ya Sh. 30,000 na isiyozidi milioni moja.

"Kutoza hela ambayo haiko kwenye sheria ni wizi, ni manyanyaso kwa wafugaji, rushwa

INAENDELEA UK. 8

# Wafanyabiashara walia corona kushusha bei bidhaa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KUIBUKA kwa virusi vya corona nchini China kumesababisha kushuka kwa mazao yatokanayo na ng'ombe mkoani Shinyanga kutoka Sh. 20,000 hadi 15,000 kwa kilo moja ya pembe za ng'ombe.

Hayo yalibainishwa jana na mmoja wa wafanyabiashara wa bidhaa hiyo mjini hapa, Emmanuel Kitonka, wakati akizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa kila siku biashara hiyo inaendelea kushuka kutokana na uwapo wa virusi hivyo.

Alisema kuwa kabla ya kuibuka kwa virusi vya ugonjwa wa corona nchini China, bei ya mazao yatokanayo na ng'ombe yalikuwa yanauzwa kwa bei kubwa ukilinganisha na hivi sasa kilo moja ya pembe inauzwa Sh. 15,000 kutoka Sh. 20,000 ya hapo awali.

Alisema awali walikuwa wakiuza kilo moja ya uume wa ng'ombe Sh. 25,000, lakini sasa bei imeshuka hadi kufikia Sh. 17,000 kwa kilo moja.

"Uume wa ng'ombe hutumika kutengenezea nyuzi za kushonea wagonjwa wenye majeraha au mwanamke aliyefanyiwa operesheni," alisema Kintoka na kuongeza:

"Virusi hivi vilivyoibuka vimefanya biashara zetu kushuka na kupata hasara jambo hili linaweza likasababisha tukashindwa kuendelea kufanya biashara hii na kama hali hii itaendelea hivi tutashindwa kufanyabiashara kutokana na wanunuzi wengi tunategemea kutoka China," alisema Kitonka.

Kitonka aliomba serikali kuwasaidia kuirasimisha biashara ya mazao yatokanayo na ng'ombe kama ilivyo biashara ya korosho, tumbaku na pamba na kuwatafutia masoko ili kuacha kuendelea kutegemea soko moja kutoka China.

Kwa upande wake, Ofisa Mifugo wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Dk. Damiani Kilyenyi, alikiri kuwapo kwa biashara ya usafirishaji uume wa ng'ombe na pembe kwenda China.

Hata hivyo, alisema sheria ya udhibiti wa magonjwa ya mifugo ya namba 17 ya mwaka 2003 hairuhusu viungo vya uzazi vya mifugo kubebwa kwa ajili ya matumizi mengine.

Dk. Kilyenyi aliwataka wafanyabiashara hao kuacha tabia ya usafirishaji wa viungo vya uzazi vya wanyama aina ya ng'ombe.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hili la ratiba Ligi Kuu, TPLB imulikwe upya

**LIGI** Kuu Tanzania Bara imeendelea jana kwa Yanga kukamilisha mzunguko wake wa 16 kwa kucheza dhidi ya Mtibwa Sugar ambayo kwao hiyo ilikuwa ni mechi yao ya 18 msimu huu.

Hata hivyo, licha ya Yanga kuwa nyuma kimchezo ukilinganisha na timu nyingine 19 zinazoshiriki ligi hiyo, katikati ya wiki, Jumatano haikuwa na ratiba yoyote ya mchezo wakati timu nyingine zikishuka dimbani.

Mtibwa Sugar ambayo jana ilivaana na Yanga, Uwanja wa Taifa, Alhamisi iliyopita ilivaana na Azam FC wakati Yanga ikipumzika hadi jana iliposhuka Uwanja wa Taifa kuwakaribisha 'Wakulima wa Miwa' hao wa Turiani, Morogoro.

Kadhalika, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu, Simba Jumatano wenyewe waliikaribisha Namungo FC, huo ukiwa ni mchezo wao wa 17 kabla ya juzi, Jumamosi kurejea tena Uwanja wa Taifa kuikaribisha Coastal Union katika Uwanja wa Taifa.

Kwa michezo hiyo michache tu, inaonyesha ni kwa namna gani Bodi ya Ligi Kuu nchini (TPLB) imeshindwa kutambua ni timu gani ilipaswa kuwa na ratiba ya kucheza katikati ya wiki na mwishoni mwa juma kulingana na kuwa nyuma ya ratiba.

Nipashe tulitarajia kuona Yanga ikicheza Jumatano na Jumamosi ili kumaliza viporo vyake, huku timu kama Simba, Ruvu Shooting, Lipuli, Biashara United zikipumzika na kucheza jana, lakini mambo yakawa kinyume chake.

Kutokana na mkanganyiko huo, tayari Mtibwa Sugar ilishafungua mdomo kwa kueleza kutofurahishwa na upangaji huo wa ratiba, ambao uliowapa wapinzani wao muda mrefu zaidi wakupumzika na kujipanga kwa mchezo huo wa jana, achilia mbali na matokeo ya mechi hiyo.

Lakini ratiba hiyo inaonyesha Yanga mbeleni itakabiliwa na ratiba ngumu ya kucheza mechi tisa mfululizo, jambo ambalo tunatarajia kuiona klabu hiyo ikilalamika.

Hii si mara ya kwanza kwa TPLB kulalamikiwa kuhusu kuvurunda katika upangaji wa ratiba hiyo, kwani ubovu huo pia ulijitokeza sana msimu uliopita hali iliyochangia baadhi ya mashabiki na hata viongozi wa klabu kudai ipo timu iliyoandaliwa kuwa bingwa.

Tukiwa kama wadau namba moja wa soka nchini, tunaona umefika wakati sasa kwa TPLB kukiri kushindwa kupanga ratiba ambayo itakuwa rafiki kwa klabu zote ili mwishoni mwa msimu pasiwe na malalamiko baadhi ya klabu kudai bingwa alikuwa ameshaandaliwa.

Aidha, ni wakati sasa kwa Shirikisho la Soka nchini (TFF) kuimulika upya bodi hiyo ya ligi ili kuweza kupata ufumbuzi wa tatizo hili ambalo limekuwa kero kuanzia kwa klabu, wadau wa soka hadi mashabiki.

Tunataka kuona kuelekea mzunguko wa pili, mtiririko wa mechi ukienda sawa kwa TFF kuisuka upya TPLB itakayoweza kuandaa ratiba isiyoegemea ama kulalamikiwa na upande wowote ule.

Tunaamini kwa kuwa ndiyo kwanza Ligi Kuu inaelekea kuingia katika mzunguko wa pili ambao ndio mgumu zaidi na wenye lawama nyingi kutokana na baadhi ya timu kutafuta pakufia, TFF itaimulika kwa makini TPLB ili kurekebisha mambo na kuondoa lawama zisizo za msingi kwa kupatikana ratiba itakayokuwa rafiki kwa klabu zote.

Lengo letu ni kuona bingwa msimu huu anapatikana bila kuwapo kwa malalamiko yanayohusishwa na upangaji mbovu wa ratiba, na hilo linawezekana tu kama TFF itaimulika upya TPLB na kwa umakini mkubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Timu mbili michuano ya Caf, Tanzania ni kujitakia

**KWA** sasa Wabongo wako 'bize' kushangilia bao la Mbwana Samatta kwenye Ligi Kuu ya England, na kuwasahaulisha kuwa msimu ujao Tanzania itapeleka timu mbili tu kwenye michuano ya kimataifa, moja Ligi ya Mabingwa Afrika na nyingine Kombe la Shirikisho.

Hili ni jambo la kuhuzunisha sana lililotokea wiki iliyopita, lakini limefunikwa na bao la Mbwana.

Ukweli ni kwamba Tanzania ilipiga hatua moja mbele msimu uliopita baada ya klabu ya Simba kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kiasi cha Shirikisho la Soka Afrika (Caf) kuiongezea timu za kushiriki michuano hiyo na kwa mara ya kwanza iliwakilishwa na timu nne, mbili zikicheza Ligi ya Mabingwa na mbili Kombe la Shirikisho.

Simba na Yanga zilikwenda kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku Azam FC na KMC zikicheza Kombe la Shirikisho. Kilichotokea hapo ni historia.

Kati ya timu zote nne, hakuna timu yoyote iliyofanikiwa kuingia hata hatua ya makundi, huku timu iliyokuwa ikitegemewa ambayo ndiyo iliyosababisha kuongezewa timu, Simba ikiondolewa kwenye hatua za awali tu na timu ya UD Songo ya Msumbiji, timu ambayo ilifungwa mechi zote nne baada ya kuwatoa Wekundu wa Msimbazi hao.

Ushindi wa Al Nasr ya Libya dhidi ya Djoliba ya Mali wa bao 1-0 majuzi kwenye mechi ya Shirikisho barani Afrika, umeiweka Tanzania kupumulia mashine kupeleka timu nne mwakani kimataifa.

Kwa sasa Al Nasr inahitaji sare tu na Horoya iweze kufuzu hatua ya robo fainali kwa sababu ina pointi nane nyuma ya Horoya ya Guinea yenye pointi 10.

Djoliba ina pointi tano na Bidvest ya Afrika Kusini ina pointi mbili tu, hivyo Watanzania wanachoombea ni kwamba Horoya iifunge Al Nasr na Djoliba iliifunge Bidvest ili timu hiyo ya Libya isiweze kutinga hatua ya robo fainali jana ambalo ni gumu.

Endapo Al Nasr itafuzu moja kwa moja Tanzania itabidi ipeleke wawakilishi wawili tu kwenye michuano hiyo, mmoja Ligi ya Mabingwa na mwingine Kombe la Shirikisho.

Ni kwa sababu Libya itafikisha pointi 16.5 na kuicha Tanzania ikiwa na pointi 14 tu.

Hili halikupaswa kutokea kabisa kwani ilitegemewa timu nne, japo mbili tu au moja ingeweza kuitoa kimasomaso Tanzania kama ilivyofanya Simba.

Kwa sasa Watanzania wanaoona hatari hii wanaomba Mungu, ingawa ni ngumu, kwani hata Djoliba yenye pointi tano ikishinda itafikisha pointi nane kama Al Nasr, lakini hata timu hiyo ikifungwa na Horoya, bado tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa ndiyo itaamua.

Kama Tanzania ikibaki na timu mbili tu, badala ya nne kama ilivyokuwa msimu uliooisha kwa mara ya kwanza, basi itabidi kujilaumu wenyewe kwa timu zote hizo kutolewa mapema msimu huu.

Ilionekana kama vile timu hazikujiandaa vema na michuano hiyo, labda baadhi zilishtukizwa, lakini zingine kama Simba zilionekana zimeanza kuchukulia poa michuano hiyo kwa sababu tu msimu uliopita ilifika robo fainali na kuona kama inaweza kufanya hivyo tena kwa urahisi.

Litakuwa ni funzo kwa timu yoyote itakayotwaa ubingwa wa Tanzania Bara, na Kombe la FA kufanya usajili bora na wenye tija, lakini pia maandalizi mema kwa ajili ya kuhakikisha angalau timu za Tanzania zinatinga hatua ya makundi na si misimu yote kuishia raundi ya mwanzo, huku kuingia makundi ikionekana kama bahati nasibu.

## MJADALA

# Chaki ubaoni bado ni bora

**Mhariri,**

*KUTOKANA na hatua za maendeleo kufikiwa na kuwapo mageuzi makubwa katika teknolojia, elimu ni moja ya sekta zilizofikiwa mapema na hatua hiyo ya utandawazi.*

*Hayo mageuzi yanagusa mfumo wa ufundishaji, ulioingiliwa sana walimu wakihama kutoka katika matumizi ya chaki ubaoni na wakahamia katika kompyuta, mahsusi wakitumia kifaa aina ya 'power point.'*

*Katika maana ya karibu, ni namna fulani ya wafundishaji wanajipumzisha na chaki ubaoni. Lakini niseme, huku chini katika ngazi ya shule siwezi kuizungumzia sana, maana chaki bado imetawala mfumo wote wa maisha ya masomoni.*

*Binafsi nikirejea katika mtazamo wa jumla wa matumizi ya chaki yana tija zaidi kuliko 'power point' ambayo kwa kiasi kikubwa ndio mwenendo mpya katika ngazi ya chuo, imebeba sura ya fasheni kwa watumiaji kuliko tija ya ufundishaji, ikilinganishwa na chaki ubaoni.*

*Ninaweza kutetea matumizi ya kompyuta inakuwa na tija iwapo tu ni darasa lenye wanafunzi wengi, mathalani inayozidi mathalani wanafunzi 100.*

*Kama ndio hivyo, iwe ama wahadhiri au wakufunzi vyuoni, ambao bado wanaaangukioa kundi la walimu, naamini katika nafasi kubwa chaki ubaoni ina nafasi kubwa ya tija.*

*Mbinu na mtiririko wa uandikaji, unaendana na maandalizi ya mfundishaji, lakini mbinu za uwasilisho na kinachoandikwa kinaendana na anavyopokea hisia darasani na kuzifanyia kazi kwa kina.*

*Nirejee imani yangu tu kwamba, chaki ni zaidi kuliko 'power point' kwa tija darasani, kama hapatakuwapo utata wa kimazingira darasani kama vile wingi wa wanafunzi.*

**Oscar Dickson,**
**Mbeya.**




# Hivi yaliyotokea Sokoine, Mkwakwani hawajajifunza?

**Na Adam Fungamwango**

KWA sasa uongozi wa Uwanja wa Sokoine, CCM na serikali ya mkoa wa Mbeya wako kwenye hekaheka ya kuutengeneza tena baada ya kuharibiwa na mashabiki wa muziki waliokuwa kwenye tamasha mwishoni mwa Desemba mwaka jana.

Picha zilizopigwa kesho yake zilionyesha uwanja huo ukiwa umegeuka kama shamba la mpunga, na ukiangalia kwa haraka haraka unaweza kudhani labda kuna watu walikuwa wameanika dagaa.

Wadau wa soka walilaumu kitendo cha uongozi kuruhusu tamasha la muziki kufanyika katikati ya uwanja wa kuchezea mpira, badala ya kutafutwa sehemu maalum kwa ajili ya tamasha hilo.

Viongozi walitupiana mpira, lakini kilichotokea ni kwamba Bodi ya Ligi iliusimamisha uwanja huo na sasa timu zilizokuwa zikitumia Uwanja wa Sokoine, Mbeya City na Prisons, zinautumia Uwanja wa Samora mjini Iringa kwa ajili ya mechi za Ligi Kuu.

Wakati mashabiki wa soka mjini Mbeya wakihaha kutoona mechi za ligi, huku wakazi wa huko wakikosa fursa za kufanya biashara, juzi tena kumetokea kitu kama hicho mjini Tanga kwenye Uwanja wa Mkwakwani.

Nako pia picha za mitandao na televisheni zimeonyesha kuwa kulikuwa na tamasha la muziki, kama kawaida mashabiki wakiwa katikati ya uwanja wakiserebuka.

Mkwakwani ni moja kati ya viwanja ambavyo kabla hata tamasha la muziki hakikuwa vizuri.

Kiwanja hicho ni moja kati ya viwanja ambavyo viliwahi kufungiwa kwa muda na kikafanyiwa marekebisho ambayo angalau kinaonekana kukidhi haja, ingawa si kwa kiasi kikubwa kama inavyotakiwa.

Kitendo cha kuruhusu tena mashabiki kuingia uwanjani kuserebuka kwenye tamasha la muziki kunaweza kabisa kusababisha sehemu ya kuchezea ikawa kama ile ya Uwanja wa Sokoine.

Mpaka sasa sijaona picha baada ya tamasha hilo kumalizika, lakini vyovyote itakavyokuwa hautokuwa kwenye hali yake ya mwanzo, na hata kama ukiwa bado vizuri, hivi ni kwa nini watu waendelee kuruhusu viwanja vya soka kufanyika matamasha ya muziki?

Hivi uongozi wa Uwanja na serikali ya mkoa wa Tanga hawajajifunza kilichotokea mkoani Mbeya kiasi kwamba athari na hasara imekuwa kubwa kuliko ilivyodhaniwa?

Cha kujiuliza ni kwamba hivi hakuna kumbi au viwanja vya wazi ambavyo vinaweza kutumika kwenye matamasha ya muziki zaidi ya viwanja vya soka?

Hata kama inasemekana kuwa waandaaji huwa wanalipa pesa, lakini hivi kweli pesa inayopatikana inaweza kuwa nyingi kiasi kwamba inazidi hata gharama ya matengenezo pale unapoharibika?

Kingine unajiuliza, hivi watu hawajui maana ya kumbi za starehe, burudani, viwanja vya wazi na viwanja ambavyo vimetengenezwa maalum kwa kuchezea soka tu?

Ifike wakati Watanzania waanze kutofautisha kati ya 'stadium' na 'hall' ambavyo ni vitu tofauti na hata wazungu walianzisha vitu hivyo wamevitofautisha.

Huwezi kukuta mwanamuziki nchini Marekani, au England akienda kutumbuiza kwenye Uwanja wa Anfield au Etihad kwa sababu vile vimetengenezwa maalum kwa ajili ya kuchezea soka na badala yake watatumbuiza kwenye kumbi.

Uzuri ni kwamba karibuni mikoa yote ya Tanzania kuna kumbi nyingi na nzuri na hata viwanja vya wazi kwa nini visitumike, badala yake muziki unakwenda kupingwa kwenye uwanja wa mpira halafu mara nyingi baada ya hapo vinakuwa vimeharibika?

Na si hilo tu, katika muziki kuna viburudisho kama soda na bia, na si jambo la kushangaa kuona chupa zikiwa zimevunjia jambo ambalo linaweza kuwa hatari kwa usalama wa wachezaji wakati wa mchezo wa soka kama hakukufanyika usafi wa hali ya juu.

Kwa miaka ya hivi karibuni kumekuwa na upungufu wa sehemu za kuchezea mpira, huku kukiwa na ongezeko la kumbi za burudani, inakuwaje hata kwenye hivyo viwanja vichache nako wachezaji wanabanwa?

Baada ya Mbwana Samatta kuanza kucheza Ligi Kuu ya England watu wengi na hata viongozi mbalimbali wamekuwa wakisisitiza wazazi kuruhusu watoto wao kucheza soka na wasiwakataze kama ilivyokuwa zamani, lakini moja ya vitu ambavyo vinapaswa kuangaliwa ili kupatikana kwa Samatta wengine ni kuwapo kwa viwanja, tena vilivyo bora.

Sasa kama wapo viongozi ambao wanashindwa kuvitunza hata viwanja vichache vilivyopo, lengo la kuzalisha kina Samatta wengine litatimia kweli?

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed




**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Mtume Mwamposa anaswa mafichoni, waziri anena

INATOKA UK. 3

kuwa vingi na kwa hivyo lazima kuviwekea utaratibu tu, kwa mfano wa Rwanda wameweka utaratibu wakasema kwa kweli mtu hawezi kuanzisha ministry au huduma mpaka awe angalau ana Shahada ya Theolojia."

Alisema huduma hizo kwa sasa zimekuwa nyingi na nyingine zinaanza na hata ukiwa wewe huna huo upako, lakini ukisikiliza, ukisikia, unasema Mungu wangu, hapa kweli Mungu yuko hapa?

Simbachawene alisisitiza: "Tutaanza kufikiria hivyo na kweli kuna huduma zinaonekana kabisa kwamba ni kinyume, lakini iko haja sasa tukatengeneza kanuni katika siku za usoni ambazo zitatufanya tuangalie na kusema hii sio sawa, kabla hatujapata madhara."

Simbachawene alisema Sheria ya Jumuiya, Sura Namba 337 na hasa kifungu cha 9 na cha 19, kinampa mamlaka yeye kama Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kuwa ndiye msajili jumuiya za kijamii na madhehebu ya dini na shughuli zote za taasisi za watu binafsi.

Aidha, Waziri Simbachawene alieleza, "Ni lazima kama serikali tuchukue hatua zinazostahili kwa sababu inasikitisha kuona una idadi kubwa ya watu umewakusanya mahali, mwenye jukumu la kuhakikisha usalama wao ni wewe uliyewakusanya hapo pamoja na kwamba kuna jukumu la serikali la kuhakikisha watu wanakuwa salama kwa idadi kubwa ya watu wa namna hiyo." Alisema kwa Mtume Mwamposa kutoa maelekezo au maneno ambayo yanaweza kusababisha mhemuko na watu kukimbizana na kufikia hatua ya kuumia, anaowajibu wa kuwajibishwa katika kosa hilo.

**MWAMPOSA ALIKIUKA MASHARTI YA KIBALI**

Kwa mujibu wa Waziri Simbachawene, Mtume Mwamposa alifanya kosa ambalo ni kukiuka masharti ya kibali alichopewa na Jeshi la Polisi, ambacho kilimtaka kufanya mikutano yake ya injili kuanzia saa 6:00 mchana hadi saa 12:00 jioni, lakini tukio hilo lilitokea kati ya saa 1:30 hadi saa 2:00 usiku wa Februari 1, 2020. Alifafanua kuwa kibali hicho cha kufanya mkutano wa injili, kinasema Mwamposa na wenzake walipaswa kukitumia kati ya Januari 30 hadi Februari 1, 2020 kati ya saa 6:00 hadi saa 12:00 jioni na si vinginevyo.

"Inaonyesha namna ambayo masharti ya kibali yalikuwa yamekiukwa, lakini kuwaelekeza watu zaidi ya 10,000 waliojazana mahali kwamba wapite sehemu moja, pia inaonyesha kutokuwajibika katika kuwa na dhamira ya kwamba unajua jukumu la kuhakikisha hawa watu wanakuwa wako salama," alifafanua Simbachawene.

**ANASWA MAFICHONI DAR**

Akitoa taarifa za kukamatwa kwa Mtume Mwamposa baada ya kutoroka Moshi usiku wa Aprili mosi mwaka huu, Waziri huyo, alisema Mtume Mwamposa alikamatwa na makachero wa Polisi katika viunga vya Jiji la Dar es Salaam jana alfajiri.

"Tulikuwa na taarifa angesafiri kwa ndege, lakini hakufanya hivyo, amekamatwa Dar es Salaam alfajiri ya leo (jana) na tulikuwa tumejitahidi kuweka barrier (kizuizi) katika maeneo mbalimbali, lakini kwa namna ambayo ameonyesha nia ya kukimbia tumemkamatia Dar es Salaam na hakusafiri kwa ndege alisafiri kwa gari.

"Kile kibali cha kufanyia shughuli ya mkutano wa injili kiliombwa na Mchungaji Elia Mwambamba na wote hao wako kwenye mikono ya Polisi."

**DC WARIOBA ANENA**

Jana alfajiri, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, alisema hadi kunakucha walikuwa wamesambaza maofisa kadhaa wa Polisi kuzunguka katika zahanati, vituo vya afya, Hospitali ya Rufani ya mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi na Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC kuchunguza idadi kamili ya majeruhi waliokimbizwa huko kupata matibabu.

**RPC HAMDUNI: 7 MBARONI**

Kabla ya taarifa ya Mwamposa kukamatwa jijini Dar es Salaam, Kamanda wa Polisi mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi, Salum Hamduni alitangaza jeshi hilo kuwashikilia watu saba hadi sasa akiwamo Mchungaji Elia Mwambamba wa Kanisa la Calvary Assemblies of God ambaye ndiye aliyeomba kibali cha kufanyika kwa kongamano hilo.




Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Iringa, SP. Yusuf Kamote (kulia), akimvisha kiakisi mwanga Mwenyekiti wa Umoja wa Bodaboda Iringa, Juma Gamba wakati wa uzinduzi wa kampeni ya 'Usitumie Kilevi na Kuendesha Chombo cha Moto' iliyoratibiwa na kampuni ya bia ya Serengeti Breweries Limited, hafla iliyofanyika katika viwanja vya Stendi ya Daladala Manispaa ya Iringa jana. Kushoto ni Meneja Uhusiano wa SBL, Neema Temba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpina awapa vigogo watatu siku saba

INATOKA UK. 5

huwezi kutoza hela ya serikali ambayo haiko kwenye kanuni yaani serikali iache kusimamia sheria ifanyie kazi maamuzi ya vikao," alisema.

Mmoja wa wachungaji hao, Koye Mmela, alilamikia kitendo cha kukamatwa na kushikiliwa msituni kwa siku sita mfululizo bila kufikishwa mahakamani jambo walilolitaja ni uonevu mkubwa waliofanyiwa na askari waliokuwa doria.

Mwanasheria wa Halmashauri ya Tanganyika, Maraka Mrisho, alimweza Waziri Mpina kuwa faini hiyo ya milioni 60 haipo kwenye sheria yoyote bali ilitozwa kufuatia makubaliano ya kikao kilichowahusisha maofisa wa misitu wa halmashauri pamoja na Maofisa wa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) wa kanda hiyo na kubariki faini ya shilingi laki moja kwa kila ng'ombe.

Mrisho alisema kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Namba 14 ya Mwaka 2002, kifungu cha 84 kifungu kidogo cha tano kinasema mtu yeyote atakayekutwa na kosa ndani ya misitu atatakiwa kulipa faini isiyopungua Sh. 30,000 na isiyozidi Sh. milioni 1 hivyo hakuna kifungu kinachozungumia kutoza faini ng'ombe.

Daktari Mkuu wa Mifugo Tanzania, Prof. Hezron Nonga, alisema waliokamata mifugo hiyo wamevunja Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Namba 17 ya mwaka 2003, Sheria ya Ustawi wa Wanyama Namba 19 ya mwaka 2008 kutokana na ng'ombe 600 kurundikana kwenye zizi dogo linalotosha ng'ombe 60 tu hali iliyosababisha mifugo kukosa hewa na kufa, ndama kukanyagwa, kujeruhiwa na kufa.

Prof. Nonga alisema ng'ombe hao wamefungiwa zizini muda mrefu bila maji wala malisho hali iliyopelekea afya zao kudhoofika, utaratibu wa ukamataji mifugo haukufuatwa kwa kuwa haukuhusisha daktari wa mifugo kama sheria inavyoelekeza huku mifugo hiyo ikinyimwa chanjo na tiba hivyo waliohusika na ukamataji huo walitakiwa kukamatwa na kushtakiwa kwa mujibu wa sheria hizo.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, Rojaz Romuli. alisema halmashauri hiyo haina bajeti ya kutibu mifugo pindi inapokamatwa msituni bali jukumu lao ni kulinda misitu isiharibiwe na wavamizi wakiwamo wafugaji na wawindaji haramu.

Hivyo baada ya mazungumzo ya kina ya kisheria na kubainika kulikuwa na ukiukwaji mkubwa wa sheria ndipo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Tanganyika, Rojazi Romuli akalazimika kubatilisha adhabu hiyo na kuwatoza faini ya shilingi milioni 11 badala ya shilingi milioni 60 ya hapo awali.

# Simanzi Moshi

INATOKA UK. 2

kutokana na kukosa hewa, kutokana na msongamano wa watu, mshtuko wa moyo na wengine walipata michubuko katika maeneo tofauti ya miili yao.

Dk. Adolph alisema majeruhi 16 wamelazwa katika wodi namba 7, 3 na watoto na hali zao ni za kuridhisha.

Baadhi ya majeruhi waliomba serikali kutazama utaratibu wa utoaji wa vibali katika mikusanyiko ya watu kwa kuhakikisha vibali vinavyotolewa vinazingatiwa. Majeruhi hao katika tukio hilo, Maureen Faustine mkazi wa Mererani, na Mary Paulo walisema iwapo mamlaka husika zingesimamia utaratibu jambo hilo lisingejitokeza.

Aidha, majeruhi hao walilalamikia kukosekana kwa utaratibu wa kukanyaga mafuta katika maombezi hayo hali iliyosababisha watu kukanyagana.

"Tulikosa utaratibu wakati wa kukanyaga mafuta, hapakuwa na polisi wala watumishi wa Mwamposa wakati wa kukanyaga mafuta hayo kila mtu alikanyaga kwa juhudi zake, lazima maafa yangetokea," alisema.

Majeruhi Paulo alilalamikia kukosekana kwa huduma ya dharura katika tukio hilo, lakini hapakuwa na mwongozo wa nini kifanyike ili kuepuka madhara. Walisema katika huduma hiyo ya maombezi hapakuwa na magari ya dharura ya kubeba wagonjwa hadi Jeshi la Polisi lilipokwenda kubeba majeruhi na miili ya watu waliopoteza maisha.

**MEYA ANENA**

Naibu Meya wa Manispaa ya Moshi, Anthony Benedict, alitaka wananchi kutafakari mienendo yao kama wapo sahihi ili kuepuka maafa.

Aliomba vyombo vya usalama kuzingatia muda wa kufanyika kwa matukio kama inavyokuwa katika mkutano wa vyama vya siasa kwamba baada ya saa 12:00 jioni ni marufuku mikutano kuendelea.

**MBUNGE ATUMA SALAMU**

Mbunge wa Moshi Mjini, Japhary Michael, katika ukurasa wake wa Facebook aliandika salamu za pole kwa waliopoteza wapendwa wao.

"Nichukue fursa hii kuwapa pole ndugu na jamaa wa waumini wote ambao walifariki siku ya juzi katika mji wa Moshi wakiwa katika ibada. Huu ni msiba mzito sana kwa wananchi wa Moshi hususani ndugu na jamaa wa marehemu," alisema na kuongeza:

# Magufuli atuma rambirambi

INATOKA UK. 3

ambao mikoa yao imepatwa na madhara ya watu kupoteza maisha kutokana na madhara ya mvua, kufikisha salamu zake za pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na wote waliguswa na vifo hivyo.

Rais Magufuli alitoa wito kwa Watanzania wote kuchukua tahadhari katika matukio yote yenye viashiria vya hatari ikiwamo mikusanyiko mikubwa ya watu na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha na amevitaka vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha vinasimamia ipasavyo tahadhari za kiusalama.

HABARI KITAIFA

# Baraza la Kilimo lajitosa tishio la nzige

Na Gwamaka Alipipi

BARAZA la Kilimo Tanzania (ACT) limesema limejipanga kukabiliana na wadudu aina ya nzige ambao wamekuwa tishia jirani ya Afrika Mashariki endapo wataingia nchini.

Limesema limeshawasiliana na Wizara ya Kilimo na wameshaweka mikakati ya kupambana na wadudu hao na kuwataka wakulima nchini kutokuwa na hofu.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya ACT, Dk. Jacqueline Mkindi, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati akielezea kongamano la kilimo biashara linalotarajia kufanyika kuanzia Februari 27 hadi 28, mwaka huu.

"Tumeanza kulizungumzia suala la nzige, tumeshawasiliana na Wizara ya Kilimo, tumejiandaa vizuri kupambana na wadudu hao endapo wataingia nchini," alisema Dk. Mkindi.

Kuhusu kongamano hilo, Dk. Mkindi alisema mgeni rasmi katika kongamano hilo ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, na kauli mbiu itakuwa 'Kuongeza tija katika kilimo na mifugo kwa maendeleo ya viwanda'.

Alisema kauli mbiu hiyo inaweka bayana haja ya majadiliano ya kina juu ya sera zilizopo pamoja na changamoto zake katika sekta ya kilimo.

"Kongamano hilo litaambatana na maonyesho makubwa ya bidhaa za kilimo, mifugo na uvuvi sambamba na teknolojia mbalimbali katika maeneo hayo, wadau wa sekta ya kilimo watapata fursa ya kuonyesha bidhaa na teknolojia mbalimbali," alisema Dk. Mkindi.

Alisema kongamano hilo ni la wadau wote walioko katika sekta ya kilimo ndani na nje ya nchi na kwamba wadau wa kilimo zaidi ya 400 wanatarajiwa kushiriki.

Dk. Mkingi alisema wadau wa kilimo wanaotaka kushiriki kongamano hilo wanapaswa kujisajili na kufanya malipo kwenye akaunti za ACT kama vilivyoainishwa kwenye fomu ya usajili katika tovuti ya baraza.



Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi, Wafanyabiashara Wadogo na wa Kati wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, akiteta jambo na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Elius Mwakalinga kwenye hafla iliyowakutanisha Benki ya NMB na makandarasi wa Kanda ya Ziwa jijini Mwanza jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yadhamini makandarasi wazawa 500

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya NMB mwaka jana imetoa zaidi ya dhamana 500 kwa makandarasi wazawa ili kuwawezesha kugharimia miradi mbalimbali ya ujenzi nchini.

Mkakati huo ulifikiwa kufuatia kilio cha muda mrefu cha makandarasi kushindwa kushiriki katika ujenzi wa miradi mbalimbali kutokana na ukata wa fedha na ushindani toka kwa kampuni za nje. Akizungumzaa wakati wa kongamano lililohudhuriwa na zaidi ya makandarasi 200 kutoka Kanda ya Ziwa mwishoni mwa wiki, Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi, Wafanyabiashara Wadogo na wa Kati wa NMB, Filibert Mponzi, alisema zoezi hilo litakuwa endelevu.

Alisema mbali na kusaidia kuwanyanyua makandarasi wadogo kimtaji, pia benki hiyo imeitikia wito wa Rais John Magufuli alioutoa juu ya taasisi mbalimbali za kibenki kuwakopesha makandarasi kwa masharti nafuu.

"Kama benki ya biashara na kama mbia wa serikali tumeshiriki kikamilifu kuwasaidia makandarasi kimtaji na pia kuitikia wito wa Rais Magufuli kuhakikisha kada hiyo inashiriki kikamilifu katika ujenzi wa uchumi," alisema Mponzi. Mkakati wa kutoa dhamana kwa makandarasi umesaidia sana kuwawezesha kupata kazi za uhakika za ujenzi na kwa mujibu wa Mponzi benki inatoa dhamana ya asilimia 50 ya thamani ya mradi husika.

Mbali na kutoa dhamana ya mikopo NMB pia itaanza kutoa huduma ya bima kwa makandarasi hao kuwawezesha kushiriki kwa ufanisi zaidi kwenye miradi mbalimbali kwa riba nafuu.

Hata hivyo, alisema wakati benki ikibuni njia mbalimbali za kuwasaidia makandarasi wadogo na wazawa kuna umuhimu mkubwa kwao kuwa waaminifu katika urejeshaji wa mikopo na kuheshimu masharti ya dhamana ili kuepuka kulipa riba kubwa kama adhabu baada ya mikataba kukiukwa.

Katika kongamano hilo lililohudhuriwa pia na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Eliud Mwakalinga, makandarasi walijadili changamoto mbalimbali na kushauri mikakati mbalimbali ya kupambana nazo.

Akizungumza nao, Mwakalinga mbali na kuishukuru NMB kwa ubunifu na huduma za mikopo na dhamana kwa makandarasi wazawa, alisema kazi za ujenzi zinahitaji uaminifu mkubwa na kuzingatia ubora.

Alisema utafiti mbalimbali unaonyesha makandarasi wazawa hasa wadogo wamekuwa wakishindwa kupewa kazi kubwa kwa zababu kadhaa zikiwamo wengi kushindwa kuajiri wahandisi waliobobea na wenye weledi usiotiliwa shaka.

"Tumefanya utafiti na kugundua kuna shida kubwa kwa makandarasi wengi wadogo kushindwa kukaa na wahandisi waliobobea kwa kukwepa kuwalipa mishahara wanayostahili na kuishia kuajiri wahandisi wanafunzi na hata mafundi mchundo tu," alisema.

Mwakalinga alidokeza mbinu kadhaa za kuwawezesha makandarasi wadogo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanashindana katika kujenga miradi mikubwa inayoshikiliwa na kampuni nyingi za nje.Mwenyekiti wa chama cha makandarasi mkoani Mwanza, Mhandisi Oscar Munishi, aliwataka makandarasi wazawa kujitathmini juu ya uadilifu wao kazini na kwamba kuna upungufu kadhaa unaohitaji kufanyiwa kazi miongoni mwao.

Aliyashukuru benki yalizojitokeza kuwadhamini kwa mikopo ya riba nafuu na akaishukuru NMB kwa kukutana nao na kujadili nao namna ya kuboresha utendaji kazi na kushindana kikamilifu sokoni.

Baadhi ya wandarasi waliozungumza na gazeti hili walilaumu utaratibu wa serikali kutwaa miradi mingi ya ujenzi wa majengo yake kwa kutumia force account na kwamba utaratibu huo umewaathiri sana kiuchumi.

Riziki Cyprian, alisema unafuu kidogo umebaki kwenye miradi ya ujenzi wa barabara na akaishukuru NMB kwa kumsaidia dhamana ya mikopo mara tatu iliyomwezesha kupata tenda kwenye miradi kadhaa mwaka jana.

# Kilimo, madini kuchangia ukuaji uchumi

Na Enock Charles

UTAFITI uliofanywa na Benki ya Standard Chartered nchini, umeonyesha kuwa uchumi wa Tanzania unatarajia kukua kwa asilimia 6.5 mwaka huu, huku kilimo na madini zikitarajiwa kuchangia zaidi katika kufikia kiwango hicho.

Akizungumzia mtazamo wa benki hiyo kwa ukuaji wa uchumi kwa nchi za Afrika Mashariki, Mkurugenzi wa Uchumi kwa Bara la Afrika wa benki hiyo, Sarah Baynton-Glen alisema kuwa sekta ya kilimo inatarajia kuchangua zaidi katika ukuaji wa uchumi kwa Tanzania ikilinganishwa na sekta zingine za kiuchumi.

"Kutokana na kurahisishwa kwa sera ya fedha ya mwaka 2018/2019, faida katika sekta binafsi imeanza kuongezeka ikilinganishwa na mwaka 2017 ilipokuwa na hali mbaya," alisema Glen.

Alisema kuwa pato la ndani linatarajia kufikia asilimia 6.5 ikilinganishwa na asilimia 6.6 kutoka kiwango cha mwaka 2019, shughuli za uchaguzi mkuu zikitajwa kushusha kiwango hicho cha pato la taifa kwa asilimia moja ikilinganishwa na mwaka jana .

Alisema kutokana na kurahisishwa kwa sera ya fedha ya mwaka 2018/2019 matokeo yanaonyesha kukua kwa sekta binafsi ikilinganishwa na miaka miwili iliyopita, akitolea mfano sekta ya madini, Glen iliyokua kwa asilimia 26 kufikia mwishoni mwa mwaka kutokana na bei ya madini kuwa nzuri, kuuzwa kwa korosho katika masoko ya nje.

Alisema Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imefanya vizuri kwa kupunguza riba ya mikopo katika benki na sekta za kifedha na kurahisisha mikopo kwa wakopaji na wenye mitaji midogo.

# Benki ya DCB yakuza faida kwa asilimia 43

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya biashara ya DCB (DCB Commercial Bank Plc) imetangaza kupata faida ya shilingi bilioni 2.3 katika mwaka 2019, ikiwakilisha ongezeko la asilimia 43 kutoka faida ya mwaka 2018 ambayo ilikuwa shilingi bilioni 1.6.

Katika taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari, kwa mujibu wa sheria za benki kuu, utendaji wa benki umeendelea kuimarika ikilinganishwa na mwaka uliotangulia, huku ufanisi katika nyanja zote muhimu ukiongezeka kwa kiwango cha kuridhisha.

Akiwasilisha taarifa za fedha za robo ya nne ya mwaka 2019, Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya DCB, Zacharia Kapama, ameeleza kuwa mafanikio haya yametokana na ukuaji wa mizania ya benki, ambao umechagizwa na ukuaji wa amana za wateja kwa asilimia 14 (shilingi bilioni 10.1), ikilinganishwa na mwaka uliotangulia.

Ukuaji wa amana umeisaidia benki pia kuongeza ukuaji wa mikopo ambapo benki imefanikiwa kuongeza kiwango ghafi cha mikopo kwa asilimia 11 (shilingi bilioni 8.0), ambacho ni kiasi kikubwa ukilinganisha na ongezeko la mikopo katika miaka miwili iliyotangulia. Mikopo ghafi ya benki imekua kutoka shilingi bilioni 90.5 mwaka 2018 kufikia shilingi bilioni 93.3 mwaka 2019.

Ili kufikia kiwango hiki, alisema benki imefanikiwa kutoa mikopo mipya kwa wateja wake kinachofikia shilingi bilioni 60, huku shilingi bilioni 18 zikiwakilisha mikopo kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati (SMEs), na Shilingi bilioni 10 ikiwakilisha mikopo ya wanawake na vijana. Benki pia imeendelea kutoa mikopo kwa sekta mbalimbali zikiwamo sekta binafsi za biashara, elimu afya na ujenzi.

Akielezea upatikanaji wa faida, Ndugu Kapama aliainisha kuwa ukuaji wa faida, ukiachilia mbali kuchangiwa na ukuaji wa mizania, pia umechagizwa na ongezeko la mapato yasiyotokana na riba baada ya benki kufanikiwa kukuza idadi ya wateja wake kutoka 175,000 mwaka 2018 kufikia wateja 194,000 mwaka 2020. Ongezeko hili limeongeza idadi ya akaunti za amana na miamala ya kibenki, huku wateja wakifurahia huduma za kidijitali bila kwenda matawini.

Kwa kuongezea, ufanisi wa benki umeongezeka hasa katika usimamizi wa matumizi ya riba na yasiyoyariba. Benki imefanikiwa kudhibiti ukuaji wa matumizi yasiyo ya riba, huku ikihakikisha huduma kwa wateja zinaboreshwa.

Aidha, alisema benki pia imefanikiwa kudhibiti ongezeko la riba kwa wateja na kuhakikisha wateja wanapata thamani bora ya huduma zake bila kuathiri ukuaji wake.

Kapama pia aliainisha upunguaji wa mikopo chechefu ya wateja kutoka asilimia 19 mwaka 2018 kufikia asilimia 13 mwaka 2019. "Hii imetokana na juhudi za benki kuhakikisha kuna ufanisi na usimamizi madhubuti katika utoaji mikopo na ukusanyaji madeni. Benki itaendelea na juhudi za kuhakikisha mikopo chechefu inafikia kiwango kinachokubalika na wadau wa sekta ya fedha mnamo mwaka huu wa 2020," alisema.

# Mount Meru kuanza kusafisha figo

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Rufani ya Mount Meru, mkoani Arusha, ina mpango wa kuanza kutoa huduma ya kusafisha figo.

Huduma hiyo inatarajiwa kuanza mra baada ya kukamilika kwa ujenzi wa jengo litakalogharimu Sh. milioni 600.

Hayo yalielezwa Juzi na Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Shafii Msechu, wakati akizungumza na waandishi wa habari na maofisa mawasiliano wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, katika kampeni yake ya 'Tumeboresha Sekta ya Afya'.

Lengo la ziara hiyo ni kuangazia mafanikio ya serikali yalipopatikana katika sekta ya afya kwa kipindi cha miaka minne.

Alisema upimaji wa eneo la ujenzi wa jengo la kutolea huduma hiyo, umekamilika na wanasubiri fedha kutoka serikali ili kuanza ujenzi huo.

"Hospitali ya Mount Meru inatarajia kuanza kutoa huduma za usafishaji wa figo na tayari tuna mashine tano za kuanza kutoa huduma hii tulizopewa na wizara na wadau wa afya na tunachosubiri ni fedha za kuanza ujenzi," alisema Dk. Msechu.

Alieleza sababu za kuanzisha huduma hiyo ni kutokana na kuwapo kwa wagonjwa wenye matatizo hayo, lakini kutokana na kutokuwa na huduma hiyo wamekuwa wakiwapeleka hospitali nyingine.

Dk. Msechu alisema kwa mwezi wanapokea wagonjwa watatu wa figo wanawahamishia katika Hospitali ya Rufani mkoani Kilimanjaro (KCMC).

Kuhusu huduma za matibabu wanazotoa alisema kwa siku wanapokea wagonjwa wapya 320 hadi 500, wa marudio 250 hadi 350 na watoto 30 hadi 50.

Alisema wana madaktari bingwa wa kufanya upasuaji na asilimia 34 wanawafanyiwa wajawazito ambao idadi yao ni 200 kila mwezi.

Kadhalika alisema wanatoa msamaha wa matibabu ya wagonjwa 3,224 kwa mwezi na wanagharamia Sh. milioni 41.8.

Dk. Msechu anasema malengo ya hospitali hiyo ni kuwa na mashine za vipimo vya MRI na CT-Scan ambazo kwa sasa hawana hivyo wanashirikiana na hospitali binafsi kupata huduma hiyo kwa sasa.




Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya Biashara ya DCB, James Ngaluko (wa pili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, wakati benki hiyo ikitangaza taarifa zake za fedha. Wengine kutoka kushoto ni Mkurugenzi wa Masoko na Mawasiliano, Rahma Ngassa, Mkurugenzi wa Fedha, Zacharia Kapama na Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi, Fortunata Benedict. **MPIGAPICHA WETU**

# Wajasiriamali wamwagiwa mamilioni

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

HALMASHAURI ya Ushetu mkoani Shinyanga, imetoa kiasi cha shilingi milioni 67.5 kwa ajili ya vikundi 14 vya kinamama, vijana na watu wenye ulemavu, ikiwa ni sehemu ya shilingi milioni 216.55 zilizokuwa zimetengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020.

Akikabidhi fedha hizo jana Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hiyo, Kichere Mwita, alisema vikundi ambavyo vinanufaika na fedha zinazotolewa na halmashauri ni vikundi vya kinamama ukilinganisha na vikundi vya vijana na watu wenye ulemavu.

Alisema halmashauri imetoa kiasi cha shilingi milioni 67.5 kwa vikundi 14 vya kinamama, vijana na watu wenye ulemavu, vikundi vya kinamama 11 vikipata milioni 52.5 huku vikundi vya vijana vitatu vikipata kiasi cha shilingi milioni 15.

Aidha, Mwita alisema kuwa, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 hadi 2019/2020 zaidi ya vikundi 77 vya kinamama vilipata mikopo ya riba nafuu wa zaidi ya Sh. milioni 272 na vikundi 38 vya vijana vilipata kiasi cha shilingi milioni 146.7 Aliongeza kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 hadi mwaka huu wa fedha 2019/2020 vikundi vinne vya watu wenye ulemavu vimepata kiasi cha shilingi milioni 12 na kuongeza kuwa mbali na kuwapati mikopo hiyo wamekuwa wakiwapati elimu ya uendeshaji wa shughuli za miradi.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Juma Kimisha, alisema mbali na changamoto ya ukosefu wa maofisa maendeleo ya jamii ngazi ya kata, wamekuwa wakiwatumia watendaji wa kata wenye elimu ya maendeleo ya jamii katika kutoa elimu sahihi ya matumizi ya mikopo hiyo.



# UVCCM yapinga shinikizo la mataifa Ulaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), umesema haukubaliani na masharti, matakwa na mashinikizo yanayotolewa na mataifa ya Ulaya namna serikali ya Tanzania kuongoza nchi.

Akizungumza wakati wa kongamano la kitaifa la UVCCM liliofanyika jijini Arusha, kuelekea wiki ya maadhimisho ya miaka 43, ya chama hicho, Mwenyekiti wa UVCCM Taifa, Kheri James, alisema UVCCM haukubaliani na mashinikizo yanayotolewa na mataifa ya Ulaya.

"Hatuta kubali shinikizo lolote kutoka kwa mataifa makubwa namna ya kuongoza nchi yetu, bali tutaiendesha na kuiongoza nchi kwa mujibu wa katiba ya nchi," alisema James. Kauli hiyo, imetokana na taarifa iliyotolewa hivi karibuni na Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ya kumpiga marufuku Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kuingia Marekani, pamoja na kupiga marufuku Watanzania kushiriki katika bahati nasibu ya kupata viza ya kuingia Marekani.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Michael Pompeo, kupitia mtandao wake wa kijamii wa Twitter alisema wana taarifa za uhakika kuwa Makonda alihusika katika uvunjifu wa haki za binadamu, kuwakandamiza wapinzani wa siasa, kuminya haki ya kujieleza.

"Wasifikiri kuwa watatupangia kama wanavyotaka wao, nchi hii ina amani, inajali haki za binadamu na utawala bora wa kisheria," alisema James.

James alisema mataifa hayo yanaweza kuishauri serikali na siyo kuipangia namna ya kuongoza kwa kuwa Tanzania siyo koloni la mataifa hayo.

Alisema kama madai ya Tanzania hakuna amani na kuna uvunjifu wa haki za binadamu mbona takwimu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha mwaka 2015/20 watalii wengi walikuja kutoka nchi za ulaya.

"Wanasema hakuna amani, uhuru wa kujieleza na uvunjifu wa haki za binadamu, takwimu zinaonyesha kwa mwaka 2015/20 watalii wengi wametoka katika mataifa hayo," alisema James na kuongeza.

"Tunataka waheshimu diplomasia yetu, watuache tujiendeshe wenyewe, kama wakiendelea na kutufuatilia basi naona diplomasia hii itaingia shakani," alisema James.

Aidha, alitoa onyo kwa baadhi ya wanasiasa wa vyama vya upinzani wanaokwenda nchi za nje kuisema nchi Tanzania ili isipate misaada kutoka mashirika na taasisi kubwa duniani. "Wapinzani wa nchi hii tumewadekeza sana na mtoto ukimdekeza kupita kiasi mwisho wa siku atakojolea kikombe cha kahawa, tukiendelea kuwadekeza hawa wapinzani wataiharibu amani na nchi itafikia pabaya, eti wanasema tusipewe fedha kwa kuwa serikali itazitumia kununua vyuo vya CCM na katika uchaguzi mkuu, tunaomba wananchi wapuuzie propaganda hizo," alisema James.

Naye Katibu wa CCM Mkoa wa Arusha, Mussa Matoroka, alisema chama hicho, kimejipanga kushinda majimbo yote ya uchaguzi mkoani humo.



Diwani wa Kata ya Naberera wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Haiyo Yamati, akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Ushuru madini ujenzi kuanza

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

KAIMU Ofisa Madini Mkoa wa Manyara, Mhandisi Godfrey Nyanda, amesema wataanza kutoza ushuru kwenye madini ya ujenzi kwa makandarasi wanaojenga miradi ya barabara ili kuiongezea serikali mapato.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na Nipashe na kueleza kuwa wanatarajia kutoza madini hayo husani kwa Wakala wa Barabara (Tanroads), na Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (Tarura).

Nyanda alitaja madini ujenzi kuwa ni pamoja na vifusi, mawe, kokoto, moramu na matofali ya kuchoma.

Alisema ushuru wa madini hayo utatofautiana kulingana na aina ya madini husika.

Alisema kuwa madini aina ya mawe tani saba yatatozwa ushuru wa kuanzia Sh.60,000 hadi Sh. 70,000 na kila safari moja ya gari itakatwa asilimia nne.

Wakizungumza na Nipashe, Mkazi wa Babati Halima Abdalla, alisema sekta ya madini kutoza ushuru makandarasi ni jambo jema kwa kuwa watapata fedha nyingi za ujenzi wa barabara.

Mkazi wa Bagara John Daud, aliishauri serikali kutowabana makandarasi hao ili wasiharibu barabara na kuzijenga chini ya kiwango.

Naye Anna Benard alisema watu wa madini wakibanwa ni jambo jema kwa kuwa awali waliachwa huru kuchimba na jamii inayozunguka maeneo ya machimbo waliachiwa mashimo watupu ambayo hayana madini.

# Wafanyabiashara 500 wa madini watimuliwa sokoni

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAFANYABIASHARA wadogo wa madini zaidi ya 500 wametimuliwa katika soko la madini jijini Arusha kutokana na kutokuwa na leseni ya kufanya biashara hiyo.

Wakizungumza na waandishi wa habari nje ya soko hilo, baadhi ya wafanyabiashara hao, walisema kuwa hatua hiyo imesababisha washindwe kufanya biashara hiyo baada ya kuzuiliwa na askari kwa madai ya kutokuwa na leseni.

Ernest Mathias mmoja wa wafanyabiashara hao alisema miongoni mwao wapo 68 waliokamatwa na Jeshi la Polisi kwa madai ya kufanya biashara hiyo nje ya soko kinyume cha sheria.

Alisema, wafanyabiashara wadogo wanategemea kupewa madini na wafanyabiashara wakubwa wakauze na baadaye kupata ujira mdogo kuanzia Sh. 5,000.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wa Madini Taifa (Tamida), Thomas Munisi, alisema sheria ya madini iliyowekwa na serikali inatakiwa kufuatwa na kwamba wafanyabiashara hao wanatakiwa kukata leseni ili wafanye biashara bila ya kusumbuliwa.

Alisema gharama ya kukata leseni kwa wafanyabiashara wadogo ni zaidi ya Sh. 250,000 na wengi wao hawana uwezo wa kifedha. Katibu Mkuu wa Wafanyabiashara wa madini, Noel Ole Valoya, amethibitisha kukamatwa kwa wafanyabiashara hao na kusema kuwa walifanikiwa kutoka kwa dhamana.

Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa Arusha, Mhandisi Hamisi Kamando, alisema wafanyabiashara wa madini wanaoruhusiwa kufanya biashara ya madini katika soko hilo ni wale wenye leseni kubwa, ndogo na leseni ya uchimbaji pekee. Alisema soko la madini siyo vijiwe vya wanaharakati, wanasiasa au sehemu ya kupiga umbea bali ni sehemu ya watu kufanya biashara.

# CEGODETA yawapa neno Watanzania uchaguzi mkuu

**Na Sabato Kasika**

TAASISI ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), imewataka Watanzania waanze sasa kuchunguza ni watu gani wanafaa kuwaongoza, ili wakati wa uchaguzi mkuu wafanye maamuzi sahihi.

Wito huo ulitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Thomas Ngawaiya, alipokuwa akizungumza na gazeti hili, jijini Dar es Salaam jana kuhusu uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba mwaka huu.

"CEGODETA inaona kuna ya Watanzania kujiwekea mchakato huo mapema kwa kuwapeleleza watu na kama wataona wanafaa, basi wawashauri waingie kwenye kinyang'anyiro," alisema Ngawaiya. Ngawaiya alisema, mtindo wa kusubiri hadi mwishoni unaweza kusababisha kupata viongozi wasiofaa, hivyo taasisi yake inashauri wananchi waanze mapema kwa ajili ya kupata wawakilishi bora serikalini na bungeni.

"Maisha yetu yategemea uongozi bora bila kujali chama, hivyo katika jambo hili, wananchi waanze uchunguzi au upelelezi ili kupata watu makini, na wakati ukifika, wawambie wachukue fomu bila kujali chama," alisema.

Alisema, Watanzania wakizingatia hilo, watapata viongozi bora na siyo bora viongozi, kwa vile mchakato wa kuwapata watakuwa wameuanza mapema kuliko kusubiri mwishoni na kujikuta wakichagua wasiofaa.

Mbali na hilo, mkurugenzi huyo pia aligusia suala la kuvuna maji ya mvua, na kusema, umefika wakati sasa Watanzania wawe na utamaduni wa kuvuna maji hayo ili yasiendelee kupotea.

"Kwa nchi za wenzetu zinazokumbwa na ukame mara kwa mara zimekuwa na utaratibu wa kuvuna maji ya mvua, hivyo siyo vibaya hata sisi Watanzania tukaiga mfano huo ili wakati wa kiangazi yatusaidie," alisema.

Alifafanua kuwa maji ya mvua yanaweza kuvunwa kwenye mapaa ya nyumba au watu kulima matuta ya kuyakinga na kutengeneza mabwawa kuliko hali ilivyo sasa, ambapo mvua zinaponyesha maji hayo hupotea.

Vile vile mwaka huu unaonekana ni wa neema, kwani mvua ni nyingi kuliko miaka mingine, ingawa madhara, hivyo wakulima wajitahidi kulima mazao mengi zaidi wapete ya ziada na kuyauza," alisema.



Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Kigoma, Ilvin Mugeta, akimkabidhi mkurugenzi wa kituo cha kulelea watoto yatima pamoja na watoto wanaoishi katika mazingira magumu cha Mokachi, Zainabu Burandeka, vyakula mbalimbali jana eneo la Kibirizi Manispaa ya Kigoma/Ujiji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Moro yataja sababu za kasi ajali za barabarani

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

UZEMBE na kutofuata sheria za barabarani umesababisha vifo vya madereva 16 wa pikipiki maarufu kama 'bodaboda' na abiria sita walifariki kutokana na ajali ya usafiri huo katika kipindi cha mwaka 2019, mkoani Morogoro.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa mkoa huo, Michael Deleli, alisema hayo wakati akijibu hoja mbalimbali za madereva wa bodaboda katika kikao cha pamoja kilichoitishwa na Mbunge wa Morogoro Mjini (CCM), AbdulAziz Abood.

Kikao hicho ambacho pia kilihudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Regina Chonjo na viongozi wa mamlaka zilizolalamikiwa na madereva hao, Kikosi cha Usalama Barabarani, na Mamlaka ya Usafishaji nchi Kavu (RATRA) pamoja na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA).

Akijibu hoja za waendesha bodaboda hao, Deleli alisema chanzo kikuu cha vifo hivyo ni wengi wao kutokutii sheria za usalama barabarani ikiwamo kutovaa kofia ngumu, kutokuwa na leseni, bima na kushindwa kusajili vyombo vyao.

Alisema baadhi yao wamekuwa wakiwagonga watembea kwa miguu yakiwamo maeneo ya alama za kuvuka kwa miguu, kukatisha kwenye alama nyekundu barabarani, kupita njia za waenda kwa miguu na kuyapita magari upande usiotakiwa.

"Tayari takwimu za mwaka huu zinaonyesha watu 15 waligongwa na bodaboda, jambo ambalo sisi Polisi wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoa hatutafumbia macho hata kidogo kwa madereva hao," alisema Deleli. Alisema Jeshi hilo litaendelea kutekeleza sheria zilizopitishwa na Bunge na kuwataka bodaboda na bajaji kufuata sheria za usalama barabarani ikiwa ni pamoja na kuwa na leseni, chombo wanachoendesha kuwa na bima na kusajili katika mamlaka zinazohusika.

Awali akiwasilisha malalamiko mbele ya kikao hicho, Katibu wa Kamati ya uchaguzi wa Uongozi wa Bodaboda, Patrick Matambo, alisema baadhi ya askari wa kikosi cha barabarani wanapowakamata wanawatoza faini kila kosa Sh. 30,000 tofauti na wenye magari ambayo hutozwa zaidi ya makosa moja kiwango kama hicho tofauti na wao .

Mbunge Abood alisema alikuwa akipokea changamoto nyingi kutoka kwa madereva bodaboda na bajaji wakiwalalamikia askari wa ngazi za chini ambao wakiwakamata na kuwaandikia makosa wakati mwingine si ya kweli wakiwa na lengo la kujipatia kipato.

Aliwashauri madereva wa bodaboda na bajaji kuunda uongozi wao ngazi ya Manispaa ili uwe ni kiungo cha kufikisha changamoto zao kwa viongozi akiwamo mkuu wa wilaya pamoja na mbunge wao ili ziweza kutatuliwa kwa wakati.

## RC Mwanri apokea msaada vifaa ujenzi, afya

**Na Tiganya Vincent,**
TABORA

KAMPUNI ya Tumbaku ya Alliance One Tanzania (AOTTL) imeukabidhi uongozi wa Mkoa wa Tabora vifaa mbalimbali vikiwamo vifaa tibaa na ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 19.8.

Msaada huo ulikabidhiwa jana na Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Kampuni hiyo, David Mayunga, kwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, katika hafla iliyofanyika ofisini kwake.

Mayunga alivitaja vifaa vilivyotolewa ni bati 200, saruji mifuko 250, magodoro 30, shuka za wagonjwa 110, vitanda vya wagonjwa 3 na kitanda maalumu kwa ajili ya mama kujifungulia kimoja.

Alisema msaada huo utapelekwa katika Kituo cha Afya cha Mazinge na Kituo cha Afya cha Mwamayunga vilivyopo wilayani Sikonge na Zahanati ya Igagala wilayani Kaliua.

Mayunga alisema kampuni hiyo imeamua kutoa msaada huo kupitia mpango wa urejeshaji wa huduma kwa ajili kuunga mkono juhudi za serikali za kuboresha huduma za afya na kuwapunguzia adha wananchi wa kwenda kupata huduma hizo mbali.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Tabora Mwanri aliitaka Idara ya Afya ya Mkoa huo kuhakikisha vifaa hivyo vinatunzwa na kutumika kwa malengo ya utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Alionya kuwa hatasita kuchukua hatua kwa watendaji wote waliopewa dhamana ya kutunza vifaa kuhakikisha haviibwi na kupelekwa kwenye majumba ya watu au kwa watoa huduma ya afya ambao sio walengwa. Kwa upande wa Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Abel Busalama, aliishukuru Kampuni ya Alliance One kwa msaada ya vitanda walivyotoa kwa ajili ya kuongezea nguvu Zahanati ya Igagala.

Alisema hatua hiyo ni muhimu katika kukabiliana na msongamano wa kupata vifaa vya kulaza wagonjwa katika zahanati hiyo.

Busalama alisema kutokana na zahanati hiyo kupata wagonjwa wengi kutoka sehemu mbalimbali wanao mpango wa kujenga kituo cha afya katika eneo hilo kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua, nguvu za wananchi na kuomba wadau wengine kuunga mkono juhudi hizo.


NIPASHE JUMATATU FEBRUARI 3, 2020

Nipashe

# Spotika




WANAMICHEZO 10 WENYE WAFUASI WENGI INSTAGRAM UK. 20



## ISIKUPITE

MOHAMED Salah amefunga mabao mengi (12) kwenye Ligi Kuu England katika uwanja wa nyumbani msimu huu kuliko mchezaji yeyote, tangu alipojiunga na Liverpool mwaka 2017, ni Lionel Messi (51) pekee mwenye mabao mengi ya uwanja wa nyumbani katika ligi tano kubwa bora Ulaya kuliko mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Misri (44).




# AKAUNTI IMEFUNGUKA...

Nahodha wa timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Mbwana Samatta akiifungia timu yake ya Aston Villa kwa kichwa bao la kufutia machozi kwenye mechi ya Ligi Kuu England, wakati wakikubali kipigo cha mabao 2-1 ugenini dhidi ya Bournemouth juzi. Bao hilo ni la kwanza kwa Samatta tangu ajiunge na klabu hiyo na huo ukiwa mchezo wake wa kwanza kwenye Ligi Kuu England. **HABARI UK. 32**

# NAFASI YA FERNANDES KUIBEBA MAN UNITED




**MANCHESTER, England**

USHAWISHI wa Manchester United kwa Bruno Fernandes hatimaye umefanikiwa na wameweza kukamilisha usajili wake kutoka Sporting CP Alhamisi iliyopita, na sasa mashabiki wa 'Mashetani Wekundu' hao watakuwa na hamu kubwa ya kumshuhudia.

Man United ilikamilisha usajili wa Bruno Fernandes kutoka Sporting CP, na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno amesaini mkataba wa miaka mitano na nusu wa kuitumikia klabu hiyo, ukiwa ni usajili mkubwa zaidi kwa klabu hiyo kwa dirisha hili lililofungwa kipindi cha majira ya baridi.

Kiungo huyo mbunifu hatimaye anajiungana na kikosi cha Ole Gunnar Solskjaer baada ya kuhusishwa kwa muda mrefu mno kusajiliwa na timu hiyo.

Nafasi ya kiungo imekuwa tatizo kubwa kwa United msimu huu na wangekuwa na wakati mzuri zaidi kama Paul Pogba na Scott McTominay wasingekuwa majeruhi.

Ujio wa Fernandes unatoa matumaini kwenye kikosi hicho na hapa tunaangalia mafanikio na uwezo wake wakati alipokuwa kule Ureno pale Sporting na namna gani alivyoweza kuisaidia klabu hiyo na tunalinganisha na kile atakachokifanya kwenye safu ya kiungo ya United.

### Kufunga na pasi za mwisho

Kufunga mabao limekuwa tatizo kubwa kwa United msimu huu, ikiwa na mabao 36 katika mechi 24 za Ligi Kuu na kuwa na idadi ndogo zaidi katika timu sita bora kwenye msimamo.

Fernandes anatakiwa kuisaidia Man Unite hasa ikizingatiwa kwamba amechangia mabao nane katika mechi 17 za Ligi Kuu ya Ureno, Primeira Liga. Mabao bora ya United yamekuwa yanatoka kwenye safu ya kiungo kutoka kwa McTominay (matatu katika mechi 17), huku Andreas Pereira akifunga moja tu katika mechi 21 na Fred (20), Jesse Lingard (19), Juan Mata (15), Nemanja Matic (8) na Pogba (7).

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 25, amekuwa msaada na nguvu kubwa kwa wachezaji wenzake kwa kugawa 'asisti', akiwa nazo saba. Pereira anazo tatu na Mata mbili sawa na Pogba. Fred, Lingard na Matic bado hajaweza kuwatengenezea mabao wachezaji wenzao.

Kwa ujumla kuhusika kwake kwenye mabao 15 ni bora zaidi kuliko mabao 11 waliochangia kwa pamoja Pereira na McTominay.

Fernandes pia ana uwiano mzuri wa jumla ya mabao 102 aliyohusika nayo. Pogba ndiye mchezaji mwenye rekodi bora katika hilo pale United, ingawa amecheza mechi chache.

### Mashuti, kutengeneza nafasi

Solskjaer kwa namna yoyote atatumainia Fernandes kuwa na uwezo wa kuiendesha safu ya kiungo na ishara zinaonekana kuwa chanya.

Fernandes amepiga mashuti 60 kwenye ligi akiwa na Sporting kwa msimu wa 2019-2020, ikiwa ni 25 zaidi ya Pereira, ambaye ndiye mwenye idadi kubwa kwa mashuti kwa United.

Uwapo wa Anthony Martial, Mason Greenwood na Marcus Rashford - wakati atakaporudi kutoka kuuguza majeraha ya mgongo pia kutakuwa na matumaini ya kupata huduma nzuri ya Fernandes.

Ametengeneza nafasi 63 msimu huu, ikiwa sawa na dakika 24 kwa nafasi moja. Kwa sasa pale Man United Pereira ndiye anashikilia rekodi ya kutengeneza nafasi nyingi zaidi akiwa ametengeneza 31.

Hivyo kwa namna yoyote, ujio wa Fernandes utakuwa na mchango mkubwa kwa kikosi cha Man United hasa katika kutengeneza nafasi nyingi zaidi za kufunga pamoja na kuwagawia mipira wachezaji wengine.

Hivyo, sasa safu ya kiungo ya Man United inaweza kuwa bora zaidi kuliko wakati mwingine wowote.

**JE, WAJUA?**



KUFUZU fainali kwa Aston Villa wiki iliyopita kwenye Kombe la EFL, kunaifanya sasa kutinga hatua hiyo mara ya tisa (sawa na Manchester United) na ni Liverpool pekee (mara 12) iliyotinga fainali mara nyingi zaidi katika michuano hiyo zaidi yake.

MICHEZO

# SAMATTA NYAVUNI BONGO HADI ULAYA

**Na Adam Fungamwango**

MBWANA Samattta, Mtanzania wa kwanza kucheza Ligi Kuu ya England, amefunga bao la kwanza kwenye mechi yake ya kwanza kucheza katika ligi hiyo.

Samatta alifunga bao Jumamosi kwenye Uwanja wa Dean Court, wakati timu yake ya Aston Villa ikiwa ugenini dhidi ya AFC Bournemouth.

Pamoja na kufungwa mabao 2-1, lakini Watanzania wengi wameonekana kufurahishwa mno na bao la dakika ya 70 lililofungwa na raia mwenzao huyo aliyewahi kuzichezea klabu za African Lyon na Simba, kabla ya kuuzwa TP Mazembe na KRC Genk ya Ubelgiji na hatimaye kutua England.

Ni bao litakalobakia kwenye vitabu vya kumbukumbu na ni mwanzo mzuri wa Samatta kwenye ligi hiyo ngumu, bora na yenye mvuto duniani.

Kwenye vibanda umiza, baada ya Mbongo huyo kufunga, mashabiki walilipuka kwa nderemo na hoihoi, kuashiria kumuunga mkono mwenzao.

Hata hivyo, si wengi ambao wanakumbuka mabao aliyoyafunga Samatta akiwa nchini Tanzania. Baadhi walikuwa hawajaanza kufuatilia mambo ya soka.

Na wengine walikuwa bado wadogo, hivyo hawajui ni kitu gani alikifanya Samatta kwenye Ligi Kuu ya Tanzania.

Hadi anasajiliwa na TP Mazembe, alikuwa amefunga mabao 13 kwenye msimu wake mmoja na nusu aliocheza, akiwa na timu za African Lyon na Simba, huku akipiga 'hat-trick' moja. Aliifungia African Lyon mabao sita kwa msimu mmoja, huku akiifungia Simba mara saba kwa nusu msimu aliyocheza.

Mwandishi wa makala haya amekusanya mabao yote ya Samatta aliyoyafunga Bongo, wakati huu akiwa ameanza kuendeleza rekodi yake ya utupiaji akiwa England...

**1. African Lyon 6-1 Toto African (2009/10)**

Alifunga mabao mawili Septemba 26, 2009 kwenye mechi ya Ligi Kuu, African Lyon ikiiangamiza Toto African 6-1, mabao mengine yakifungwa na Rashid Gumbo, Robert Ssentongo na Yusuph Soka akifunga mawili.

**2. African Lyon 2-1 Manyema FC (2009/10)**

African Lyon iliichapa Manyema mabao 2-1 kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Septemba 20, 2009, mechi ikichezwa Uwanja wa Uhuru, Ligi Kuu msimu wa 2009/10 kwa mabao ya Yusuph Soka na Samatta akipiga bao la pili dakika ya 79.

**3. African Lyon 1-0 Mtibwa Sugar (2009/10)**

Mechi hii ilichezwa kwenye Uwanja wa Manungu mjini Morogoro, Mtibwa Sugar ikilala kwa bao 1-0 nyumbani dhidi ya African Lyon, bao la Mbwana Samatta dakika 74, Januari 24 mwaka 2010, msimu wa Ligi Kuu 2009/10.



**4. African Lyon 1-0 Manyema FC (2009/10)**

Dakika ya kwanza tu, Samatta alifunga bao pekee lililoipa ushindi African Lyon dhidi ya Manyema kwenye Uwanja wa Uhuru, zamani ukiitwa Uwanja wa Taifa na hiyo ilikuwa na Februari 20, 2010.

**5. African Lyon 2-0 Majimaji (2009/10)**

Ilikuwa ni Machi 12, 2010 kwenye Uwanja wa Uhuru, Lyon ilipoibabua Majimaji ya Songea mabao 2-0, Samatta akifunga bao la pili, Stephano Mkomolwa akitangulia kufunga bao msimu huo wa ligi.

**6. Simba 3-0 African Lyon (2010/11)**

Wakati akiifungia Aston Villa bao la kwanza kwenye Ligi ya ya England Februari Mosi 2020, Samatta alianza kuifungia Simba Februari 3, 2011, ikicheza na timu yake ya zamani ya African Lyon.

Ilikuwa ni baada ya kutimiza masharti yake ya kumpa gari, mzunguko wote wa kwanza Samatta aligoma na hakucheza mechi yoyote, lakini alianza shughuli mzunguko wa pili wa Ligi Kuu msimu wa 2010/11. Kwenye mechi yake hiyo ya kwanza akiwa Simba alifunga mabao mawili, Simba ikichapa African Lyon 3-0, bao la kwanza likifungwa na Amri Kiemba.

**7. Simba 2-2 Toto African (2010/11)**

Mechi hii ilichezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba mjini Mwanza, Simba ikilazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Toto African kama kawaida yao. Tete Kang'anga na Mohamed Sudi waliifungia Toto, mechi iliyochezwa Februari 16, 2011, Samatta na Rashid Gumbo aliyetoka naye Lyon, wakiifungia Simba.

**8. Simba 4-1 Mtibwa Sugar (2010/11)**

Hii ndiyo mechi ambayo Samatta alipiga 'hat-trick'. Ilikuwa ni Februari 27, 2011 kwenye Uwanja wa Uhuru, Simba ikiiadhibu Mtibwa Sugar mabao 4-1. Samatta alifunga mabao matatu dakika ya 13, 66 na dakika 90 kwa mkwaju wa penalti, goli lingine likifungwa na Kiemba, na la kufutia machozi la Mtibwa likiwekwa wavuni na Hussein Javu.

**9. Simba 4-1 Majimaji (2010/11)**

Ilikuwa ni mechi ya mwisho wa msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Simba kutwaa ubingwa, lakini pia ilikuwa ni mechi ya mwisho ya Samatta kwenye ligi iliyochezwa Aprili 10, 2011 ikichezwa Uwanja wa Uhuru.

Simba ilishinda mabao 4-1 dhidi ya Majimaji, Samatta akifunga bao la nne dakika ya 71, Emmanuel Okwi akifunga mawili, Shija Mkina akifunga moja, Kassim Kilungo akiifungia Majimaji bao la kufutia machozi.

## NJE YA UWANJA

KWA hisani ya Mbwana Samatta, Aston Villa imepata bao lake la kwanza kwa njia ya kichwa kwenye Ligi Kuu England tangu Ciaran Clark alipofunga dhidi ya Watford Aprili 2016.






# SABABU 3 KWA NINI MAN CITY ITATAWALA MIAKA 10

**MNCHESTER, England**

KUCHOMOZA kwa Manchester City na kuwa timu bora kwenye soka la Uingereza kwa kipindi cha muongo mmoja uliopita kumetambulika. Walikuwa kwenye nafasi ya katikati katika msimamo wa ligi wakati Sheikh Mansour alipoinunua klabu hiyo mwaka 2008. Tangu hapo, hawajaangalia nyuma. Kwa kipindi cha muongo mmoja uliopita, City imejiimarisha yenyewe kama moja ya klabu tawala nchini England.

Wameshinda mataji manne ya Ligi Kuu, manne ya Ligi na mawili ya FA kwa muongo mmoja. Wanashikilia rekodi ya kushinda mechi nyingi zaidi, mabao mengi waliyofunga na pointi nyingi kwenye Ligi Kuu. Huku wakiwa wameshindwa kuonyesha utawala wao barani Ulaya, lakini kiwango chao kinaimarika kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kuibuka na kutawala soka la Uingereza kunaweza kutajwa kuwa sababu kubwa ni uwapo wa Pep Guardiola hapo Manchester. Raia huyo wa Hispania ameendeleza rekodi ya utawala kwa klabu hiyo. Sasa wakati muongo mpya ukianza, City inaweza kuwa moja ya klabu itakayotawala kwa kipindi kijacho cha miaka 10.

Hapa kuna sababu tatu kwa nini Manchester City inaweza kutawala soka la Uingereza kwa miaka mingi ijayo...

1.Nguvu ya fedha

Sheikh Mansour bin Zayed al-Nahyan wa familia inayotawala Abu Dhabi aliinunua Manchester City kwa pauni milioni 150 mwaka 2008. Tangu hapo ametumia zaidi ya bilioni kuimarisha klabu na kuwa bora.

Klabu isingeweza kuchomoza yenyewe na kufikia kwenye daraja la juu bila ya mmiliki wake kuwa na uwezo mkubwa wa kifedha. Amewekeza fedha nyingi kwenye klabu. Fedha zimetumika kuijenga klabu na kuwa moja ya daraja la juu kwa kununua wachezaji bora.

Mafanikio ya City yanaweza kupimwa na idadi ya mataji waliyoshinda na rekodi walizoziweka chini ya umiliki wa Sheikh Mansour. Ilikuwa klabu yenye mafanikio zaidi nchini England kwa miaka 10 iliyopita. Hata hivyo, klabu hiyo sasa inaonyesha ishara ya kuweza kujitegemea yenyewe kwenye suala la fedha.

Manchester City imeendelea kuongeza mapato yake kwa kipindi cha miaka ya hivi karibuni. Walitangaza rekodi ya klabu ya kupata pauni milioni 535.2 katika ripoti ya msimu wa 2018-19 na faida ya pauni milioni 10.1. Kiasi hicho chini ya mmiliki ambaye ni tajiri kinaweza kuihakikisha klabu hii kuendelea kukua zaidi kimapato kwa miaka inayokuja.

**2. Kikosi cha vipaji na sera nzuri ya ununuzi**

Man City imeweza kusajili wachezaji bora katika kila nafasi na kuwa moja ya timu yenye kikosi kipana. Kocha wake anaweza kuwaacha benchi wachezaji kama Riyad Mahrez na Gabriel Jesus, kitu ambacho kwa timu nyingine ni ndoto kuwa na wachezaji hao. Kuna msemo maarufu kwamba wanaweza kutengeneza timu mbili ambazo zote zinauwezo wa kutwaa taji la Ligi Kuu.

Moja ya sababu kubwa kwa kuwa na kikosi kama hicho ni sera nzuri ya kuwanunua wachezaji. Wako makini mno kwenye aina ya wachezaji ambao wanataka kuwasajili. Klabu inafanya haraka pale inapopata mchezaji aliyefikia vigezo vyake kumsajili.

City pia inajulikana kwa kusajili wachezaji wa kuziba nafasi ya wachezaji wakubwa. Mfano mzuri kwa sera hiyo ni Gabriel Jesus. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil anachukuliwa kama ndiyo mrithi wa Sergio Agüero. Sera hiyo inaisaidia klabu kuendelea kuwa na timu bora na yenye mafanikio dimbani. Ukiangalia kikosi cha City unaona wazi kwamba klabu itaendelea kutawala soka la Uingereza.

**3. Kuimarisha Akademi ya vijana**

Manchester City imetumia fedha nyingi kwa kusajili wachezaji wakubwa kwenye kikosi cha kwanza, hata hivyo, maendeleo kwa vijana yamekuwa yakiendelea kukua. Uongozi wa klabu unajua umuhimu wa kuwa na akademi ya vijana kwa ajili ya kuwa na mafaniko ya muda mrefu kwa timu hiyo. Timu yao ya vijana inaweza isiwe bora kama ile ya Chelsea, lakini bado wanaimarika.

Akademi ya vijana ya City sasa inaweza kuimarisha majina makubwa yenye vipaji barani Ulaya. Jadon Sancho amekuwa na wakati mzuri kule kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita. Winga huyo kijana ni zao la akademi ya vijana ya City. Brahim Diaz, ni zao jingine la akademi hiyo, hivi karibuni alisajiliwa na Real Madrid.


Phil Foden, naye ni zao la akademi ya City na sasa anacheza kama mtu muhimu kwenye kikosi cha kwanza na ametambulika kama mrithi wa David Silva. Uwekezaji kwenye akademi sasa unaanza kutoa matokeo mazuri, kitu ambacho kinaifanya City kuwa bora zaidi katika miaka inayokuja.

## Nukuu

"Kobe alikuwa gwiji. Kumpoteza yeye na Gianna ni maumivu makali mno moyoni hasa kwa sisi wazazi. Michelle (mkewe) na mimi tumetuma salamu za sala kwa Vanessa na familia yote ya Bryant juu ya siku hii isiyofikirika," **Rais wa zamani wa Marekani, Barack Obama aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter baada ya gwiji wa mpira wa kikapu, Kobe Bryant na mwanawe Gianna kufariki dunia kwa ajali ya helikopta Jumapili Januari 2, mwaka huu.**



"Ushindi mkubwa tumepata jana (Jumanne) usiku na ninafuraha kwa nafasi niliyopata, mwonekano bora kutoka kwa mashabiki na kiwango kikubwa tulichokionyesha, sasa tunaelekea Wembley (fainali dhidi ya Manchester City," **Mbwana Samatta baada ya kuichezea Aston Villa kwa mara ya kwanza wakati ikishinda 2-1 dhidi ya Leicester kwenye nusu fainali ya Kombe la Ligi, EFL Cup**



"Kobe Bryant, licha ya kuwa mchezaji bora zaidi wa wakati wote wa mchezo wa kikapu, ndio kwanza alikuwa akianza maisha. Aliipenda sana familia yake, na alikuwa na hamasa kubwa na majaliwa yake ya baadaye. Kumpoteza binti yake mzuri Gianna, kunaufanya wakati huu kuwa mgumu zaidi," **Rais wa Marekani, Donald Trump baada ya gwiji huyo kufariki dunia kwa ajali ya helikopta Jumapili Januari 2,**



# KOBE BRYANT NA AJALI ZA MASTAA WA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA ilishtushwa na kifo cha ghafla cha mchezaji nyota wa kikapu maarufu nchini Marekani na duniani kote.

Nyota huyo alifariki kwa ajali ya helikopta iliyotokea mji wa Calabasas, California Januari 26, mwaka huu.

Watu tisa walifariki kwenye ajali hiyo akiwamo binti yake kipenzi, Gianna mwenye umri wa miaka 13, huku nyota huyo wa NBA akiwa na miaka 41.

“Haukuwa kama mlipuko, lakini tulisikia kama bomu limelipuka kwa sauti kubwa. Lakini ilisikika kama sauti ya ndege au helikopta, ilisikika sauti kubwa sana, niliingia ndani na kwenda kumtaarifu baba yangu na kumwambia kilichotokea. Hivyo nilivyotoka nikaona moshi mweusi ukitokea mlimani, ulikuwa mweusi au kama kijivu,” alisema Gavin Masak, shuhuda mmoja anaishi karibu na eneo ambalo ajali ilipotokea akihojiwa na kituo kimoja cha kimataifa.

Ni moja ya ajali iliyowashtua wanamichezo wengi duniani ikiwamo Watanzania.

Ni ajali iliyowakumbusha mengi, kwani Tanzania imeshawahi kupoteza wanamichezo wengi, wakiwamo wacheza soka kutokana na ajali.

Ajali ni ajali, iwe ya helikopta, ndege, gari, bajaj, pikipiki na vyombo vingine vya moto zote ni ajali tu, na kwenye makala haya tumekusanya kumbukumbu ya wachezaji ambao walifariki kwa ajali kama Kobe Bryant...

**Said Mwamba ‘Kizota’**

Ni mmoja wa wachezaji wenye vipaji vya hali ya juu kuwahi kutokea kwenye ardhi ya Tanzania.

Jina lake kamili ni Said Nassor Yusuph Mwamba ambaye alizichezea klabu mbalimbali zikiwamo Simba, Yanga na timu ya Taifa, Taifa Stars.

Alikuwa na uwezo mkubwa wa kucheza nafasi mbalimbali uwanjani. Awali akiwa kijana mbichi aliicheza kama kiungo mshambuliaji akiwa klabu ya Yanga na kufanya vema kiasi cha kupewa jina la ‘Kizota’, ambao ulikuwa ukumbi maarufu wa mikutano mjini Dodoma.

Baadaye alibadilisha namba na kuwa mshambuliaji, tena hatari aliyefunga mabao mengi kwenye wasifu wake na kuipatia Yanga mataji mbalimbali ya Ligi Kuu, pamoja na Kombe la Kagame mwaka 1993 na 1999 zote zikifanyika nchini Uganda akifunga kwenye fainali zote hizo.

Alijiunga na Simba na kuifunga Yanga, lakini baadaye alirejea tena kwenye klabu yake aliyochezea kwa muda mrefu ya Yanga.

Kabla hajastaafu kucheza soka alibadilisha tena namba na kucheza beki wa kati, namba ambayo pia aliimudu vizuri sana.

Kizota alifariki kwa ajali ya gari Februari 11, mwaka 2007. Akiwa anatoka Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kutazama mechi ya soka Kombe la Shirikisho la Soka Afrika kati ya Simba dhidi ya Textil de Pungue ya Msumbiji.



Mafisango enzi za uhai wake.

Ajali hiyo ilitokea eneo ya Veterinary, maeneo ya Temeke jijini Dar es Salaam kwa kugongwa na gari wakati akivuka barabara.

**Patrick Mutesa Mafisango**

Mei 17, 2012, ilikuwa ni siku ya huzuni kwa mashabiki wa soka Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, na hasa wanachama na mashabiki wa Simba, walipopata taarifa mapema alfariji ya siku hiyo ya kifo cha kiungo wao maarufu, Patrick Mutesa Mafisango.

Mafisango aliyekuwa tegemeo kwa Simba, hasa kwenye nafasi ya kiungo mkabaji, lakini akiwa na kipaji cha kufunga, hasa mechi muhimu, alifariki kwa ajali ya gari maeneo ya Keko VETA jijini Dar es Salaam.

Ajali hiyo ilitokea usiku wa manane baada ya gari alilokuwa akiendesha kuingia kwenye mtaro, alipokuwa akimkwepa mwendesha bodaboda.

Alikuwa tayari ameifungia Simba mabao 11 kwenye msimu wake wa mwisho wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2011/12 na kuipa ubingwa.

Ilikuwa ni siku chache tu baada ya Simba kurejea kutoka nchini Sudan kucheza mechi ya Kombe la Shirikisho dhidi ya Al Shandy na kutolewa kwa mikwaju ya penalti.

Mafisango ambaye alikuwa Mkongomani mwenye uraia wa Rwanda, pia alikuwa nahodha wa timu ya Taifa ya Rwanda, Amavubi.

Simba ilimsajili mchezaji huyo mwaka 2011, akitokea Azam FC, ikiwa ni mabadilishano ya wachezaji, Simba ikimchukua kwa kubadilishana na Abdulhalim Humud ambaye yeye alipelekwa Azam FC. Alizikwa kijiji cha Lembe, Kinshasa nchini DR Congo.

**Barnabas Sekelo**

Ni beki wa zamani wa pembeni wa Simba aliyekuwa na uwezo mkubwa wa kufunga, aliyefariki dunia Juni 6, mwaka jana kwa ajali ya pikipiki maeneo ya Tazara jijini Dar es Salaam. Alikuwa na uwezo wa kucheza nafasi zote za kulia na kushoto.


Alicheza mechi nyingi na kuisaidia Simba kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini mechi inayokumbukwa zaidi aliyocheza na kufanya vizuri ni ile ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka 2002 dhidi ya Nkana Red Delvis.

Katika mechi ya kwanza nchini Zambia, Simba ilifungwa mabao 4-0, huku wachezaji wake sita wakifungiwa kwa kufanya fujo, lakini mechi ya marudiano iliyofanyika kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro, nusura Simba ipindue meza iliposhinda mabao 3-0, ikichezesha wachezaji wengi ambao si mastaa, ingawa ushindi huo hakuiwezesha timu hiyo kusonga mbele kwa kutolewa kwa mabao 4-3.

Katika mechi hiyo, Sekelo alifunga mabao mawili na kuwa moja ya mechi bora kabisa kuwahi kucheza.

Alifariki dunia wakati pikipiki aliyokuwa akiendesha ilipogongana na gari na kuzikwa maeneo ya Tandale jijini Dar es Salaam.

**NAJUA WAJUA**



TANGU kuanza kwa msimu uliopita, beki wa pembeni wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold ndiye mwenye pasi nyingi za mwisho ‘assists’ (22) kwenye Ligi Kuu England kuliko mchezaji mwingine yeyote katika ligi hiyo.

SOKA

# MABADILIKO MA3 CHANYA YA ARSENAL KWA ARTETA



**LONDON, England**

NI salama kucheza, kwamba Arsenal imeimarika tangu Mikel Arteta achukue mikoba ya kuinoa. Tangu nahodha huyo wa zamani wa Arsenal mwenye umri wa miaka 37, achukue mikoba kutoka kwa Unai Emery mambo yanaonekana kuwa chanya pale katika dimba la Emirates.

Kumekuwa na mabadiliko makubwa kwenye timu. Na makala haya inakuchambulia mabadiliko matatu chanya ya Arsenal chini ya Arteta.

**3. Umiliki bora wa mpira**

Kwa sasa Arsenal imekuwa na asilimia kubwa ya kumiliki mpira. Ikiwa na wastani wa asilimia 53.7%. 'Washikabunduki' hao msimu uliopita na mwanzoni mwa msimu huu walishindwa kufunga mabao mengi kutokana na ukweli kwamba walikuwa na tatizo kubwa kati ya safu ya kiungo na ushambuliaji. Wachezaji kama Pierre-Emerick Aubameyang, Alex Lacazette na Nicolas Pepe, hawakulishwa pasi za kutosha kuweza kufunga mabao.

Hata hivyo, tangu kuja kwa Mikel Arteta wamekuwa na uwiano mzuri zaidi wa kutengeneza nafazi za kufunga mabao katika kila mchezo. Katika mchezo wa kwanza wa Arteta akishika mikoba ya Arsenal, timu yake iliweza kupiga mashuti mengi zaidi. Katika mchezo wake dhidi ya Bournemouth pale Dean Court, Arsenal ilipiga mashuti 17 mengi zaidi ya iliyokuwa chini ya Emery ambapo idadi hiyo aliipata kwenye mechi tano.

Arsenal imeanza kupiga pasi za kwenda mbele na kutengeneza mashambulizi ya haraka tofauti na iilivyokuwa mwanzo.

**2. Kuimarika kiwango binafsi kwa wachezaji**

Granit Xhaka baada ya mgogoro wake na mashabiki baada ya mchezo dhidi ya Crystal Palace alikuwa akihushwa na mpango wa kuondoka hapo kwenye dimba la Emirates kipindi cha majira ya baridi kilichopita. Lakini sasa Xhaka ndiye mchezaji aliyecheza dakika nyingi zaidi pale Arsenal tangu Arteta achukue mikoba. Kiwango cha Xhaka mwenye umri wa miaka 27, sasa kimekuwa cha kuvutia na ameonyesha kuimarika zaidi.

Mchezaji mwingine aliyeonekana kuimarika zaidi ni Lucas Torreira, ambaye alionekana kutokuwa na nafasi chini ya Emery na sasa amekuwa nguzo ya Arteta kwenye safu ya kiungo mkabaji.

David Luiz, Ainsley Maitland-Niles na Alexandre Lacazette ni wachezaji wengine wachache ambao wameonekana kuimarika zaidi.

**1. Kuimarika safu ya ulinzi**

Mashabiki wa Arsenal kwa muda mrefu walikuwa wanalia na udhaifu wa safu yao ya ulinzi na Mikel Arteta ndiye anaonekana kama aliyebadili mambo kwa sasa. Ni jambo la kushangaza kuona kwamba, mabeki ambao walionekana kuwa tatizo chini ya Emery sasa wamebadilika na kuwa muhimu mkubwa kwenye kikosi hicho.

Arsenal kwa sasa ina wastani mzuri wa kuruhusu mashuti 3.5 kwenye lango lake chini ya Arteta ukilinganisha na wastani wa tisa chini ya Emery.

Wachezaji kama Shkodran Mustafi na Sokratis Papastathopoulos walionekana kutokuwa kwenye kiwango kizuri chini ya kocha aliyepita, lakini sasa wanaonekana kuwa nyota muhimu zaidi kwa kikosi hicho. David Luiz mwenye umri wa miaka 31, ambaye ndiye beki mwenye uzoefu mkubwa zaidi kwenye kikosi cha Arsenal ameshamsifia Arteta hadharani kwamba mbinu zake zimekuwa bora zaidi.

Mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea amebainisha kwamba, Arsenal chini ya Arteta imekuwa ikicheza kwa mbinu bora zaidi hasa kwenye safu ya ulinzi tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

Na kama Arteta atazidi kuimarisha vizuri zaidi safu ya ulinzi ya Arsenal maana yake kwamba kikosi hicho kitakuwa bora zaidi na kuweza kutoruhusu mabao mengi kama ilivyokuwa hapo awali. Na ishara zinaonyesha wazi kwamba, Arteta katika hilo anaelekea kufanikiwa.

**NDANI YA 18**




WINGA Jack Grealish amehusika moja kwa moja katika mabao 16 kwenye michuano yote aliyoichezea Aston Villa msimu huu (mabao tisa, pasi za mwisho 'assists' saba), zaidi ya mchezaji yeyote wa Kiingereza wa nafasi ya kiungo kwenye Ligi Kuu England.



KUCHOMOZA kwa Manchester City na kuwa timu bora kwenye soka la Uingereza kwa kipindi cha muongo mmoja uliopita kumetambulika. Walikuwa kwenye nafasi ya katikati katika msimamo wa ligi wakati...
**Uk. 16-17**




# WANAMICHEZO 10 WENYE WAFUASI WENGI INSTAGRAM

**LONDON, England**

MITANDAO ya kijamii kwa sasa imekuwa sehemu bora zaidi kwa wanamichezo duniani kupata wafuasi na mashabiki wengi. Ukiachana na facebook na twitter, mtandao wa Istagram unaonekana kupendwa na nyota wengi zaidi duniani.

Makala haya yanakuchambulia wanamichezo 10 wanaongoza kuwa na wafuasi wengi zaidi kwenye mtandao wa Istagram kwa sasa duniani...

**10. Gareth Bale (Wafuasi: 42,935,675)**

Winga huyu wa kimataifa wa Wales amekuwa na wakati mzuri na mbaya pale Real Madrid, akishinda mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini majeruhi yamekuwa tatizo kubwa kwake. Bale kwa sasa yupo kwenye msimu wake wa saba katika klabu hiyo na bado anajaribu kumshawishi Zinedine Zidane kuendelea kucheza hapo, ingawa kwa sasa hana namba kikosi cha kwanza.

**9. Marcelo (Wafuasi: 43,657,119)**

Beki huyo wa kushoto wa Brazil amekuwa na kipaji cha kuvutia na kumfanya kuwa na mashabiki wengi wanaovutiwa naye. Amekuwa pale Real Madrid tangu mwaka 2007, na bado ana uwezo wa kupigania namba yake katika umri wake wa miaka 31.

**8. James Rodriguez (Wafuasi: 44,916,685)**

Rodriguez alipata mashabiki wengi zaidi wakati wa Kombe la Dunia mwaka 2014 nchini Brazil wakati aliposhinda Kiatu cha Dhahabu. Ukafuatia uhamisho wa kwenda Real Madrid, lakini mambo hayakuwa mazuri zaidi kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Colombia. Akapelekwa kwa mkopo kule Bayern Munich, lakini sasa amerudi tena Madrid.

**7. Virat Kohli (Wafuasi: 48,671,763)**

Huyu ni nyota wa mchezo wa Criketi kutoka nchini India na amekuwa na mashabiki wengi zaidi duniani. Akiwa anafuata nyao za gwiji wa mchezo huo, Sachin Tendulkar, Kohli kwa sasa ndio nyota anayetazamwa zaidi kwenye mchezo huo na amekuwa na mashabiki wengi zaidi katika historia ya nchi ya India ambayo mchezo huo ni maarufu zaidi.

**6. Ronaldinho (Wafuasi: 51,011,124)**

Mchezaji fundi wa wakati wote. Ronaldinho alishinda Kombe la Dunia mwaka 2002 akiwa na kikosi cha Brazil, akifunga shuti la 'free-kick' dhidi ya England kwenye mchezo wa robo fainali, kabla ya kwenda kupata umaarufu mkubwa pale Barcelona. Anatambulika kama mchezaji bora zaidi kwa miaka ya 2000, pamoja kwamba kastaafu kucheza soka, lakini bado ana wafuasi wengi zaidi duniani kote.

**5. LeBron James (Wafuasi: 58,029,804)**

Huyu ni mchezaji wa mpira wa kikapu nchini Marekani. Nyota huyu anajulikana kama Mfalme kwenye mchezo huo kwa sasa. James ameshinda mataji ya Ligi Kuu ya Marekani, NBA (mara tatu), ana medali mbili za Olimpiki na mara nne ametajwa kuwa mchezaji mwenye thamani kubwa zaidi duniani (MVP) kwa mchezo huo.

**4. David Beckham (Wafuasi: 60,576,055)**

Alistaafu soka tangu mwaka 2013, lakini bado ana mashabiki wengi duniani kote. David Beckham katika umri wake wa miaka 44, amejiimarisha yeye mwenyewe kama mchezaji bora zaidi wa kupiga krosi wakati akiwa pale Manchester United na Real Madrid, pia akicheza mechi 115 kwa timu ya Taifa ya England, na kumfanya kuwa mchezaji wa tatu nchini humo katika historia aliyeichezea mechi niyngi zaidi timu ya taifa.

**3. Neymar (Wafuasi: 132,646,774)**

Neymar yupo kwenye tatu bora akiwa ameng'ara pale Barcelona na sasa akiwa kule PSG. Ameichezea timu yake ya Taifa ya Brazil jumla ya mechi 101 akifunga mabao 61 akiwa nafasi ya tatu kwa kuwa mfungaji bora wakati wote kwa kikosi hicho nyuma ya Pele na Ronaldo.


**2. Lionel Messi (Wafuasi: 141,937,702)**

Messi ameshika nafasi ya pili kwa kuwa na wafuasi wengi zaidi. Ni mchezaji bora zaidi kwa kizazi hiki. Mshindi mara sita wa Ballon d'Or, ni mambo machache mno ambayo hajashinda kwenye soka na bado haonyeshi dalili za kuchoka hadi sasa.

**1. Cristiano Ronaldo (Wafuasi: 200,347,435)**

Mjadala wa nani bora kati ya Ronaldo na Messi hauwezi kumalizika duniani kwa miaka mingi inayokuja, lakini katika wafuasi wengi kwenye mtandao Ronaldo ndiye kiboko yao. Raia huyo wa Ureno ameng'ara pale England, Hispania na kwa sasa Italia na pia kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Bado bao moja tu kufikisha mabao 100 katika kikosi cha timu ya Taifa ya Ureno na kumfanya kuwa mmoja wa nyota bora zaidi duniani.

**USILOLIJUA**



Kipa wa Liverpool, Mbrazil Alisson ameruhusu bao moja katika kila dakika 214 kwenye Ligi Kuu msimu huu, kama akiendelea na kiwango hiki, anaweza kuvunja rekodi ya mlinda mlango wa zamani wa Chelsea na Arsenal, Petr Cech ambaye aliruhusu bao moja kila baada ya dakika 242 kwenye Ligi Kuu.



Mganga Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Dk. Mariamu Ngwere, akitoa taarifa za ujenzi wa zahanati ya kijiji cha Kyangala wakati wa ziara ya kamati ya siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani humo. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Biashara magendo zapungua mpakani Kasumulu

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

OFISA Mfawidhi Mkuu wa Forodha Kituo cha Mbeya, Robert Nyoni amesema uboreshaji na uimarishaji vituo na mifumo ya forodha unaofanywa na serikali umesaidia kupunguza biashara za magendo.

Amesema pia imesaidia kurahisisha biashara na usafirishaji wa mizigo pamoja na kuongeza makusanyo ndani ya serikali.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe na kubainisha kuwa biashara ya magendo katika mpaka wa Kasumulu unaotenganisha nchi ya Tanzania na Malawi imepungua kwa kiasi kikubwa.

Alisema kwa sasa kuna mifumo bora na imara ya ufuatiliaji wa mizigo inayoingia na kutoka nchini na kwamba vitendo vya udanganyifu kwa baadhi ya wasafirishaji na waingizaji wa mizigo imepungua kwa kiasi kikubwa mkoani mbeya.

"Unajua kuna mifumo ya aina mbalimbali na iliyoboreshwa ya kufuatilia mizigo ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia sana kupunguza vitendo vya magendo ambavyo vimekuwa vikifanywa na watu wasiowaaminifu na wanao lenga kukwepa kulipa mapato ya serikali," alisema Nyoni.

Alisema hali ya makusanyo imekuwa ikipanda kwa kasi katika maeneo ya forodha kwa Mkoa wa Mbeya yaliyopo katika mpaka wa Kasumulu ikilinganishwa na kipindi cha nyuma.

Alisema maofisa wa kituo hicho cha forodha wamekuwa na ushirikiano na vyombo vya dola na wananchi katika kuhakikisha watu wanaokusudia kukwepa kodi wanatiwa nguvuni.

Alisema kutokana na ushirikiano huo wamefanikiwa kukamata watu mbalimbali wanaoingiza na kusafirisha bidhaa kwa kupitia vichochoro vya mipaka.

Alisema baada ya kuanzisha mfumo wa kununua bidhaa zilizokamatwa, kwa sasa kampuni ya udalali zilizokuwa zinahusika kupiga mnada mali zilizokamatwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hayata husika kwa sababu mfumo huo umeonyesha kuwa na manufaa kutokana na wateja kushindana kununua bidhaa kwa njia ya mtandao.

"Hata mkoani Mbeya mfumo huu unakusudiwa kuanza hivi karibuni kwa kuwa ni mfumo wenye manufaa makubwa na ambao unaiingizia serikali fedha nyingi kwa muda mfupi," alisema Nyoni.

Alisema miongoni mwa majukumu ya kituo cha forodha ni kukusanya ushuru wa serikali, kurahisisha mambo ya biashara, kuzuia magendo na kutoa takwimu za bidhaa zilizouzwa nje ya nchi, zilizoingizwa ndani ya nchi na kuuzwa.

# Sido yashushia fursa wajasiriamali wadogo

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

SHIRIKA la kuhudumia viwanda vidogo (SIDO) katika mikoa ya Mbeya na Songwe limesema limejipanga kuhakikisha linawawezesha wajasiriamali katika mikoa hiyo, ili kuongeza thamani ya mazao yao.

Limesema litawahamasiaha wakulima hao kuanzisha viwanda vidogo katika maeneo yao kwa lengo la kuuza bidhaa zitokanazo na mazao.

Meneja wa Sido katika mikoa ya Mbeya na Songwe, Henrick Mdede, aliyasema hayo jana na kusema kuwa uamuzi wa Sido ni kuona wajasiriamali hao kuona viwanda vidogo wanaongeza thamani ya mazao yao.

Alisema mkakati wa SIDO ni kuona wajasiriamali hao kuchangamkia fursa za kibiashara nchini na nchi za Zambia, Malawi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Alisema suala la kuwahamasisha wajasiriamali kuanzisha viwanda vidogo vya kukoboa mchele, kusaga unga na kusindika baadhi ya bidhaa za matunda kutasaidia wazalishaji wa mazao hayo kuweza kuuza kwa tija na kwa wakati kwa kutegemea soko la ndani badala ya soko la nje.

Mdede alisema Sido katika mikoa ya Mbeya na Songwe limeanzisha mfumo wa kongano unaolenga kuviwezesha viwanda vinavyozalisha bidhaa za aina moja kujengwa katika eneo moja.

"Lengo ni kuona mkoa wa Mbeya pekee kuna kongani takribani nne ambazo kuna viwanda vya ukamuaji wa mafuta ya alizeti, viwanda vya kuongeza thamani ya mpunga katika Jiji la Mbeya na wilayani Mbarali," alisema Mdede.

Alisema kutokana na jitihada za SIDO katika kuwahamasisha wananchi kuanzisha viwanda vidogo mpaka sasa kuna viwanda vidogo zaidi ya 29 vya kuongeza thamani ya zao la mpunga, viwanda vidogo vya kuchuja alizeti ambavyo vimeongezeka kutoka 25 hadi kufikia 32.

Alisema Shirika la Sido limekuwa mstari wa mbele katika kutoa mafunzo ya aina mbalimbali kwa ajili ya kuchochea uanzishwaji wa viwanda pamoja na mafunzo ya usindikaji wa vyakula vya aina ya mboga na matunda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi kwa maendeleo ya watu na taifa.

# NIDA yatupiwa lawama wananchi kushindwa kujisajili

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

KAMATI ya ushauri ya watumiaji wa huduma za mawasiliano mkoani Mbeya (TCRA-CCC) imesema wananchi wengi wanaoishi katika maeneo ya vijiji mkoani humo wameshindwa kusajili laini zao za simu kwa sababu hawajafikiwa na huduma ya vitambulisho vya Taifa.

Akizungumza na Nipashe Katibu wa Kamati hiyo, Atupele Dold, alisema kumekuwa na malalamiko ya wananchi wengi wanaoishi maeneo ya vijijini kutofikiwa na huduma hiyo.

Alisema umefika wakati kwa watendaji wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kwenda maeneo ya vijijini kwa lengo la kuwawezesha wananchi waliokosa kupata huduma hiyo kuweza kujisajili na kupata vitambulisho kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Alisema kwa sasa wananchi wengi wamekuwa wakitumia gharama kubwa ya kusafiri umbali mrefu kwa lengo la kufuata vituo vya Nida ambavyo vipo katika makao makuu za wilaya.

Alisema ni wakati sasa kwa serikali kuongeza watumishi Nida na vifaa kwa lengo la kuwawezesha Watanzania ambao hawajajisajili kujisajili.

Aidha, alisema tangu usajili kwa kutumia vitambulisho vya Taifa uanze vitendo vya wananchi kutapeliwa vimepungua kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na hapo awali, ambapo wengi wa wananchi walikuwa wakitoa malalamiko ya kutapeliwa na watu wasiyo na nia njema.

"Hali ya malalamiko ya wananchi kwa mkoa wa Mbeya kutapeliwa fedha na watu wasiowafahamu imepungua kwa kiasi kikubwa baada ya serikali kuwataka wananchi kuwa na vitambulisho vya taifa na kujisajili kwa njia ya simu," alisema Dold.

Alisema uamuzi wa serikali kuwataka wananchi kuwa na vitambulisho vya Taifa kutasaidia kupunguza vitendo vya uhalifu kwenye mitandao ya simu na watu kuwa na laini nyingi za simu.





# Watakiwa kuacha wizi wa dawa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAFAMASIA nchini wametakiwa kuacha tabia ya wizi wa dawa katika maeneo mbalimbali kwa kuwa wanachafua jina na sifa za wafamasia.

Onyo hilo lilitolewa jana na Mfamasia Mkuu wa Serikali, Daudi Msasi, alipokuwa akizungumza kwenye hafla fupi ya kuwasajili wafamasia wapya 108, kutoka katika vyuo mbalimbali.

Alisema upotevu wa dawa katika maeneo ya nchi kumekuwa kunawatia doa wafamasia ambao ndiyo wahusika wakuu katika eneo hilo. "Yaani mimi nikisikia suala la upotevu wa dawa najisikia vibaya sana natamani kujificha kwani tunachafuliwa sana jina letu na watu ambao hawazingatii kiapo chao na maadili ya kazi yao waliyoisomea," alisema.

Aliwataka wafamasia hao kuhakikisha kuwa wanafanya kazi kwa kuzingatia weledi pamoja na misingi ya utumishi wa umma.

"Nawaombeni nyinyi mmesoma na kusoma kwenu mnaweza kufanya chochote hasa katika matumizi ya dawa za kulevya maana mnaweza kuchanganya vitu tu mkawa mmegeuza vitu vikawa na madhara kwa watu wengine," alisema.

Naye Msajili wa Baraza la Famasi nchini, Elizabeth Shekalaghe, alisema kuwa Tanzania inakabiliwa na uhaba mkubwa wa wafamasia, hali ambayo inasababisha wananchi katika baadhi ya maeneo kukosa huduma za wataalamu hao katika kada ya afya.

Shekalaghe, alisema idadi ya wafamasia nchini bado ndogo ukilinganisha na idadi ya watu walipo hivi sasa.

Alisema pamoja na kuwasajili wafamasia hao 108, idadi yao itaongezeka hadi kufikia 1,971 ambao hawakidhi mahitaji ya Watanzania zaidi ya milioni 55, waliopo hivi sasa.

"Ukiangalia katika nchi zilizoendelea au kwa mujibu wa miongozo ya WHO, inaonyesha kuwa kila mfamasia mmoja anatakiwa kuhudumia watu 10,000 kiasi ambacho ni kiwango cha kimataifa," alisema Shekalaghe.

Aidha, alisema kutokana na uhaba huo hivi sasa wanashirikiana na vyuo mbalimbali ili kuongeza idadi ya udahili kwa wanafunzi wanaosoma masuala ya famasi ili kuziba pengo lililopo.

"Kwa kutumia mbinu hiyo ndani ya miaka minne ijayo nafikilia kuwa hali itakua tofauti sana na ilivyo sasa tutakua tumeongeza idadi ya wafamasia katika maeneo mbalimbali ya nchi," alisema.

Akizungumzia suala la nidhamu msajili huyo, alisema mpaka sasa tayari wameshawachukulia hatua wafamasia 32, ambao wamesimamishwa kutoka na makosa mbalimbali.

Vilevile, aliitaka jamii kutoa taarifa baraza la famasi, pale wanapoona kuwa wafamasia wanafanya kinyume na miongozo ya utumishi wa umma.

Mkurugenzi wa Huduma za Afya kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Dk. Ntuli Kapologwe, aliwataka wafamasia hao kuacha tabia ya kuchagua maeneo ya kwenda kufanya kazi.

Alisema pamekuwapo na tabia ya baadhi ya watumishi kukwepa kwenda kufanya kazi katika maeneo ya vijijini ambako pia serikali imewekeza katika vituo mbalimbali vya afya.

"Msichague sehemu ya kwenda kufanya kazi kwani ni lazima mtumie ujuzi wenu kwenda kuungana na serikali kuwasaidia wananchi hawa ambao wanahitaji huduma yenu katika zahanati pamoja na vituo vya afya tulivyo jenga katika awamu hii ya tano," alisema Dk. Kapologwe.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo (katikati), akimkabidhi taarifa ya miaka minne ya mafanikio ya wizara hiyo Mbunge wa Rombo, Joseph Selasini (kulia) kwa niaba ya vyama vya upinzani, baada ya kuwasilisha mwisho wa wiki jijini Dodoma. Kushoto ni Naibu Waziri Wizara hiyo, Mwita Waitara. **PICHA: INRAHIM JOSPEH**

## Spika Ndugai aipa neno mahakama

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema Bunge litaendelea kushirikiana na Mahakama ili kuhakikisha mpango wao wa miaka mitano wa utekelezaji wa majukumu mbalimbali unafanikiwa.

Ndugai alitoa kauli hiyo juzi katika uzinduzi wa Wiki ya Utoaji Elimu ya Sheria iliyoambatana na matembezi maalum, jijini hapa.

Aliipongeza mahakama kwa utendaji mzuri na Bunge litashirikiana na serikali kuhakikisha Mahakama ya Tanzania inapate rasilimali za kutosha ili kutekeleza majukumu yake ya kutoa haki kwa wakati.

Aidha, alitoa wito kwa wakazi wa Dodoma, kufike katika viwanja hivyo ili wajue haki zao na kupata elimu ya sheria kwa kuwa mahakama si sehemu ya kuogopwa.

"Ni muhimu wananchi wakielewa haki zao hawatadanganywa," alisisitiza.

Naye Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, alisema mtumishi wa umma anayeenda kutekeleza sheria kwa operesheni hafai kwa kuwa anapaswa kutoa elimu ndio afanye operesheni.

Alisema sheria inapaswa iwekwe katika mizani sawa ili kufanya kazi ipasavyo.

# Tamisemi yajivunia mafanikio miaka minne ya Magufuli

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imetaja mafanikio sita yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais John Magufuli, huku ikisema tatizo la usafiri kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wanaotumia mabasi ya mwendokasi itamalizika Julai mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni wiki na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tamisemi, Selemani Jafo, alipokuwa akizungumzia mafanikio ya wizara hiyo katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Magufuli.

Alitaja mafanikio hayo kuwa ni ujenzi wa miundombinu ya barabara, hospitali za wilaya na vituo vya afya, mpango wa elimu bure, ukusanyaji mapato, ujenzi wa viwanda vidogo, utoaji mikopo kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu na mradi wa mabasi yaendayo haraka.

Alisema ujenzi wa miundombinu ya barabara unaofanywa na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) umekuwa na mafanikio makubwa na kurahisisha usafiri kwa wananchi.

Alibainisha katika eneo hilo, kumekuwapo na miradi ya kimkakati kwa majiji na manispaa ambapo zaidi ya Sh. bilioni 840 zinatumika kujenga barabara, masoko, stendi za kisasa, mitambo na madampo ya taka.

Akizungumzia sekta ya afya, alisema kabla ya uongozi wa Rais Magufuli kulikuwa na vituo vya afya 115, lakini serikali imejenga vituo 352 ambavyo vina uwezo wa kufanya upasuaji.

"Pia zimejengwa hospitali za wilaya 69 na mwaka huu wa fedha zitajengwa zingine 27 kwa kupitia utaratibu wa 'force account'," alisema.

Kuhusu sekta ya elimu, Jafo alisema kila mwezi serikali inatoa Sh. bilioni 23.86 kugharamia elimu bila malipo.

"Pia tumeboresha shule kongwe ambazo zilikuwa zimechakaa na kwa wastani wa Sh. milioni 800 hadi Sh. bilioni 2 kwa kila shule zinatumika kukarabati, pia miundombinu ya shule za msingi na sekondari imejengwa na inaendelea kujengwa," alisema.

Kadhalika, alisema wameweka sheria kwa ajili ya utoaji mikopo ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ambapo asilimia 10 ya mapato ya ndani yanatumika kwa ajili hiyo na mabilioni ya fedha yametolewa kwa makundi hayo.

Waziri Jafo alisema kwenye ujenzi wa viwanda vidogo, lengo lilikuwa kila mkoa kuwa ni viwanda 100, lakini hadi kufikia Desemba 2018 viwanda 4,877 sawa na asilimia 186.75 vilikuwa vimejengwa.

Akizungumzia ukusanyaji wa mapato, alisema wanajivunia kuanzisha mifumo ya ukusanyaji mapato kwa njia ya kielektroniki ambapo kumeleta mapinduzi makubwa kwenye makusanyo na kuwapo na uadilifu.

Waziri huyo akizungumzia kuhusu mradi wa mwendokasi, Jafo alisema tatizo la usafiri kwa wananchi litamalizika baada ya mzabuni mpya wa kuendesha mradi kupatikana.

"Shida inayojitokeza sasa ni upungufu wa mabasi ambapo yanayofanyakazi ni 140 kati ya mabasi 305 yanayohitajika, mzabuni mpya ataleta mabasi yote 305 yanayohitajika kutoa huduma ya usafiri," alisema.

Alisema ifikapo Julai hadi Agosti mwaka huu, shida hiyo itamalizika baada ya serikali kumpata mzabuni huyo huku akisema awamu ya pili ya ujenzi wa miundombinu ya mradi huo kwenda Mbagala imekwishaanza, na itafuatiwa na awamu ya tatu kwa ajili ya mabasi ya mwendokasi kuelekea Gongo la Mboto.

Kadhalika, alisema kupitia mradi wa uboreshaji miundombinu Jiji la Dar es Salaam (DMDP) barabara za mitaa zinazojengwa zitakuwa kiungo muhimu na zile za mwendokasi.





# RC aahidi kuendeleza tamasha la utalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhamed Mahmoud, amesema kuwa ataendeleza tamasha la utalii wa baiskeli kwa ajili ya kutangaza utalii wa ndani kwa lengo la kukuza pato la taifa.

Akizungumza na washiriki wa tamasha hilo, alisma azima ya serikali ya mkoa huo siyo kuanzisha vivutio vipya vya utalii bali kuhamasisha vijana na watu waliomo ndani ya Zanzibar Tanzania na mataifa mengine kujua utalii uliomo ndani ya mkoa huo.

Alisema serikali imejipanga kuandaa matamasha mengine yatakayoweza kuvitangaza vivutio vya utalii vilivyomo ndani ya mkoa huo hali itakayoleta chachu ya maendeleo.

Aidha, alisema wanatarajia kuanzisha vituo vipya vya utalii kutokana na tamasha hilo litakalofanyika kwa awamu ya pili na kwamba litayahusisha mabaraza ya vijana ya mkoa huo.

Awali, Mkuu wa Wilaya wa Kusini Unguja, Idirisa Kitwana Mustafa, alisema kuwa kupitia tamasha hilo na maeneo yaliyopitiwa na matembezi ya tamasha hilo yatawawezesha vijana kuibua fursa za ajira kwa kuwashirikisha katika kamati za utalii za mkoa huo.

Alisema kuwa tamasha hilo litawafanya vijana kuhamasika juu ya utalii wa ndani ya nchi, na hivyo kusimamia utalii wa ndani kwa kutembeza watalii.

Kwa upande wao washiriki, waliwapongeza waandaaji wa tamasha hilo kutokana na kuwapa fursa vijana ya kuweza kuvifikia vivutio mbalimbali vya utalii.



Baadhi ya wachuuzi wa samaki katika soko la mnada wa samaki Unguja Ukuu Mkoa wa Kusini Unguja, wakisaidiana kupandisha samaki mkubwa aina ya taa katika gari la abiria. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wafanyabiashara watwishwa mzigo uchumi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, amewataka wafanyabiashara kukuza sekta ya viwanda ili kuendeleza ukuaji wa uchumi katika ngazi zote.

Akifungua mkutano wa wafanyabiashara juu ya kujadili hatua na taratibu za uingizwaji bidhaa hivi karibuni, alisema hatua hiyo itapunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje na kwamba baadhi yake umekuwa ulifanyika ujanja wa kibiashara.

Alisema kupitia wafanyabiashara waaminifu waliopo nchini wanaweza kuzalisha bidhaa zikiwamo vibiriti, chumvi na nyinginezo kwa kuzingatia ubora kutokana na malighafi zilizopo na kupelekea Zanzibar nayo kutoa bidhaa kuuza nje badala ya kuuziwa pekee.

Balozi Amina alieleza kuwa serikali inatambua na kuthamini mchango wao ndio maana imekuwa ikiweka mazingira bora kwa wafanya biashara hivyo nao watambue umuhimu wa kufanya biashara kwa ushindani halali kwa kujali ubora wa bidhaa wanazoingiza

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Viwango (ZBS), Dk. Yussuf Nuh Pandu, aliwaomba wafanyabiashara hao kufuatilia na kuzitambua sheria za uingizwaji wa biashara ili kuepuka kupata hasara endapo wataagiza bidhaa zisizokuwa na ubora.

Kwa upande wao wafanyabiashara waliiomba ZBS kuzifanyia kazi bidhaa zinazoingizwa nchini ikiwamo mifuko ya aina ya plastiki inayoingizwa kutoka nchi za Asia ambayo bado inaendelea kuingizwa nchini.

Walisema mifuko hiyo inaathiri soko la mifuko inayozalishwa ndani na pia kuifanya nchi kuwa 'jalala' la kutupia bidhaa hizo.

Mkutano huo ulioandaliwa na ZBS una lengo la kutoa elimu kwa wafanyabiashara hao kuhusiana na kuitumia ZBS katika kuingizwa bidhaa zenye ubora ili kulinda afya za wananchi.

# CCM yaahidi kutoengua yeyote 2020

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi, Balozi Seif Ali Iddi, amesema chama hicho hakitamwengua mgombea yeyote ambaye atapitishwa na wananchi kwenye kura za maoni kwa ajili ya kugombea majimbo ya uchaguzi.

Aliyasema hayo jana katika hafla ya ufunguaji wa tawi la CCM la shehia ya wazee pamoja na ugawaji wa vifaa katika Jimbo la Amani visiwani humo pamoja na kuangalia utekelezaji wa ilani ya CCM.

Alisema CCM inathamini maoni ya wananchi wenyewe hivyo alisema katika vikao vyao hakuna atakayekata jina la mgombea ambaye amechaguliwa na wananchi wenyewe.

"Wananchi msiwe na wasiwasi kama viongozi wenu mmewachagua wenyewe basi sisi tutawarejesha hao hao ili muwapigie kura katika uchaguzi mkuu," alisema Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Aidha, aliwataka wananchi kutokaribisha kiongozi ama kundi la watu kuharibu amani na badala yake wapige vita kwa mtu yoyote aliyekuwa na lengo la kuibomoa amani ya nchi kwa kuwa ikivunjika haitarudi tena.

"Amani ikitoweka lazima tutumie nguvu nyingi kuirejesha na hivyo sisi tuendelee kuidumisha amani na tusiwaachie watu wachache wanaotaka kuivunja amani iliyopo," alisema.

Balozi Iddi aliwataka viongozi wa kisiasa kuheshimu demokrasia iliyopo ili kudumisha amani.

"Ubabe hausaidii kitu katika kuongoza nchi na hakuna serikali inayokubali kuchezewa," alitahadharisha.

Kwa mujibu wa Balozi Iddi, jimbo hilo la limetekeleza ilani kwa vitendo, na kuwataka wananchi kuendelea kufanya kazi ya kuendelea kuidumisha amani.

Aidha, alisema CCM itaendelea kujenga matawi yake yenye kuendana na hadhi ya chama hicho.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Amani Kichama, Talib Ali Talib, alisema, viongozi wa Jimbo la Amani wametekeleza ilani kwa vitendo na wameweza kuwapelekea wananchi maendeleo kwa vitendo.

# Biteko: Wawekezaji changieni maendeleo

**Na Romana Mallya,**
MOROGORO

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, amewataka wawekezaji sekta ya madini wanapofanya uwekezaji wao nchini wahakikishe wachangia shughuli za maendeleo kwa sababu mali wanayochimba ni ya Watanzania.

Biteko aliyasema hayo juzi wakati akipokea majengo matatu kwa ajili ya Serikali ya Kijiji ya Nahenge, Mdindo na Kisewe yaliyojengwa Wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro na Kampuni ya Madini ya Mahenge Resources kwa thamani ya Sh. milioni 51.

Kampuni hiyo inajishughulisha na uchimbaji wa madini ya kinywe (Graphite) ambayo hutumika kutengeneza vitu mbalimbali zikiwamo betri, breki na kinga za mashine na Aprili 24, mwaka 2018 sampuli zake tani 500 zilisafirishwa na Mahenge kwenda Canada kufanyiwa majaribio.

Biteko alisema kampuni ya Mahenge licha ya kwamba haijaanza uchimbaji wa madini hayo, lakini imeweza kushiriki katika shughuli za maendeleo ya wananchi na kuamua kujenga majengo matatu kwa ajili ya ofisi za serikali za vijiji hivyo.

Waziri Biteko alisema Rais John Magufuli anataka madini yawanufaishe Watanzania wenyewe na siyo vinginevyo. "Niwatoe wasiwasi wananchi wa hapa kuwa, hakuna mtu hata mmoja atakayekuja Tanzania kuchimba madini aondoke na kuwaacha wananchi wanashangaa, zama hizo zilipendwa.

"Wawekezaji wote watakaokuja watachimba na madini watakayoyapata faida yake lazima irudi Tanzania."

Waziri Biteko alisema soko la madini ambalo limeanzishwa Aprili mwaka jana Ulanga limewezesha kuleta faida kwa serikali ambapo hadi sasa fedha iliyopatikana ya madini yaliyouzwa ni Sh. milioni 396 wakati kwa miaka mitano iliyopita walipata Sh. milioni nne tu.

Aidha, ameiomba Mahenge yale waliyoahidi siku hiyo wayafanyie kazi kwa haraka kwa sababu kampuni nyingi zimekuwa zikiahidi vizuri, lakini baadaye hutokea malalamiko.

"Tayari nimemwelekeza Mkuu wa Wilaya wa hapa wawe na wawakilishi wa kijiji kwenye timu hiyo ili baadaye kusitokee malalamiko."

Waziri Biteko alisema kampuni hiyo imeshapewa sampuli mbalimbali za madini hayo ambazo walizipeleka katika maabara tofauti na wamejiridhisha, Kinywe ya Tanzania ni bora kuliko zinazopatikana maeneo mengine duniani.

Mwenyekiti wa Mahenge, John De Vries ambaye pia ni Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Black Rock Mining kutoka Australia, alisema wajibu wao ni kurejesha manufaa kwa jamii.

Alisema hadi sasa wamewaombа wanahisa wao na tayari wameshapata Dola za Marekani milioni 23 kwa ajili ya uwekezaji huo na kwamba wanahitaji kuwa na fedha nyingi zaidi kwa ajili ya fidia.

"Tupo katika hatua muhimu ya mchakato wa kujenga mgodi, tunawasiliana na benki zenye mitaji mikubwa ili tufanikishe hili na tuweze kukabidhi serikalini asilimia 16 kama mkataba wa madini unavyosema," alisema.

Vries alisema kampuni hiyo imechukua tahadhari kubwa ili wasiahidi kitu ambacho baadaye washindwe kukitekeleza.

Mkuu wa Wilaya ya Ulanga, Ngolo Malenya, alisema kampuni hiyo imekuwa ikishirikiana nao katika shughuli mbalimbali za kijamii.

"Mwaka jana tulikuwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 38, tulifanya harambee na kampuni hii ya Mahenge ilichangia Sh. milioni 15, katika shughuli za Mwenge wa Uhuru walitoa sare za watoto wa alaiki zenye thamani ya Sh. Milioni 10 na leo wanatukabidhi ofisi za vijiji vitatu vinavyogusa maeneo yao ya uwekezaji," alisema.

Mbunge wa Jimbo la Ulanga, Goodluck Mlinga, alisema kampuni hiyo imetoa mchango mkubwa katika maeneo hayo na imekuwa ikishirikisha jamii.

Kampuni ya Mahenge Resources itakapoanza uchimbaji inatarajia kuzalisha tani 80,000 kwa mwaka na uzalishaji huo baadae utafikia mpaka tani 250,000 kwa mwaka na utachangia Dola za Marekani milioni 100 (sawa na Sh. bilioni 226).



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, akikabidhi tuzo kwa Mkurugenzi wa kituo cha mafuta Puma Arusha Centre, Husein Sajan, baada ya kuibuka mshindi wa kwanza katika tuzo za waendesha vituo vya mafuta vya Kampuni ya Puma Energy Tanzania Ltd, wakati wa utoaji tuzo hizo Dar es Salaam. Kutoka ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Dominic Dhanah na Mwenyekiti wa Bodi Selemani Majige. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachimbaji madini wasio na vyoo wapewa siku 15

**Na Mohab Dominick,**
KAHAMA

OFISA Madini Mkazi wa Mkoa wa Shinyanga, Joseph Kumburu, ametoa siku 15 kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu katika Kata ya Segese Halmashauri ya Msalala kukamilisha ujenzi wa vyoo ili kuepusha uchafuzi wa mazingira na kutishia kuyafunga iwapo watashindwa kutekeleza agizo lake. Kumburu amesema maeneo mengi ya uchimbaji wa madini ya dhahabu katika kata hiyo yamegundulika kukosa vyoo, hivyo kuwa tishio kwa afya za wachimbaji wenyewe pamoja na wananchi wanaozunguka machimbo hayo, hali ambayo inaweza kusababisha magonjwa ya milipuko kwa kuzingatia kuwa na sasa ni msimu wa mvua za masika.

Aliwaomba maofisa afya kutekeleza majukumu yao kwa kusimamia ujenzi huo pamoja na elimu kwa wachimbaji itolewe juu ya madhara yatokanayo na kukosekana kwa vyoo vya kutosha katika maeneo ya uchimbaji.

Kumburu aliyasema hayo katika kikao kazi chenye lengo la kutatua migogoro baina ya wachimbaji kwa wachimbaji kutokana na kuingiliana kwa mipaka na ukwepaji kodi ya serikali. Alisema baada ya siku 15 atatembelea maeneo yote ya uchimbaji ili kujiridhisha kama agizo lake limetekelezwa na kuahidi kuwa iwapo suala hilo halikutekelezwa hatashindwa kuungana na timu ya wataalamu kuyafunga maeneo yote ya uchimbaji.

# Kongamano kujadili elimu ya sekondari

**Na Sabato Kasika**

MKOA wa Mara umeandaa kongamano maalumu la kuboresha kiwango cha elimu kwa shule za sekondari na kuchangia ujenzi wa madarasa, ambalo litashirikisha wadau mbalimbali wa elimu wa ndani na nje ya mkoa huo.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu jana, Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mara, Emmanuel Kisongo, alisema kongomano hilo litafanyika Februari 23 mwaka huu, na kwamba maandilizi yake bado yanaendelea.

"Tumeamua kuandaa kongamano hilo, ili kupata maoni ya wadau mbalimbali wa elimu kwa ajili ya kuboresha elimu mkoani kwetu na kuhakikisha changamoto zinazozikumbwa shule zinapungua," alisema Kisongo.

Kisongo aliwataja baadhi ya wadau wa elimu watakaoshiriki kongamano hilo kuwa ni maofisa elimu sekondari na msingi, wakuu wa wilaya, wabunge wote wa majimbo ya mkoa huo.

"Mkoa wetu kwa sasa una shule 204 za sekondari na 847 za msingi...tutakutana kujadili changamoto za shule hizo ikiwamo ya uhaba wa madarasa ambao unazikabili ili kuhakikisha unaisha na kubaki historia," alisema.

Alisema, ujenzi wa madarasa umekuwa ukikabiliwa na changamoto, kutokana na baadhi ya wazazi kukataa kushiriki wakidai kwamba serikali ilishaamua kutoa elimu bure, hivyo hakuna haja ya wao kuchangia ujenzi huo.

Ofisa elimu huyo wa mkoa alisema, hilo ni tatizo ni miongoni mwa matatizo, ambayo wanataka wayamalize haraka iwezekanavyo, ili wanafunzi wasiendelee kusomea chini ya miti au kubanana katika madarasa.

"Hivyo niwaombe wadau wajiandae kushiriki katika kongamano hilo ili tuchangie kwani tunataka ushirikiano wa wananchi na serikali uendelee kuzaa matunda, kwa ajili ya watoto wetu," alisema.

Kisongo alisema, wadau watakaoshiriki watadadisi na kupata uzoefu kutoka kwa wingine jinsi walivyofanikiwa kuboresha elimu kwenye maeneo yao na hatimaye watatoka wakiwa na kitu walichojifunza.

HABARI KIMATAIFA

# Idadi waliofariki na corona yafikia 300

**BEIJING, China**

IDADI ya vifo vitokanavyo na homa inayosababishwa na virusi vya corona imeongezeka na kufikia 300 huku zaidi ya 14,380 wakiambukizwa.

Kutokana na hali hiyo, Shirika la Afya Duniani (WHO) limetoa tahadhari kwa nchi mbalimbali duniani kuandaa mikakati kabambe ya kukabiliana na ugonjwa huo iwapo utaenea

na kuwaambukiza wakazi wake kwa kuzingatia kwamba mataifa zaidi yanaendelea kuripoti matukio ya maambukizo.

Nchi za Ujerumani, Australia, Japan, Korea Kusini, Falme za Kiarabu, Marekani na Vietnam zote zimeripoti maambukizi mapya ya ugonjwa huo huku Hispania ikithibitisha maambukizi ya kwanza katika nchi hiyo.

Nchi ya Ufilipino imetangaza kifo cha kwanza kutokana na homa inayosababishwa na virusi vya ugonjwa huo.

Wakati huo huo, maofisa sita wamefukuzwa kazi katika mji wa Huanggang uliojirani na Mji wa Wuhan ambako ndiko virusi hivyo vilipoanzia.

Kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Habari la China, Xinhua, maofisa hao wamefukuzwa kazi kutokana na utendaji kazi mbaya katika kushughulikia mlipuko wa virusi vya corona tangu vilipozuka.

Licha ya kuonyesha dalili za kupungua maambukizo mapya, mamlaka ya mkoa wa Hubei imerefusha muda wa likizo ya mwaka mpya wa Lunar iliyotarajiwa kumalizika mwisho wa wiki hii hadi katika mwezi huu wa Februari.

Msongamano wa idadi kubwa ya watu wanaosafiri wakati kama huu ambao wanarejea kutoka sehemu mbalimbali unaleta hofu ya uwezekano wa kusababisha maambukizo mapya.

Mamlaka za miji katika mkoa wa Hubei zinawahimiza watu wote waepukane na mikusanyiko.

Shule zote katika mkoa huo zimeahirisha kufunguliwa kwa muhula mpya hadi taarifa rasmi itakapotolewa.

Pamoja na kuweka vikwazo vikali vya usafiri nyumbani, China

imekasirishwa na vikwazo vilivyowekwa na serikali za nje na imekosoa agizo la Marekani la kuwazuia kuingia nchini humo watu wasio raia wa Marekani ambao waliitembelea China katika kipindi cha wiki mbili zilizopita.

China imesema mbali na kuiteremshia sifa ya kimataifa, hatua kama hiyo inaweza kuathiri zaidi uchumi wake wa ndani ambao kwa miongo kadhaa unakua kwa kiwango cha chini, huku vita vya kibiashara kati yake na Marekani vikiwa bado kwa kiasi kikubwa havijapata suluhisho.

Mashirika ya ndege ya Canada, Lufthansa, Uingereza, Uturuki, Marekani, KLM, Air France, Qantas na Delta yamesitisha safari zake za ndege kwenda na kutoka China.

Hatua hiyo inaiweka China katika hali ya kutengwa kutokana na

kuongezeka kutokuwapo na shughuli za usafiri za kimataifa pamoja na kusimamishwa kwa safari za ndege.

Ujerumani, Uturuki na Marekani ni kati ya nchi ambazo zilipeleka ndege kuwaondoa raia wao kutoka mji wa Wuhan.

Nchi nyingine ambayo inajiandaa kuondoa raia wake ni India na kwamba raia wapato 250 kutoka mji wa Wuhan.

Nayo Urusi ilitangaza kufunga mpaka wake na China hatua sawa iliyochukuliwa na nchi zingine majirani wa China.

**DW**




Maofisa afya nchini China wakipuliza dawa katika baadhi ya majengo kwa ajili ya kupamba na virusi vya corona. **PICHA: Chinatopix**

# Waandamanaji wagoma kuondoka barabarani

**BAGHDAD, Iraq**

VIJANA waliokuwa na ghadhabu wanaoipinga serikali nchini Iraq,

wameendelea kubakia katika maeneo wanayofanyia maandamano kusini mwa nchi hiyo licha ya kuteuliwa kwa waziri mkuu mpya, Mojammed Allawi.

Ni muda wa miezi minne sasa imepita tangu kujiuzulu kwa Waziri Mkuu, Adel Avdel Mahdi na kuzuka kwa vurugu nchini Iraq chanzo kikuwa ni kuipinga serikali iliyoko madarakani.

Waandamanaji hao walikuwa wanataka kuteuliwa kwa mrithi huru wa kisiasa ambaye hajawahi kuhudumu serikalini na kwa majibu wa maelezo ya waandamanaji hao, aliyekuwa waziri wa mawasiliano Allawi hakufikia matakwa hayo.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa vijana wadogo waliokuwa wamefunika nyuso zao kwa vitambaa, walichoma magurudumu ya magari usiku kwa ghadhabu inayotokana na kuteuliwa kwa Allawi.

**VOA**

## Mwakilishi EU atua Iran kupatanisha

**TEHRAN, Iran**

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Umoja wa Ulaya (EU) Josep Borell, anasafiri kuelekea Iran kukutana na viongozi wa nchi hiyo.

Ziara hiyo inaonekana kuwa hatua ya EU kuokoa mkataba wa nyuklia kati ya Iran na mataifa yenye ushawishi mkubwa duniani.

Hali ya wasiwasi kati ya Iran na Marekani imeongezeka

tangu Rais wa Marekani, Donald Trump alipojiondoa katika mkataba wa nyuklia na kurejesha tena vikwazo dhidi ya Iran mnamo mwaka 2018.

Hata hivyo, Iran imejibu kwa kujiondoa polepole katika uwajibikaji wake katika mkataba huo.

Taarifa kutoka Kituo cha Habari cha IRNA imeeleza kuwa Borrell

atakutana na Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Mohammad Javad Zarif na maofisa wengine wakuu wa Iran leo.

**DW**

## Corona yaua mmoja Ufilipino

**MANILA, Ufilipino**

NCHI ya Ufilipino imeripoti kifo cha kwanza kutokana na virusi vipya vya corona.

Idara ya Afya nchini Ufilipino, imesema kuwa mwanamume mmoja raia wa China mwenye miaka 44 kutoka mji wa Wuhan, alilazwa Januari 25 baada ya kupata joto kali na kukohoa.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa baadaye baada ya kuchukuliwa vipimo aligundulika kuwa na homa ya mapafu na baada ya matibabu hali yake ikaimarika.

Hata hivyo saa 24 kabla ya kifo chake, hali yake iligeuka kuwa mbaya zaidi na kufariki baada ya kugunduliwa kuwa na virusi hivyo vya corona.

Mpenzi wake naye amethibitishwa kuwa na virusi hivyo na ametengwa ili kupata matibabu katika hospitali moja mjini Manilla.

**DW**

**Hata hivyo saa 24 kabla ya kifo chake, hali yake iligeuka kuwa mbaya zaidi na kufariki baada ya kugunduliwa kuwa na virusi hivyo vya corona.**

# Serikali: Hii ndiyo hali ya mafuta nchini

**Na Mwandishi Wetu**

UWEZO wa nchi kuhifadhi mafuta umeongezeka kutoka lita milioni 900 mwaka 2015 hadi lita bilioni 1.3 kwa sasa, imeelezwa.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam juzi wakati wa hafla ya kutunuku tuzo na zawadi kwa waendesha vituo vya mafuta vya Kampuni ya Puma Energy Tanzania.

Dk. Kalemani alibainisha kuwa kwa sasa Tanzania ina akiba ya mafuta ya petroli lita milioni 97 ambayo yanatosha kuendesha nchi kwa siku 38 kuanzia juzi, dizeli lita milioni 197 zinazotosha siku 28 na mafuta ya ndege lita milioni 30 yanayotosha siku 56.

"Pia tuna akiba ya lita 600,000 za mafuta ya taa, hii ni kutokana na kupungua kwa uhitaji wa nishati hii maana Watanzania wengi sasa, hasa maeneo ya vijijini wameunganishwa na gridi ya taifa ya umeme," alitamba.

Alisema mafanikio hayo yametokana na uboreshaji wa huduma za uagizaji wa mafuta uliofanywa na serikali tangu mwaka 2012, akibainisha kuwa tangu serikali ya awamu ya tani iingie madarakani, nchi haijakumbwa na tatizo katika upatikanaji wa nishati hiyo.

Dk. Kalemani ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, aliutaka uongozi wa kampuni hiyo kupanua wigo wa biashara na kuyafikia maeneo yote ya nchi, hasa vijijini ambako hakuna vituo vya mafuta, hivyo wananchi wanalazimika kuhifadhi mafuta kwenye madumu na kuyauza kwa rejereja kwenye makopo ya maji.

Aliitaka kampuni hiyo ijenge vituo vya kuuzia mafuta katika maeneo ya mikoa ya Katavi, Mara na Geita ambayo haijayafikia.

Waziri huyo pia aliwataka waongeze mapato ya kampuni ili kodi iongezeke na wahakikishe mwaka huu wanatoa gawio la Sh. bilioni 13 kwa serikali, ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni mbili kulinganishwa na gawio lao la mwaka jana.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Puma Energy, Dominic Dhanah, alisema ni mara ya kwanza tuzo hizo zinatolewa nchini kwa lengo la kutambua mchango na kutoa zawadi kwa waendesha vituo bora zaidi vya mafuta vya kampuni hiyo.

Dhanah alisema Kampuni ya Puma inaunga mkono juhudi za serikali katika kutoa ajira kwa wananchi na ndiyo maana inawapa fursa Watanzania kuendesha vituo vyake na wao kuajiri Watanzania wengine kama wauza mafuta, waendesha maduka na walinzi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Puma Energy, Dk. Selemani Majige, alimhakikisha waziri huyo kuwa watayafanyia kazi maelekezo aliyowapa ili kampuni hiyo iendelee kufanya vizuri zaidi katika kuchangia mapato ya serikali kwa kodi na gawio.

Tuzo zilizotolewa ni pamoja na msimamizi bora wa kituo, mwendesha kituo bora katika huduma za magari, mwendesha kituo bora wa mwaka katika ubunifu na kituo chenye huduma bora kwa wateja kwa huduma tofauti na uuzaji wa mafuta.

Zingine ni mwendesha kituo bora wa mwaka, mhudumu bora katika vituo vya mafuta, mwendesha kituo bora wa mwaka katika huduma za malipo ya kidijitali na mwendesha kituo bora wa mwaka katika uhusiano bora na jamii inayomzunguka.

Puma Energy Tanzania ni kampuni ya mafuta iliyosajiliwa nchini na inamilikiwa kwa pamoja na serikali kupitia Msajili wa Hazina na Puma Investments Limited, kila upande ukiwa unamiliki hisa kwa asilimia 50.



Mkurugenzi wa Bidhaa za Kijamii wa T-MARC Tanzania, Flavian Ngole, (kushoto), akikabidhi taulo za kike kwa mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Mugabe wilayani Kinondoni, Judith Michael, wakati wa hafla ya kukabidhi msaada wa taulo za kike zilizozinduliwa na taasisi hiyo nchini, zinazojulikana Flowless, kwa wanafunzi wa shule hiyo mwishoni mwa wiki. Wa pili kushoto ni balozi wa bidhaa hiyo, Dinnah Marrios. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ofisi ya Waziri Mkuu yakidhi viwango Osha

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA) imetoa cheti kwa Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu baada ya kufanyia ukaguzi katika maeneo yote ya ofisi hiyo na kuonyesha kuwa yamekidhi viwango.

Cheti hicho kimetolewa jana jioni (Jumamosi, Februari 1, 2020) na Kaimu Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda na kupokelewa na Katibu wa Waziri Mkuu, Raymond Gowelle.

Akikabidhi cheti hicho, Khadija alipongeza ofisi hiyo kwa kuonyesha mfano wa utekelezaji wa sheria, ambapo amezishauri ofisi nyingine za umma ziige.

"Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu imeonesha mfano wa kuigwa kwa utekelezaji wa sheria, kwani walituita tukaja kufanya ukaguzi na tukatoa maelekezo ya namna ya kuboresha baadhi ya maeneo na wamerekebisha."

Alisema baada ya kutekeleza maelekezo hayo suala lililokuwa limebakia ni upimaji wa afya kwa wafanyakazi pamoja na kutoa mafunzo ya huduma ya kwanza ambayo yalifanyika jana.

Mtendaji huo alisema ni muhimu kwa ofisi zote kuzingatia Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi kwa kuwa hakuna aliye juu ya sheria.

Baada ya kukamilisha zoezi la upimaji wa afya na mafunzo ya OSHA, pia watumishi wa Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu walikumbushwa namna bora ya kufanyakazi kwa uadilifu. Mafunzo yalitolewa na wataalamu kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Watumishi hao waliushukuru uongozi wa ofisi kwa kuandaa utaratibu wa upimaji wa afya ambao ulikuwa na muitikio mkubwa, mafunzo ya huduma ya kwanza pamoja na kukumbushwa kuhusu uadilifu na matumizi ya madaraka na ofisi kwa manufaa ya umma.

# Ufaransa yaendesha mdahalo utunzaji wa Ziwa Victoria

**Na Faustine Feliciane**

UBALOZI wa Ufaransa hapa nchini umeendesha mdahalo juu ya namna bora ya kutunza Ziwa Victoria kwa ajili ya kizazi kijacho.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mdahalo huo uliofanyika Alliance de France jijini Dar es Salaam, Balozi wa Ufaransa nchini, Fredric Clavieter, alisema Ufaransa inathamini urithi wa kizazi kijacho cha Watanzania hivyo kuna umuhimu wa kupunguza matumizi ya kemikali viwandani na kwenye kilimo ambazo zinaingia kwenye ziwa na kuathiri ziwa hilo.

"Ufaransa tutaendelea kushirikiana na Tanzania kuhakikisha usalama wa Ziwa Victoria, lakini tutaendelea kuangalia namna bora ya kutunza ziwa hili kubwa Afrika," alisema Balozi.

Aidha, alisema Ufaransa kupitia shirika lake la misaada, limewekeza kiasi cha dola milioni moja kwa ajili ya kilimo cha asili kisichotumia kemikali.

Mkurugenzi wa taasisi ya utafiti wa uvuvi (TAFIR), Ishmael Kimirei, alisema njia pekee za kutunza Ziwa Victoria ni kuhakikisha zinaondolewa kemikali za viwandani zinaingia ziwani, lakini kuepuka kilimo cha kutumia kemikali pembezoni mwa ziwa.

"Ziwa letu linaathiriwa na matumizi yetu wanadamu, lakini mabadiliko ya tabia ya nchi, kwa upande wa shughuli za binadamu ni pamoja na matumizi ya kemikali kwenye kilimo katika maeneo ya karibu na ziwa, hii inapelekea samaki kuathirika, lakini udongo unaotoka shambani na kuingia ziwani unapelekea kupunguza kina cha maji… sasa njia ya kutunza ziwa letu ni kuhakikisha tunaondoa haya yote," alisema Kimirei.

Aidha, alisema juhudi zinazoendelea kufanywa katika uhifadhi wa Ziwa Victoria umesaidia kuongeza mazalio ya samaki kwa kiasi kikubwa.

"Ripoti inaandaliwa juu ya hili, lakini kwa sasa samaki wameongezeka hii inatokana na juhudi zinazofanywa kuzuia uvuvi haramu pamoja na utunzaji wa ziwa," aliongezea Kimirei.

Baadhi ya washiriki walitaka elimu itolewe kwa wakazi wanaozunguka Ziwa Victoria juu ya uhifadhi wa ziwa hilo.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

**ANAHITAJIKA MUUGUZI**

Anahitajika muuguzi msaidizi au Nurse Assistant kwa anayehitaji

**Apige: SImu Namba:**

**0786 641903 au 0716 172929**

***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TANGAZO**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Moshi Mjini**
**USIMAMIZI WA MIRATHI NO 3 2020**
**Ombi la ALBERT JUSTIN MINJA**
**Usimamizi wa miradhi ya marehemu**
**JUSTIN STEPHEN**

**……LUCIA MINJA………**

Kwa: Yeyote anaehusika

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhuthuria kesi wakitaka mnao tarehe 13/02/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 27-10-20120 mwaka 2019

115612502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84)**
**Wilaya ya Moshi**
**Mahakama ya Mwanzo Moshi Mjini**
**Wilaya ya Moshi**
**MADAI NAMBARI 7 YA 2020**
**Mdai Rajesh Kumar Shivji Aggarwal**
**Mdaiwa Stella Ebenezar Mwacha**
**Kwa Stella Ebenezar Mwacha**

……………………………………………………

Kwa kuwa Mdai /Wadaiwa ameleta /wameleta madai yake/ yao kwamba/Eleza hapa habari ya Madai): FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA KWENYE SHAURI LAMADAI NO,7/2020

Kwa hiyo " Unahitajiwa /Mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku Jumatano Tarehe 19/02/20saa 3:30 Asubuhi/alasiri kwa kujibu Madai hayo na. kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo

Angalia kama hukuhudhuria /hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha kama umepokea /Mmepokea kutwa shauirini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 29/07/2019

115612402

**JAMHURI YAMUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)YA 5 KANUNI YA 2**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA DODOMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI NA. 97 OF 2019**

**TANGAZO**

**Ombi la: UREMBO JOHN FUNGA**

Kuteuliwa msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **JOHN FURAHISHA FUNGA**

Watu wote wanaodai kuwana uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo na wana nia ya kupinga au kuthibitisha uteuzi wa mwombaji wanaalikwa kufika Mahakamani na kuhudhuria kesi, mnamo tarehe 27/02/2020 ili kuwasilisha mapingamizi yao au la kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

IMETOLEWA TAREHE 31/01/2020.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
DODOMA

156132O2

***Kwa Habari Motomoto***

***usikose***

***Gazeti lako la Nipashe***

***kila siku Tupigie***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# UNITED YAMSAJILI IGHALO WA NIGERIA

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imemsajili aliyekuwa mshambuliaji wa Watford, Odion Ighalo kutoka Shanghai Shenhua kwa mkopo hadi mwisho wa msimu huu.

Makubaliano ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria, Ighalo mwenye umri wa miaka 30, hayana kipengele kinachowaruhusu miamba hiyo ya Old Trafford kumnunua.

Ighalo, ambaye bado yuko China anatarajiwa kusafiri kwenda Uingereza ndani ya siku chache zijazo, alifunga mabao 39 katika mechi 99 alizocheza Watford kati ya mwaka 2014 na 2017.

"Odion ni mchezaji mwenye uzoefu mkubwa," alisema kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer.

"Ataingia na kuongeza idadi ya washambuliaji tulionao katika kipindi kifupi atakachokuwa nasi."

"Mchezaji mahiri sana katika kazi yake, atakuwa na manufaa makubwa hapa." alisema Solskjaer.

Ighalo alijiunga na Super League ya China mwaka 2017, kwanza akiwa na timu ya Changchun Yatai.

Baada ya misimu miwili, akajiunga na timu ya Shanghai Shenhua na kufunga mara 10 katika mechi 19 ambazo alishiriki.

Aidha, Odion Ighalo alikuwa mfungaji bora katika mashindano ya Kombe la Afrika kwa kufunga mabao saba kabla ya kufunga matano katika mashindao ya msimu wa joto.

Inafahamika kwamba klabu za ligi nyingine za Ligi Kuu England zimeonyesha nia ya kumsajili Ighalo lakini mwenye alitaka kuichezea United.

Ighalo ni mchezaji wa kwanza kusajiliwa kwa mkopo wa aina hiyo tangu kuwasili kwa Radamel Falcao kutoka Monaco mwaka 2014.

# GUARDIOLA HANA HOFU KIWANGO CHA STERLING



**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola hana hofu na kiwango cha Raheem Sterling licha ya mshambuliaji huyo kuanza mwaka 2020 kwa kiwango kisichoridhisha.

Sterling hajafunga bao katika mechi saba mwaka huu, ambapo kwa mara ya mwisho alifunga dhidi ya Wolves Desemba 27, mwaka jana.

Mshambuliaji huyo amefunga mabao 20 kwenye mashindano yote msimu huu na Guardiola amesema haoni tatizo lolote kwa kiwango cha Sterling kuelekea mchezo wake wa jana Jumapili dhidi ya Tottenham.

"Raheem alikaba vizuri dhidi ya (Aaron) Wan-Bissaka kwenye mchezo wa mwisho na alitengeneza nafasi ambazo mchezaji mwingine hakuweza kuzitengeneza na bahati mbaya hakufunga," alisema.

"Lakini alikuwa pale na nina furaha kubwa juu yake na kiwango alichoonyesha dhidi ya United.

"Mwezi uliopita, watu walizungumza kuhusu takwimu zake, mabao, lakini mara zote nimesema simuhukumu Raheem katika pointi hizo."

Sterling tayari amecheza mechi 34 kwa City msimu huu, akiwa amecheza michezo 51 kwa klabu hiyo kwa msimu wa 2018-19.

# Zidane achambua dabi na Atletico

**MADRID, Hispania**

ZINEDINE Zidane amekubali kwamba yeye alihusika kwa namna moja wakati Real Madrid ikionyesha kiwango kibovu katika kipindi cha kwanza kwenye mchezo dhidi ya Atletico Madrid.

Bao la Karim Benzema katika kipindi cha pili liliwawezesha 'Los Blancos' hao kupata ushindi wa 1-0 katika dimba la Santiago Bernabeu, na kuongoza msimamo wa ligi kwa pointi sita dhidi ya Barcelona waliopo nafasi ya pili.

Hata hivyo, Madrid hawakuwa kwenye kiwango kizuri kwa kipindi cha kwanza na Zidane akafanya mabadiliko ya wachezaji wawili, akimwingiza Vinicius Jr ambaye ndiye alikuwa mpishi wa bao la Benzema.

"Sikufurahishwa na kile nilichokiona uwanjani wakati wa kipindi cha kwanza. Lakini halikuwa tatizo kwa wachezaji, lilikuwa ni jukumu langu," alisema Zidane akiwaambia waandishi wa habari.

"Hivyo, nikawabadili Isco na Toni (Kroos), lakini ingewezekana kwa wachezaji wengine wawili. Mabadiliko yalihitajika.

"Wachezaji watano kwenye kiungo walifanya vizuri katika mchezo mwingine. Lakini leo (juzi) mambo yalikuwa tofauti kabisa, ilikuwa ngumu kwa upande wetu kupata mpira.



# CONTE

## AFUNGUKA ERIKSEN KUTUA INTER

**MILAN, Italia**

UAMUZI wa Christian Eriksen kuchagua kujiunga na Inter Milan dhidi ya klabu nyingine za Ulaya ni uthibitisho kwamba klabu hiyo ipo vizuri zaidi kwa mujibu wa kocha, Antonio Conte.

Eriksen alikamilisha usajili kutoka Tottenham na kujiunga na Inter Jumanne iliyopita, na kuwa mchezaji wa tatu kutua timu hiyo ya Serie A kwenye dirisha la Januari, baada ya Ashley Young na Victor Moses.

Aliingizwa akitokea benchi wakati zikiwa zimesalia dakika 24 mpira kumalizika katika mchezo wa robo fainali ya Kombe la Coppa Italia na jana Jumapili alitarajiwa kucheza dhidi ya Udinese kwenye mchezo wa Ligi Kuu.

Conte amesema Eriksen alikuwa akiwaniwa na klabu kadhaa na anaamini uamuzi wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark kuhamia pale San Siro ni ushahidi tosha kwamba, Inter ni moja ya klabu zinazovutia Ulaya.

"Eriksen aliwaniwa na klabu nyingi na alikuwa na machaguo mengi na akaamua kuichagua Inter," alisema Conte akiwaambia waandishi wa habari.

"Na hilo linathibitisha kwamba, ameona njia sahihi na wote tunafanya kazi vizuri kwa kuiweka timu yetu kwenye daraja la juu."

## NEVILLE AMFANANISHA FERNANDES NA VERON

**MANCHESTER, England**

GARY Neville anaona ishara za Juan Sebastian Veron kwa Bruno Fernandes baada ya kucheza mchezo wake wa kwanza kwa Manchester United.

Fernandes alicheza kwa dakika zote 90 pale Old Trafford Jumamosi wakati United ilipotoka sare ya bila kufungana na Wolves kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno, aliyesajiliwa kwa thamani inayodhaniwa kuwa ni pauni milioni 67 kutoka Sporting CP, alipiga mashuti matano, huku matatu yakilenga goli na alipiga pasi 88, ingawa hakutengeneza nafasi ya kufunga.

Neville aliona inatosha Fernandes kumchukulia kwa mtazamo chanya na kwamba alionekana akiwa katika kiwango cha kuvutia kwenye namba 10 kama ambavyo Veron alivyocheza.

"Ni mapema sana, lakini nilipenda kile alichokifanya," alisema beki huyo wa zamani wa United, Neville akimzungumzia Fernandes akiambia Sky Sports.

"Nafikiri alifanya vizuri, ingawa ulikuwa mchezo mgumu kwake.

"Tumesikia mengi kuhusu uwezo wake wa kutoa pasi za mwisho na kufunga mabao, naamini atakuwa na kiwango bora ndani ya siku chache zijazo."

## Barca yatoa ofa nono kwa Aubameyang

**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Arsenal imepewa ofa ya pauni milioni 50 na Barcelona ili wamuachie mshambuliaji wao, Pierre-Emerick Aubameyang wakati wa kipindi cha majira ya joto kijacho.

Mabingwa wa Hispania, Barcelona, ndio wanaohitaji saini ya mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Gabon.

Lakini, taarifa kutoka Emirates zinadai Arsenal ipo tayari kuzuia dili hilo lisifanyike licha ya mchezaji huyo kubakiza miezi 18 ya kuitumia timu hiyo.

Itakapofika mwishoni mwa msimu, Aubameyang atakuwa amebakiza mwaka mmoja wa mkataba na haonekani kama anaweza kusaini dili jipya.

Hilo likitokea na kwa umri wa mchezaji huyo, Arsenal haitakuwa na uhakika tena wa kupata ofa ya mkwanja mrefu kama huo na badala yake itamuuza kwa pesa ndogo itakayoipa shida kusajili mbadala wake.

Taarifa zinaeleza wazi na The Telegraph linasisitiza kuwa Barcelona inahitaji kusajili mshambuliaji haraka na harakati zote imezielekeza kwake.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SANCHO, HAALAND WAWEKA REKODI MPYA BUNDESLIGA

Tayari ameingia kwenye orodha ya wafungaji 10 kwenye ligi, lakini pia...

**DORTMUND, Ujerumani**

MAKINDA wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho na Erling Braut Haaland wote wameweka historia ya mabao wakati timu yao ikiibuka na ushindi mtamu dhidi ya Union Berlin.

Sancho mchezaji wa kimataifa wa England amekuwa kinda pekee kufunga mabao 25 kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, na kwenye mchezo huo yeye ndiye alikuwa wa kwanza kufunga bao la ufunguzi.

Mchezaji wa kimataifa wa Norway, Haaland sasa anakuwa ni mchezaji wa kwanza kufunga mabao saba katika mechi zake tatu za kwanza kwenye Bundesliga. Alifunga bao la pili na kufanya matokeo kusomeka 2-0 katika mchezo huo wa juzi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, alisajiliwa kipindi cha dirisha dogo la usajilila Januari akitokea Red Bull Salzburg na alifunga mabao matano katika mechi zake mbili za kwanza za Ligi Kuu ya Ujerumani.

Tayari ameiingia kwenye orodha ya wafungaji 10 kwenye ligi, akiwa amecheza dakika 136, baada ya kufunga mabao yake hayo saba.

"Ilikuwa ni siku ngumu leo (juzi), lakini lilikuwa jambo zuri kucheza kuanzia dakika ya kwanza," alisema Haaland akiiambia Sky Sports. "Kwa uhakika nimekuwa fiti zaidi, ingawa bado siko fiti kwa asilimia 100."

Makinda hao pia walihusika kwenye mabao mengine mawili ya Dortmund.

Sancho alimtengenezea krosi safi kiungo wa kimataifa wa Ubelgiji, Axel Witsel aliyefunga la nne.

Mchezaji huyo wa zamani wa Manchester City, Sancho sasa amefunga mabao tisa na kutengeneza pasi za mwisho saba katika mechi tisa zilizopita za Bundesliga.

Marco Reus alifunga bao jingine kwa Dortmund kwa mkwaju wa penalti, ambayo alizawadiwa Haaland.

Wachezaji wa mwanzo kufunga kwenye Bundesliga kabla hawajafikisha umri wa miaka 20, alikuwa Horst Koppel ambaye aliichezea Stuttgart miaka ya 1960 na kiungo wa sasa wa Bayer Leverkusen, Kai Havertz.

Kwingineko Bayern Munich ilipaa kileleni kwa msimamo baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Mainz shukrani kwa mabao ya Robert Lewandowski, Thomas Muller na Thiago, huku wapinzani wao, RB Leipzig wakitoka sare na Borussia Monchengladbach.

## KWA UFUPI

**BARCA KUMSAJILI WILLIAN**

KLABU ya Barcelona inakaribia kukubali kumsajili winga wa Chelsea, ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Brazil, Willian mwenye umri wa miaka 31, mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu. ***(Marca)***

**ARTETA AZUIA OZIL KUSEPA**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta alizuia usajili wa kiungo wa Ujerumani, Mesut Ozil mwenye umri wa miaka 31, kwenda kwenye klabu moja ya Qatar wakati wa dirisha dogo la usajili Januari. ***(90min)***

**UNITED, KOULIBALY KITAELEWEKA**

KLABU ya Manchester United wapo kwenye hatua nzuri katika jitihada zao za kutaka kumsajili beki wa Napoli, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 28. ***(Mirror)***

**MADDISON AWANIWA UNITED**

MANCHESTER United inamwania kiungo wa kimataifa wa England anayekipiga pale Leicester City, James Maddison mwenye umri wa miaka 23, pamoja na winga wa Borussia Dortmund, Mingereza Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 19, wakati wa dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto. ***(Standard)***

**ANCELOTTI AIONYA BARCA**

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti ameionya Barcelona kwamba watapoteza muda wao kama watatuma ofa nono kwa mshambuliaji wa kimataifa wa Brazil, Richarlison mwenye umri wa miaka 22, kipindi cha majira ya joto. ***(Star)***

**CHELSEA YAJITOSA KWA SANCHO**

KLABU ya Chelsea itajaribu kuipiku Manchester United katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Manchester City, Jadon Sancho. ***(Sun)***

**INTER YAMCHEFUA GIROUD**

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Ufaransa, Olivier Giroud mwenye umri wa miaka 33, alikasirishwa na miamba wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Inter Milan kwa kuamua kuachana na mpango wao wa kumsajili. ***(RMC, via Mail)***

**CAVANI AIDINDIA CHELSEA**

KLABU za Manchester United na Chelsea zilishindwa jaribio lao la kutaka kumsajili nyota wa Paris St-Germain, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 32, kwa sababu mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Uruguay moyo wake ulitaka ahamie Hispania. ***(Mirror)***

**TAKUMI AFUNGUKIA LIVER**

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Takumi Minamino raia wa Japan menye umri wa miaka 25, amesema klabu kadhaa za Ligi Kuu ya England zilikuwa zinamtaka pamoja na zile kutoka kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga. ***(Star)***

**ARSENAL YATAJIWA BEI YA PABLO**

KLABU ya Arsenal italazimika kulipa pauni milioni nane ili kugeuza usajili wa mkopo kwa beki wa Hispania, Pablo Mari mwenye umri wa miaka 26, na beki wa kulia wa Ureno, Cedric Soares mwenye umri wa miaka 28, ili kuwasajili moja kwa moja. ***(Star)***

**LEMAR AMULIKWA BAYERN**

Bayern Munich imejiweka sawa na uwezekano wa kwenda kumsajili kiungo wa Atletico Madrid, Mfaransa Thomas Lemar, 24. ***(France Football)***



## HABARI MICHEZO

# SVEN AMPONGEZA MGUNDA AKIKUBALI KIPIGO CHA SIMBA



**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji, Sven Vandenbroeck (pichani), alimsifu Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda kwa kukubali kushindwa, mpinzani wake huyo amesema kilichowaponza katika mechi hiyo ya juzi hadi kupoteza ni kukosa umakini kwa wachezaji.

Juzi katika Uwanja wa Taifa, Simba iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya 'Wagosi wa Kaya' hao, shukrani kwa kiungo Mbrazil Gerson Fraga aliyefunga yote mawili.

Kwa ushindi huo, Simba imezidi kujikita kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 47 baada ya mechi 18 wakati Coastal Union ambayo nayo imeshuka dimbani mara 18, ikibaki na alama zake 30.


Hata hivyo, baada ya mechi hiyo Mgunda alisema soka ni mchezo wa makosa na Simba imewaadhibu kutokana na makosa waliyoyafanya huku akiahidi kwenda kuyafanyia kazi ili kuyapunguza ama kuyamaliza kabisa.

"Mpira ni mchezo wa makosa, vijana wamepambana kwa kadri ya uwezo wao, lakini mwisho wa siku wamefanya makosa na wapinzani wetu wameyatumia kutuadhibu.

"Kwa sasa nitakwenda kuyafanyia kazi makosa hayo ili kuyapunguza ama kuyaondoa kabisa kabla ya mechi yetu ijayo," alisema.

Kwa upande wake, Sven mbali na kuwapongeza wachezaji wake kwa ushindi huo, pia alimpongeza Mgunda kwa kuonyesha uanamichezo kwa kukubali kipigo hicho huku akieleza akili zake sasa ni mchezo ujao dhidi ya Polisi Tanzania.

**MSHINDI...**



Mkurugenzi wa Masoko wa Zantel Tanzania, Sakyi Opoku (kulia), akitoa zawadi kwa mshindi wa jumla wa mashindano ya Zantel Monthly, Mug Femin Mabachi (katikati) yaliyofanyika mwishoni mwa wiki kwenye viwanja vya Lugalo jijini Dar es Salaam. Kushoto ni nahodha wa timu ya Lugalo Gofu ya Wanawake, Hawa Wanyenche. Mashindano hayo ya gofu yaliandaliwa na Kampuni ya Mawasiliano ya Zantel Tanzania. **MPIGAPICHA WETU**

## Chuoni yataka 3 za Selem View

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Chuoni imedhamiria kupata alama tatu katika mchezo wake wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya mapumziko ya kupisha usajili wa dirisha dogo.

Chuoni ambayo inawakaribisha Selem View kutoka Kisiwani Pemba itashuka katika Dimba la Mau A kwenye mchezo utakaopigwa leo majira ya saa kumi alasiri.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa Chuoni, Ramadhani Madundo alisema wamejiandaa vema kuhakikisha wanapata alama tatu muhimu katika mchezo huo.

Alisema hadi sasa kikosi chake Kipo vizuri na hakuna majeruhi, hivyo ana matumaini makub wa ya kupata ushindi na kuzidi kujikusanyia pointi katika mzunguko huu wa lala salama am bao kila timu inataka kupata matokeo mazuri.

Aidha, akizungumzia wapinzani wake timu ya Selem View kutoka Pemba, alisema anawaheshimu kutokana na kutambua wamejiimarisha zaidi katika dirisha dogo lililofungwa mwezi uliopita.

Timu ya Chuoni ipo nafasi ya tano ikiwa na alama 19 baada ya mzunguko wa kwanza huku Selem View ikiwa nafasi ya tisa na alama zake 13.

# Mvua yazibeba Prisons, Polisi Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Tanzania Prisons ya Mbeya na Polisi Tanzania zinazomilikiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani, jana ziliondoka na ushindi kwenye mechi zao za Ligi Kuu ambazo ziliahirishwa kuchezwa juzi jioni kutokana na mvua kubwa kunyesha jijini Dar es Salaam na Dodoma na kusababisha viwanja kujaa maji.

Mechi hizo zilizopigwa jana asubuhi, Prisons iliichapa KMC ya Kinondoni bao 1-0 kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, huku Polisi Tanzania ikiichapa JKT Tanzania bao 1-0 katika Uwanja wa Uhuru.

Prisons ambayo imekimbilia Dodoma na kuufanya Uwanja wa Jamhuri kuwa wake wa nyumbani badala ya Uwanja wa Samora Iringa iliyokuwa ikichezea kama uwanja wa nyumbani kwa muda, ilipata bao pekee dakika ya 22 likifungwa na straika wao mkongwe Jeremiah Juma dakika ya 22.

Timu hiyo yenye maskani yake mjini Mbeya, awali ilikuwa ikitumia Uwanja wa Sokoine mjini humo, lakini uli pigwa marufuku na Bodi ya Ligi, baada ya kuhar ibiwa kutokana na kutumiwa kwenye shughuli za tamasha la muziki.

Kwa matokeo hayo, timu hiyo imefikisha pointi 21 kwa michezo 17 iliyocheza, huku ikikamata nafasi ya 12.

Kwa upande wa KMC, imefikisha jumla ya pointi 17, kwenye michezo 17, huku pia ikiwa imecheza mechi 17.

Kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salam, Polisi Tanzania ikiwa ugenini iliibuka na ushindi wa bao 1-0, ikiwa ni mechi nyingine ambayo ilibidi ichezwe juzi, lakini ikaahirishwa kwa sababu ya mvua kubwa jijini Dar es Salaam.

Bao pekee lililoipa ushindi Polisi Tanzania lilifungwa na beki wa siku nyingi nchini, Jimmy Shoji.

Kwa matokeo hayo, timu hiyo inapaa mpaka kwenye nafasi ya saba, ikiwa imecheza mechi 17, na kujikusanyia pointi 27.

JKT Tanzania yenyewe iko kwenye nafasi ya nane ikiwa na pointi zake 26, baada ya mechi 17.

Michezo
Jumatatu Februari 3, 2020
Nipashe



Sancho, Haaland waweka rekodi mpya Bundesliga HABARI UK 30

# YANGA, MOLINGA SASA MWENDO WA KUDUNDA

●●●Mtibwa Sugar yalala ikimaliza mbwembwe za Morrison, Azam nayo yashikwa na Mbeya City kwa...

**Na Adam Fungamwango**

MKONGOMANI David Molinga, ameendelea kuwa shujaa kwa Yanga, baada ya jana kufunga bao pekee lililoipa pointi tatu dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye mechi ngumu ya Ligi Kuu, ikichezwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Ilikuwa ni dakika ya 51, alipounganisha krosi safi iliyochongwa na Ditram Nchimbi aliyeingia badala ya Mnyarwanda Patrick Sibomana.

Hilo linakuwa ni bao lake la sita msimu huu akiwa amewafikia Miraji Athumani wa Simba na Waziri Junior wa Mbao FC, lakini likiwa ni la pili mfululizo baada ya kuwa miongoni mwa wafungaji wakati wakiichapa Singida United 3-1 kwenye Uwanja wa Liti zamani Namfua, katika mechi iliyopita Januari 22.

Kwenye mechi hiyo ya jana, Mtibwa itabidi ijilaumu yenyewe kwa kushindwa hata kupata sare, kwani ilikosa mabao ya wazi dakika za mwishoni, kufuatia Ally Makarani akiwa na kipa Metacha Mnata kupiga shuti lililookolewa na kipa huyo dakika ya 71, huku Kibwana Shomari naye akiwa anatazamana na Metacha dakika ya 89, lakini alipiga shuti kubwa nje la lango.

Kabla ya hapo, Sibomana ambaye hakuwa kwenye kiwango chake cha kawaida, alikosa bao la wazi dakika ya 32 akiwa ana kwa ana na Shaaban Kado.

Yanga ilikosa bao la wazi dakika ya 36, baada ya faulo iliyopigwa na Haruna Niyonzima kumkuta Molinga aliyepiga shuti hafifu, lakini lilitemwa na kipa Kado na kuzua kizaazaa golini, kabla ya kuuwahi tena kuudaka.

Yikpe Gnamien, straika raia wa Ivory Coast aliikosesha Yanga bao la pili baada ya kuwatoka mabeki wa Mtibwa dakika moja tu kabla ya mechi kumalizika, lakini shuti lake la mguu wa kushoto lilipaa juu la lango.

Burudani nyingine kwenye mechi hiyo ni mchezaji Abdulhalim Humud kupewa kazi moja tu ya kutembea na winga machachari Benard Morrison na kuifanya kazi yake vema kiasi cha kutoonekana sana, wala kufanya mbwembwe zake kwenye mechi ya jana, kwani kila anapopasiwa, kiungo huyo mkabaji alikuwa ameshafika eneo la tukio na kutibua mipango kwa kumnyang'anya mpira, au kutumia nguvu zaidi.

Kwa matokeo hayo Yanga inafikisha pointi 31, ikiwa inakamata nafasi ya nne nyuma ya Namungo yenye pointi kama hizo 31, lakini ikiwa na faida ya uwiano mzuri wa mabao ya kufunga na kufungwa inayoshika nafasi ya tatu, Azam FC ambayo jana ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mbeya City ikishika nafasi ya pili kwa pointi zake 37, na Simba wakiwa kileleni na alama zake 47.

Hata hivyo, Yanga imecheza mechi 16, ikizidiwa mechi moja na Namungo, huku Simba na Azam zikiizidi kwa michezo miwili.

Mtibwa imebakiwa na pointi zake 23, ikikamata nafasi ya 10 kwa michezo 18 ambayo imecheza, ikiwa imebakisha mechi moja tu kumaliza mzunguko wa kwanza.




Mshambuliaji wa Yanga, David Molinga, akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao pekee wakati ikishinda 1-0 dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Taifa jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Samatta hesabu kwa Mourinho

**LONDON, England**

LICHA ya kutanguliwa kwa mabao mawili ndani ya dakika sita (dk. 37 na 44) kupitia kwa Philip Billing na Nathan Ake, Mbwana Samatta aliandika rekodi mpya akiifungia Aston Villa bao la kufutia machozi dhidi ya Bournemouth juzi wakati huu sasa akikisubiri kikosi cha Jose Mourinho, Tottenham.

**Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Dean Court zamani Vitality na Aston Villa kuchapwa mabao 2-1 , Samatta alitupia bao lake dakika ya 70, ambalo linamfanya kuwa mchezaji wa kwanza kufunga bao kwenye mechi ya kwanza ya Ligi Kuu England kwa Aston Villa tangu Rudy Gestede alipofunga Agosti 2015, pia dhidi ya Bournemouth.**

Lakini kwa hisani ya Samatta, Aston Villa imepata bao lake la kwanza kwa njia ya kichwa kwenye Ligi Kuu England tangu Ciaran Clark alipofunga dhidi ya Watford Aprili 2016.

Aidha, Samatta amekuwa mchezaji wa kwanza kutoka Tanzania kucheza Ligi Kuu England, wakati pia Tanzania ikiwa taifa la 117 tofauti kuwa na mchezaji mchezaji kwenye michuano hiyo.

Kocha wa Aston Villa, Dean Smith akizungumza baada ya mechi hiyo alisema: "Hatukucheza vizuri katika kipindi cha kwanza, ila kipindi cha pili baada ya [Jefferson Lerma] kutolewa kwa kadi nyekundu, ingawa hatukufanya vya kutosha kwa umiliki wetu."

Aston sasa itaikaribisha Tottenham katika Uwanja wa Villa Park Jumapili ya wiki ijayo, Februari 16 kwenye mwendelezo wa ligi hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >